**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Thelathini na Mbili - Tarehe 23 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya msiba tulionao, kwa kufiwa na mwenzetu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Kikao hakitaanza hivi sasa bali tutasitisha Shughuli za Bunge ili tuweze kwenda kutoa heshima zetu za mwisho kwa mwili wa Marehemu ambao utakuwa hapa katika sebule ya Wabunge, pale tunapochukulia barua zetu kwenye *pigeonhole* na baada ya hapo tutajitahidi kuharakisha kwa sababu safari ni ndefu, mwili wa Marehemu unakwenda Ifakara ni mbali, ratiba inaonesha wanaweza wakafika saa nne usiku.

Kwa hiyo, tutasitisha Shughuli za Bunge ili tusiwatese wenzetu kule wanaosubiri mwili wa Marehemu, Wapiga Kura, wanandugu, jamaa, isiwe usiku sana wakati wanapowasili. Kwa hiyo, nimewaomba wanaosimamia shughuli za kuleta mwili wa Marehemu wafanye haraka ili hivi nitakapositisha Shughuli za Bunge, tukute mwili wa Marehemu umeshafika, tutoe heshima zetu ili tuwawezeshe kuondoka mapema zaidi kuliko ilivyopangwa.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 5.00 asubuhi ambapo tutakuwa tumeishakamilisha hizo taratibu za kuaga mwili wa Marehemu.

*(Saa 3.03 asubuhi Bunge lilisitishwa kwa muda mpaka Saa 5.00 asubuhi ili kutoa heshima za mwisho kwa Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki)*

*(Saa 05.00 asubuhi Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla kikao hakijaanza, nieleze tu kwamba, kutokana na msiba uliotupata, zile shughuli zote za burudani zilizokuwa zimepangwa, moja leo jioni na nyingine kesho, zote sasa zimeahirishwa mpaka wiki ijayo. Hali kadhalika leo hatutakuwa na maswali, kwa hiyo, tutaanza na hoja moja kwa moja. Baada ya maelezo hayo, kikao kinaanza.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Chuo Kikuu Dar es Salaam kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report and Audited Accounts of the University of Dar es Salaam for the Year 2001/2002).*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa jana hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Ileje na kwa niaba yangu mwenyewe, naomba kutoa pole nyingi kwanza kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kutokana na kifo cha Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira. Pili, kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kutokana na kifo cha Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Tatu, napenda kuwapa pole Waheshimiwa Wabunge wote, waliopatwa na misiba katika mwaka wa Fedha wa 2003/2004. Mwenyezi Mungu, aendelee kuwapa subira na kuziweka mahali pema peponi roho za marehemu wote. *Amina.*

Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliopata ajali au kuvamiwa wakiwa njiani kuja Bungeni Dodoma. Naomba Mwenyezi Mungu, aendelee kuwalinda na kuwapa afya njema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge letu Tukufu mwaka wa Fedha wa 2003/2004. Pongezi maalum zimwendee Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, waliochaguliwa kutuwakilisha katika vikao vya Bunge la Afrika na *SADC,* Mashirika ya Elimu Afrika na Mazingira Duniani. Katika eneo hili pongezi maalum zimwendee Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara yangu katika kipindi chote cha mwaka 2003/2004. Pili, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa. Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa kuiongoza Kamati hii kwa mafanikio. Ushauri wa Kamati umeiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu na malengo yake kwa kipindi chote cha mwaka 2003/2004. Kipekee tumetambua na kuthamini sana mchango wao kwanza katika kushirikiana na wadau wakati wa kupitisha mabadiliko muhimu ya Sheria ya Ardhi mapema mwaka huu na pili, katika kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005. Tunatumaini na tunaomba ushirikiano huo uendelee katika kipindi chote cha uhai wa Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekwishaelezwa na kuzingatia misingi ya jumla ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Nawapongeza na kuwashukuru wote kwa hotuba zao nzuri. Kama ilivyo kawaida, baada ya kuzingatia misingi hiyo ya jumla, hoja yangu itajielekeza katika kuainisha kwa undani zaidi malengo na mikakati ya utekelezaji katika Sekta ya Ardhi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ambayo ni kusimamia Sera na Sheria za Ardhi zinazohusu utoaji, uhifadhi na utumiaji endelevu wa ardhi nchini. Kusimamia Sera na Sheria za uendelezaji makazi mijini na vijijini na kusimamia upimaji wa ardhi na utayarishaji wa ramani kwa matumizi mbalimbali. Majukumu mengine ni pamoja na kupima na kuhifadhi alama za mipaka kati ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo, kutafsiri mipaka ya maeneo mbalimbali ya kiutawala kama vile Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji ndani ya nchi yetu, kusimamia taaluma za Wizara na kuwaendeleza kitaaluma na kiutumishi Wafanyakazi wote wa Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2003/2004, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya Sh. 5,430,401,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2004, Wizara imekusanya Sh. 5,650,823,404.36/=, ambazo ni sawa na asilimia 104 ya lengo. Kati ya makusanyo hayo, Sh. 5,036,909,340/= ni kodi ya pango la ardhi itokanayo na viwanja na mashamba ambayo ni asilimia 89 ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha wa 2003/2004, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh. 5,448,928,900/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 600,000,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika tengeo la fedha za bajeti ya kawaida, Sh. 1,149,588,100/= zilitengwa kwa ajili ya mishahara na Sh. 4,299,340,800/= zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha hizi zilikuwa ni kwa ajili ya kutimiza malengo mbalimbali ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kama yalivyoainishwa kwenye hotuba yangu kwa mwaka wa Fedha wa 2003/2004 yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza mazungumzo na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa Serikali kugharamia ujenzi wa Jengo jipya la Ramani katika mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

(ii) Kuendeleza mazungumzo na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa kutunisha Mfuko wa *Plot Development Revolving Fund (PDRF),* utakaowezesha Wizara na Halmashauri kutwaa ardhi na kupima viwanja kwa lengo la kupunguza uhaba wa viwanja mijini.

(iii) Kutafuta Wahisani mbalimbali ili kugharamia utayarishaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima. Hii ni kwa sababu kazi hii inahitaji fedha nyingi, ambapo serikali pekee haiwezi kutekeleza kazi hiyo.

(iv) Kuanzisha utaratibu utakaowezesha Wananchi kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba.

(v) Kurekebisha Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* ili kuwabana wapangaji wasiolipa kodi za pango.

(vi) Kutoa elimu kwa umma juu ya Sera na Sheria za Ardhi kwa kuzingatia mkakati uliokubaliwa na Wadau Morogoro Mei, 2003 ili kuwafikia Wananchi wengi zaidi.

(vii) Kujenga mfumo wa Wizara ili kuunganisha mifumo iliyopo ya kila Idara kwa lengo la kurahisisha mawasiliano *(Ministry of Lands Information System - MOLIS).*

(viii) Kujenga uwezo wa kutumia teknolojia ya *satellite* katika kutengeneza ramani.

(ix) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Upimaji wa Viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam.

(x) Kuimarisha ofisi za Sekta ya Ardhi katika Halmashauri.

(xi) Kurekebisha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 ili kurahisisha taratibu za utoaji mikopo.

(xii) Kutekeleza Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002.

(xiii) Kuendeleza taaluma za watumishi.

(xiv) Kuwa na Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi na kuhuisha Sheria ya Mipangomiji.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2004, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina Sh. 5,712,638,868/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 584,064,708/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004 ni pamoja na:-

(i) Mazungumzo na Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa Serikali kugharamia ujenzi wa Jengo jipya la Ramani bado yanaendelea.

(ii) Mashauriano na Wizara ya Fedha kwa lengo la kutunisha mfuko wa *PDRF* ili kupunguza uhaba wa viwanja mijini yanaendelea

(iii) Serikali bado haijafanikiwa kupata wahisani wa kusaidia kugharamia utayarishaji wa ramani za msingi kwa nchi nzima. Wizara inaendelea kutumia rasilimali ndogo inayotolewa kutayarisha ramani kwa kiwango kidogo.

(iv) Upembuzi yakinifu *(Feasibility study)* unaohusu kuweka mazingira ambayo yatawezesha kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba umewasilishwa Serikalini kwa maamuzi.

(v) Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa Na. 2 ya Mwaka 1990, inafanyiwa marekebisho kwa lengo la kuboreshwa ili kuwadhibiti wapangaji wasiolipa kodi.

(vi) Mkakati wa Kitaifa ulioandaliwa kwa ajili ya kuelimisha umma kuhusu Sheria Mpya za Ardhi umeanza kutekelezwa.

(vii) Wizara imefanikiwa kuanzisha mifumo ya Kompyuta inayorahisisha mawasiliano, kubadilishana na kuhifadhi nyaraka.

(viii) Majaribio ya awali ya kutumia teknolojia ya *Satellite* katika kuhuisha ramani yamefanyika katika Miji ya Sengerema, Bariadi na Nansio.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ahadi zilizotolewa mwaka 2003, Wizara pia imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Upimaji picha *(Ground Photo Control)* wa miji 38 ya Kanda ya Ziwa Victoria.

(ii) Kupima mipaka ya vijiji 644 katika Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

(iii) Kutayarisha ramani zilizotumika kutoa vyeti vya ardhi katika vijiji saba Wilayani Mbozi na kutambua mashamba 1,400 katika kijiji cha Halungu na kutoa plani za hati za kimila.

(iv) Kukamilisha ramani ya mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya na kuongeza alama za mpaka kati ya Tanzania na Uganda.

(iv) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa kudhibiti mkondo wa mto Songwe na kusaini makubaliano kati ya Tanzania na Malawi ili kutekeleza usanifu wa kina.

(vi) Kuchapisha na kusambaza nakala za Sheria ya Mahakama za Ardhi, Na.2 ya Mwaka 2002 *(The Land Disputes Courts Act, 2002)* na Kanuni zake.

(vii) Kukarabati majengo kwa ajili ya Ofisi za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika ngazi za mikoa saba.

(viii) Kujenga Masjala za mfano za Usajili wa Hati ngazi ya Wilaya katika Wilaya za Iringa Vijijini na Mbozi na katika ngazi ya kijiji katika vijiji vya Kiwere (Iringa) na Halungu (Mbozi).

(ix) Marekebisho ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 yamefanyika na yamepitishwa na Bunge lako Tukufu.

(x) Elimu kwa umma iliendelea kutolewa.

(xi) Kuendelea na ulipaji fidia, kupima na kumilikisha viwanja na kutengeneza barabara katika maeneo ya mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam.

(xii) Mipango ya kimkakati ya Miji ya Songea, Kibaha, Vwawa na Tunduma imekamilika na mipango ya kuendeleza maeneo ya kati katika miji ya Tabora na Mbeya imekamilika.

(xiii) Rasimu ya Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Nyumba imekamilika.

(xiv) Uandaaji wa Kanuni za Ujenzi *(Building Regulations)* umekamilika na kuwasilishwa TAMISEMI kwa kutangazwa.

(xv) Usambazaji wa matokeo ya utafiti na utaalam wa ujenzi wa nyumba bora nchini umeongezeka.

(xvi) Rasimu za marekebisho ya Sheria ya Mipangomiji na Vijiji (Sura 378) na Muswada wa Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini zimekamilika.

(xvii) Jumla ya Watumishi 85 wa Serikali wamepatiwa mikopo ya nyumba kutoka Mfuko wa Mikopo ya Nyumba wa Serikali.

(xviii) Shirika la Nyumba la Taifa limeendelea na ujenzi wa nyumba za makazi na biashara katika Miji ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza.

(xix) Mafunzo ya kitaaluma yametolewa, mazingira ya ofisi yameboreshwa na watumishi wamepewa stahili zao.

(xx) Wizara imeendeleza vita dhidi ya rushwa na mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI.

(xxi) Mpango wa kutambua ardhi katika maeneo ya makazi yasiyopangwa Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kuyapa hadhi na kutambulika kisheria umeandaliwa.

(xxii) Uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi kwa Halmashauri mbalimbali umefanyika na Kamati hizo zinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyosababisha baadhi ya malengo ya Wizara kutofikiwa ni pamoja na:-

(i) Jengo lenye mitambo ya kutengenezea ramani ni bovu sana kwani lilijengwa tangu enzi za utawala wa Wajerumani. Ubovu huu unatishia usalama na mazingira yanayotakiwa katika kutunza na kutumia mitambo, zana na kompyuta zilizomo.

(ii) Uchakavu wa mitambo na uhaba wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa malighafi ya uchapaji wa ramani.

(iii) Uhaba wa ramani za msingi *(Base Maps),* kwa nchi nzima ili kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi na upimaji wa viwanja na mashamba.

(iv) Ukosefu wa fedha za kuwekeza katika sekta ya ardhi kwa ajili ya kulipa fidia wakati wa utwaaji wa ardhi.

(v) Uhaba wa vitendea kazi na nafasi za ofisi kwa watendaji.

(vi) Ukosefu wa utaratibu/mfumo wa kuwawezesha Wananchi kupata mikopo ya kujenga/kununua nyumba za kuishi.

(vii) Mipaka kati ya nchi yetu na nchi jirani kutotambulika kutokana na alama kuharibika, kung'olewa au kuwa mbali mbali sana.

(viii) Ufinyu wa rasilimali za kuwezesha kueneza elimu ya sheria za ardhi.

(ix) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoundwa kwa wakati kutokana na utata wa kisheria na matatizo ya utendaji yaliyojitokeza.

(x) Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hayajaweza kuanza kazi zake za utatuzi wa migogoro ya ardhi.

(xi) Halmashauri nyingi hazijaajiri wataalam wenye sifa za kusimamia na kutoa huduma za ardhi. Aidha, ofisi za ardhi kwenye Halmashauri hizo hazipewi kipaumbele katika kugawiwa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na matatizo haya Wizara imeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Ili kupunguza tatizo la upungufu wa fedha za fidia, Serikali inatafakari uwezekano wa kuruhusu fedha kiasi cha Sh 8,959,113,000/= ambazo ilizitoa kwa ajili ya

kupima viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam ziwekwe katika Mfuko wa *Plot Development Revolving Fund (PDRF).*

(ii) Mazungumzo na wahisani mbalimbali bado yanaendelea ili kupata fedha za kutayarisha ramani za msingi kwa nchi nzima.

(iii) Kutokana na ufinyu wa bajeti yake ya matumizi mengineyo, Wizara itajitahidi kupunguza tatizo la uhaba wa vifaa hivyo kwa kutumia fedha za Matumizi Mengineyo *(Other Charges)* kununua vitendea kazi kwa awamu.

(iv) Wizara inatumia mtaalam mwelekezi kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa kutekeleza Sheria za Ardhi na ya Mahakama za Ardhi.

(v) Suala la mipaka ya nchi linatatuliwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

(vi) Kuandaa utaratibu kwa kushirikiana na TAMISEMI ili kuhakikisha Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yanafanya kazi.

(vii) Kutambua ardhi na kutoa leseni za makazi katika maeneo yasiyopangwa ili kufufua mitaji mfu kuwa hai hivyo kuwawezesha wananchi wenye ardhi hiyo kuitumia kwa ajili ya kujipatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2004/2005, unatoa kipaumbele kwa maeneo makuu matatu ambayo yanaweza kuwa kichocheo kikuu cha kuwaletea Watanzania maendeleo. Kwanza, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Pili, kuwawezesha wananchi kutumia rasilimali ya ardhi ili kuwaondolea wananchi umaskini, na Tatu, kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Ardhi ili kutoa uhakika wa miliki za ardhi sambamba na kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini. Katika kutekeleza maeneo hayo matatu ya kipaumbele Wizara itaendelea na mikakati iliyojiwekea katika mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara imejiwekea lengo la kukusanya jumla ya Sh. 5,896,650,000/= kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato. Aidha, nakusudia kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Sh. 5,690,672,400/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 673,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, Sh. 73,000,000/= ni kwa ajili ya kupambana na janga la UKIMWI kwa wafanyakazi wa Sekta ya Ardhi. Maelezo ya kina kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali yamefafanuliwa kwa kila Idara kama inavyoelezwa hapa chini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara iliendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi zenye misingi na lengo la kuimarisha utawala bora ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini. Huduma hizo ni pamoja na kutoa

miliki za ardhi, utwaaji ardhi kwa manufaa ya Umma, utatuzi wa migogoro ya ardhi, usajili wa hati miliki pamoja na nyaraka mbalimbali, kutoa vibali vya uwekaji rehani hakimiliki za ardhi na uhamisho wa miliki, uthamini wa mali na kutoa elimu kwa umma kuhusu Sheria mpya za Ardhi.

Pia, Wizara iliendelea kuchapisha na kusambaza fomu za aina mbalimbali kwa ajili ya umilikishaji ardhi kwenye Halmashauri. Aidha, Wizara inatekeleza mkakati maalum wa kuboresha mfumo wa utoaji huduma za ardhi kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Pamoja na kutoa huduma hizo Wizara iliendelea na ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara ilikamilisha utwaaji wa ardhi na ubatilisho wa miliki wa jumla ya viwanja na mashamba 239. Utwaaji huo wa ardhi ulihusisha viwanja na mashamba yaliyopo katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam, Arusha, Manyara na Morogoro.

Aidha, katika kutekeleza Sheria Mpya za Ardhi madaraka ya kugawa ardhi yamekwishapelekwa kwenye Halmashauri.

Hata hivyo, Wizara inaendelea na jukumu la kushughulikia maombi ya viwanja kwa ajili ya Balozi mbalimbali, maeneo ya uwekezaji chini ya Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Centre - TIC)* na maeneo ambayo matumizi yake ni ya manufaa kwa Taifa kama viwanja vya ndege na migodi. Ili kuziwezesha Halmashauri kutekeleza jukumu la kugawa ardhi, Wizara yangu imekamilisha uteuzi wa Kamati za Kugawa Ardhi kwa Halmashauri 104 na ambazo zimeanza kufanya kazi.

Pamoja na uteuzi huo bado Halmashauri za Manispaa ya Morogoro, Mji wa Lindi, Wilaya za Nachingwea, Ruangwa, Chunya, Kisarawe, Mpanda, Nkasi, na Sikonge, hazijapendekeza majina ya wajumbe wa kamati hizo. Natoa wito kwa Halmashauri hizo wafanye hivyo mara moja ili waweze kutekeleza jukumu la kugawa ardhi kwa mujibu wa sheria.

Aidha, ninakumbusha kuwa usimamizi na uendeshaji wa masuala ya ardhi unahitaji utaalam. Hivyo, nasisitiza kuwa Halmashauri zote nchini zihakikishe zinaajiri Maafisa Ardhi wenye sifa zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na jukumu lake la kukamilisha taratibu za uandaaji wa hati miliki za ardhi zilizowasilishwa kutoka Halmashauri mbalimbali na ambazo zimetayarishwa Wizarani. Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004, jumla ya hati 13,424 zilisainiwa. Kati ya hizo hati 3,706 zilitoka Halmashauri na 9,718 ziliandaliwa Wizarani chini ya mradi wa viwanja 20,000 Dar es Salaam. Kutokana na takwimu hizi idadi ya hati zinazoandaliwa katika Halmashauri ni chache mno ukilinganisha na idadi ya viwanja vilivyopimwa na kumilikishwa katika Halmashauri hizo. Kwa sababu hiyo, napenda kusisitiza Halmashauri ziongeze kasi za uandaaji wa hati. Katika kipindi hicho, Wizara pia ilifanya ukaguzi wa viwanja na uhakiki wa miliki kwa lengo la kujenga kumbukumbu sahihi za ardhi, ili zisaidie kutatua migogoro ya

miliki za ardhi na kufanya maamuzi mbalimbali. Wizara ilikagua eneo la Tegeta Jijini Dar es Salaam ambapo viwanja 2,594 vilihakikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004, Hati za kumiliki ardhi 11,558 zilisajiliwa. Nyaraka 5,854 zinazohusiana na hatimiliki pia zilisajiliwa. Nyaraka nyingine zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka ni 4,001. Dhamana 544 za mali zinazohamishika zilisajiliwa. Ingawa kuna ongezeko katika hati zilizosajiliwa na kutumika kama dhamana ukilinganisha na mwaka 2003 bado Wananchi walio wengi hawatumii hatimiliki kama dhamana ya kujipatia mitaji. Natoa msisitizo kuwa wakati Wizara inaongeza juhudi katika kutoa hatimiliki wananchi watumie hatimiliki zao kwa ajili ya kujipatia mitaji.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2002/2003, nilizungumzia kuhusu uanzishwaji wa huduma ya Usajili wa Hati za Kimila ngazi ya Wilaya na Kijiji. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imejenga na kufungua Masjala ya Ardhi za mfano katika Wilaya ya Mbozi na Masjala ya Ardhi ya Kijiji cha Halungu. Lengo la kujenga masjala hizo za mfano ni kuzihamasisha Halmashauri za Wilaya na vijiji ili nazo zijenge masijala kama hizo kwa kuwa jukumu hilo ni la Halmashauri. Masjala hizo zitawawezesha wananchi kupata hati za kumiliki ardhi kimila na hatimaye kutumia hati hizo kama dhamana ya kujipatia mitaji.

Sambamba na ufunguzi wa masjala hizo, Wizara pia iliiwezesha Wilaya ya Mbozi kusajili na kutoa Vyeti vya Ardhi kwa Vijiji saba ambavyo ni Halungu, Halambo, Malolo, Shasya, Ibembwa, Msia na Iganduka. Pia, hati za kumiliki ardhi kimila zimesajiliwa na kutolewa kwa Wanavijiji katika kijiji cha Halungu. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa masjala nyingine ya mfano katika Wilaya ya Iringa na katika kijiji cha Kiwere wilayani humo unaendelea. Ningependa kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Halmashauri zote kuchukua jukumu la kujenga masjala za ardhi za Wilaya na Vijiji ili wananchi waweze kupata hati za kumiliki maeneo yao na hivyo kuwa na uhakika wa miliki zao. Wizara iko tayari kutoa ushauri katika kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara yangu ilikamilisha utoaji vibali vya uhamisho na uwekaji rehani kwa hati 1,796 za kumiliki ardhi. Aidha, kutokana na hoja za Wadau mbalimbali kwamba sheria za ardhi ni kikwazo katika kutoa mikopo, Wizara iliwasilisha Bungeni Muswada wa kurekebisha sheria hiyo na Bunge lako Tukufu likapitisha marekebisho hayo kwa *The Land (Amendment) Act, 2004* mwezi Februari, 2004. Kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaandaa Kanuni *(Regulations)* za kutekeleza marekebisho hayo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2004, Wizara imethamini nyumba 433 ambazo zilitozwa ada ya uthamini ya Sh. 12,365,858/=. Aidha, Wizara ilipokea na kupitisha jumla ya taarifa za uthamini 1,712 kutoka makampuni binafsi na kutoza ada ya uhakiki *(Approval Fee)* ya Sh. 113,713,415.95/=. Pia, ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi kwa matoleo mapya ya viwanja na mashamba 168 ulifanyika. Vile vile, Wizara

yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa imethamini nyumba ambazo zinatarajiwa kununuliwa au kuuzwa na Balozi zetu huko London (Uingereza), Berlin na Bonn (Ujerumani), Nairobi (Kenya), Pretoria (Afrika Kusini), Lusaka (Zambia), na Washington (Marekani).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilikuwa na jukumu la kukamilisha uandaaji wa mapitio ya viwango vya kodi ya viwanja nchini ili kuboresha makusanyo ya kodi ya pango la ardhi. Zoezi hili limekamilika na kijitabu cha viwango kitachapishwa tayari kwa usambazaji kwa Halmashauri zote. Aidha, utaratibu wa kukadiria kodi ya pango la ardhi ya viwanja vya ndege nchini nao umekamilika, hivyo kuwezesha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kutayarishiwa Hati za kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara yangu iliendelea na programu ya kutoa elimu kwa umma kwa njia ya redio, televisheni na makala katika magazeti mbalimbali, semina pamoja na kushiriki maonyesho ya Sabasaba. Wizara iliandaa na kusambaza nakala 5,000 za jarida la Wizara na vipeperushi 51,000 vinavyoelezea huduma mbalimbali zitolewazo na Wizara ya Ardhi. Aidha, vitabu 3,000 vya Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na nakala 3,000 za Kanuni zake zimechapishwa. Tangu sheria hizo zilipoanza kutekelezwa hadi sasa Wizara imekwishasambaza vitabu 9,300 vya Sheria za Ardhi na Kanuni 10,000 za sheria hizo. Aidha, nakala 30,000 za Mwongozo wa Kufundishia Sheria ya Ardhi ya Vijiji zilichapishwa na kati ya hizo nakala 24,000 zilisambazwa. Nakala za vitabu hivyo zimesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Sekta ya Ardhi, Viongozi mikoani na wilayani na katika Halmashauri, Watendaji wa Kata, Serikali za Vijiji, Ofisi mbali mbali za Serikali na asasi zisizo za kiserikali. Pia, Wizara imeandaa Mwongozo wa kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo sasa tunayo miongozo ya kutoa elimu ya sheria za ardhi kwa sheria zote mbili. Vile vile, Wizara imekuwa ikielimisha wananchi kupitia mikutano na waandishi wa habari kuwaelezea Sheria Mpya za Ardhi na mambo mengine muhimu yanayotekelezwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kutoa elimu na kuboresha utendaji, watumishi wote wa Wizara wamepatiwa elimu ya Sheria Mpya za Ardhi na kugawiwa nakala za vitabu vya sheria hizo, Kanuni zake pamoja na Mwongozo wa kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Aidha, wakati wa kuanzisha masjala za ardhi za mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, nilioueleza awali, elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999 ilitolewa kwa Viongozi wa Mkoa wa Mbeya, Halmashauri zote za Mkoa huo na Wananchi kwa jumla katika vijiji saba katika Wilaya ya Mbozi. Pia, walipatiwa vitabu vya Sheria, Kanuni na Mwongozo wa kutoa elimu ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ilitoa elimu ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999 kwa Maafisa Watendaji Kata 788 na hivyo kufanya jumla ya maafisa hao waliopata elimu hiyo kuwa 2,408 kwa nchi nzima. Vile vile, viongozi 72,000 wa Serikali za Vijiji kutoka mikoa yote 21 ya Tanzania Bara walipatiwa mafunzo. Katika mwaka 2004/2005, juhudi zitaendelea kutoa elimu kwa watendaji kata 224 waliobaki, viongozi

na watendaji wa Halmashauri za Miji, Wilaya, Kata na Vijiji. Napenda kuishukuru TAMISEMI na Asasi zisizo za Kiserikali kama *Tanzania Home Economics Association (TAHEA)* na *Women Advancement Trust (WAT),* kwa kuendelea kutoa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali nchini. Ninawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza Sera na Sheria hizo kwani kazi bado ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, utekelezaji wa Sheria za Ardhi na ya Mahakama za Ardhi unahitaji programu maaalum na hasa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ambayo inaitaka Serikali kuitekeleza Sheria hiyo katika vijiji visivyopungua 10,000 kote nchini. Hii ni programu kubwa inayohitaji mkakati maalum. Kutokana na hilo Serikali imepatiwa msaada kutoka Kamisheni ya Umoja wa Ulaya *(Commission of the European Union)* wa kutayarisha mkakati wa utekelezaji. Mkakati huo utakapokamilika, utasaidia kubainisha mambo muhimu yanayopaswa kutekelezwa katika Sheria hiyo, gharama zake na muda wa utekelezaji. Napenda kutoa shukrani kwa Umoja wa Ulaya kwa kutoa msaada huo. Naziomba taasisi za kiserikali na asasi mbalimbali zisizo za kiserikali kushirikiana na Wizara yangu katika kuutekeleza mkakati huo pindi utakapokamilika. Elimu kwa umma inayoendelea kutolewa inalenga kuhamasisha wananchi kutambua haki na wajibu wao ili hatimaye waweze kunufaika na huduma zitolewazo na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imedhamiria kubadilisha mfumo wa kuhifadhi kumbukumbu zake kwa kutumia mifumo ya Kompyuta kama njia muafaka ambayo itarahisisha utendaji kazi wa kila siku na kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi. Matumizi ya mifumo ya kompyuta yanategemea usahihi, uimarishaji na upatikanaji wa kumbukumbu hizo. Tayari Wizara imeanza kutumia kompyuta katika umilikishaji na uandaaji wa hati za viwanja. Aidha, Wizara imefanikiwa kuwa na mifumo ya kompyuta ambayo inasaidia kufuatilia barua za wananchi, mienendo ya majalada ya viwanja, plani za upimaji na ukadiriaji wa kodi za ardhi. Juhudi hizi zote zinalenga kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi ili kupunguza kero ambazo zilikuwa zinasababishwa na mifumo ya zamani.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kutambua na kuweka kumbukumbu za Ardhi liliendelea na hadi kufikia Juni, 2004, jumla ya wamiliki 52,045 wa viwanja na mashamba walitambuliwa katika mkoa wa Dar es Salaam na kati ya hao, wamiliki 37,704 wana hati miliki. Katika Ofisi za Kanda za Usajili wa Hati za Mwanza na Moshi, zilitambuliwa hati 27,845 na zote zimehifadhiwa kwenye kompyuta. Vile vile, majalada ya viwanja 152,826 yaliyopo katika masijala ya Wizara yalipigwa picha na kuhifadhiwa kwenye kompyuta. Aidha, hadi Juni, 2004, ujenzi wa jengo la Idara inayoshughulikia uwekaji wa kumbukumbu na mawasiliano ulikuwa umekamilika kwa asilimia 80.

Katika mwaka 2004/2005, Wizara ina mpango wa kuunganisha Ofisi za Ardhi Mkoa wa Dar es Salaam kwenye mtandao wake, kuanzisha tovuti itakayowezesha Ofisi za Ardhi za Halmashauri za Miji na Wilaya kuwasiliana na Makao Makuu, kupiga picha hati katika Ofisi ya Usajili Kanda ya Mashariki na kuimarisha mifumo ndani ya Wizara kwa lengo la kuwa na mfumo mmoja. Ofisi za kanda zilizobaki za Mbeya, Dodoma na Mtwara kazi itaendelea mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mahakama za Ardhi Na. 2 ya Mwaka 2002, *The Land Disputes Courts Act, 2002* ilianza kutumika tangu tarehe 1 Oktoba, 2003. Hata hivyo, Mabaraza ya Ardhi na Nyumba hayakuweza kuundwa kutokana na matatizo ya kiutendaji na kisheria. Tatizo la kiutendaji lilihusu namna ya kuwapata wanasheria ambao ndio wanaotakiwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Mabaraza. Hili lilionekana kuwa tatizo kwa sababu wanasheria wengi wanapenda kujiajiri au kutafuta ajira katika makampuni kwa kufuata maslahi bora. Aidha, kifungu cha Sheria kinachohusu kiapo cha Mwenyekiti wa Baraza, kilionekana kuwa na utata. Kuhusu maslahi, uchambuzi umefanyika na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imekubali kuweka ngazi maalum ya mshahara wa Wenyeviti wa Mabaraza. Kuhusu tatizo la kisheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameliomba Bunge lako Tukufu na limekubali kukifanyia marekebisho kifungu cha kiapo cha Mwenyekiti. Kufuatia ufumbuzi wa matatizo haya Wizara inalenga kuunda jumla ya Mabaraza 23 na katika kila mkoa litaundwa Baraza moja isipokuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam ambapo yataundwa matatu, moja katika kila Manispaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya maandalizi mengine ya utekelezaji wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002. Ukarabati wa Ofisi za Mabaraza katika Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Dodoma, Morogoro, Mbeya, Tanga, Kilimanjaro pamoja na Manispaa ya Temeke umekamilika. Wizara bado haijapata ofisi katika Mkoa wa Manyara na Manispaa ya Kinondoni. Kwa sababu hiyo, naomba ushirikiano wa viongozi wa Mkoa na Manispaa husika ili zipatikane Ofisi za Baraza, kwa sababu maeneo haya mawili ni miongoni mwa maeneo yenye migogoro mingi nchini. Wizara imechapisha nakala 10,958 za Sheria na zimegawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Watendaji wa Sekta ya Ardhi katika Halmashauri za Miji, Manispaa, Wilaya na Watendaji wa Kata. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara yangu itaendelea kusambaza nakala za Sheria hiyo kwa vijiji vyote Tanzania Bara na kuandaa mwongozo wa kuwaelimisha viongozi wa Halmashauri na wananchi juu ya Sheria Namba 2 ya Mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi na Mabaraza ya Nyumba katika ngazi ya wilaya/mkoa na rufaa, yameendelea kukamilisha utatuzi wa migogoro iliyokuwepo kabla ya Sheria Na. 2 ya 2002. Katika kipindi hiki cha mpito, mabaraza yamesuluhisha na kuamua mashauri 1,215 ya ardhi na 837 ya nyumba. Jumla ya mashauri 1,646 ya ardhi na 464 ya nyumba yanaendelea kushughulikiwa kati ya hayo mengi yapo katika mikoa ya Arusha, Dar es salaam na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa migogoro mingi ya ardhi ipo vijijini, Serikali imeweka mfumo mpya wa utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba unaoanzia ngazi ya Kijiji. Mfumo huu unalenga kutatua migogoro kwa muda mfupi, kwa kutumia taratibu rahisi na shirikishi zisizo na gharama kubwa. Pamoja na nia hii nzuri, hadi sasa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji hayajaundwa na Mabaraza ya Kata hayajafufuliwa, hii imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuunda Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na kufufua Mabaraza ya Kata kote nchini. Ningependa kusisitiza umuhimu wa Halmashauri kuanzisha na kuyaendesha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Aidha, Mabaraza ya Kata yanayoundwa chini ya Sheria Na. 7 ya Mwaka 1985 ambayo

hayafanyi kazi yafufuliwe na yatatue migogoro ya ardhi na nyumba kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002. Kwa kuwa suala la kudumisha amani nchini ni jukumu la kila mtu, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutoa elimu ya Sheria ya Mahakama za Ardhi kwa Wananchi, Watendaji wa Vijiji na Kata kwa kutumia mwongozo ambao umeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali na Wananchi wanatambua kuwa ardhi ni rasilimali kuu ya maendeleo. Ili kuitumia vizuri rasilimali hii, ni sharti kujenga kumbukumbu kamili, sahihi na hakika kuhusu ardhi yote ya nchi na jinsi inavyotumika wakati hadi wakati. Nchi nyingi zilizoendelea duniani ziliandaa kwanza kumbukumbu za ardhi zao ndipo zikawa na mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi. Kumbukumbu za ardhi zinawezesha usimamizi bora wa mipango ya maendeleo ya kitaifa, ulinzi wa mazingira bora, upatikanaji wa dhamana, uhamasishaji wa uwekezaji, ukusanyaji mapato na kwa jumla, kupiga vita umaskini. Gharama ya kazi hii Kitaifa ni kubwa na inahitaji muda mrefu na rasilimali nyingi lakini ni muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Katika zama hizi za utandawazi, kumbukumbu sahihi za ardhi ni anwani ya msingi ya kiuchumi nje na ndani ya nchi. Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri zote nchini kubuni mradi wa kutambua kila kipande cha ardhi ili kuwezesha upangaji wa matumizi bora ya ardhi na kutoa hati miliki inayotambulika kwa mujibu wa Sheria za Ardhi Na. 4 na 5 za Mwaka 1999. Ni nia ya Wizara yangu, kuanzia mwaka huu, kufanya kidogo kidogo utambuzi wa ardhi yote isiyopimwa, hasa katika maeneo ya miji, na kwa kuanzia na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya teknolojia za kisasa katika kazi za Upimaji na Ramani yameongeza ufanisi kwa kiwango kikubwa. Mwaka jana Wizara iliendelea kupima viwanja zaidi katika mradi wa viwanja 20,000 Dares salaam. Iliwezekana kufanya Upimaji Picha *(Ground Photo Control),* kwa ajili ya utayarishaji wa ramani za miji 38 katika kanda ya Ziwa Victoria. Upimaji ulifanyika na kufufua sehemu ya mpaka kati ya Tanzania na Uganda yenye urefu wa kilomita 110 kwa muda wa miezi 5 tu, kazi ambayo ingechukua miaka 2 kwa kutumia mbinu na teknolojia ya zamani. Ni nia ya Wizara yangu sasa kupanua na kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa ili kuongeza ufanisi na tija katika kutambua miliki za wananchi mijini na vijijini, upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani.

Mheshimiwa Spika, tatizo la upatikanaji wa viwanja katika Jiji la Dar es Salaam umepungua sana baada ya Wizara yangu, ikishirikiana na Halmashauri za Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, kufanya upimaji wa viwanja 27,460 chini ya Mradi wa Kupima Viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Idadi ya viwanja vinavyopimwa katika Halmashauri bado ni ndogo. Uzalishaji wa viwanja nchini ungeweza kuwa mkubwa kama matatizo yanayozikabili Halmashauri nyingi katika utoaji huduma za ardhi yangepatiwa ufumbuzi. Baadhi ya matatizo hayo ni ukosefu wa fedha za kutosha kulipa fidia ili kuwezesha kutwaa ardhi ya kupima viwanja, teknolojia duni, ajira ndogo ya wataalam wa fani ya upimaji, zaidi ya Halmashauri 48 kati ya 113 nchini hazijaajiri Wapima Ardhi wenye sifa zinazotakiwa na ofisi duni za upimaji ardhi ambazo hazikidhi mahitaji ya

wataalam na vifaa vya kazi. Wizara ilichukua jukumu na kugharimia matengenezo ya vifaa 47 vya upimaji ardhi na pia kushauri Halmashauri zifanye ajira za wapima ardhi wenye sifa kwa lengo la kuimarisha huduma za upimaji ardhi katika Halmashauri nchini. Ulipaji fidia na utwaaji ardhi kwa utaratibu wa sheria ni muhimu sana kabla ya kupima na kuendeleza makazi bora nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa viwanja vilivyopimwa, hasa mijini, Serikali iliamua kuanzisha Mfuko Maalum wa Kupima Viwanja *(The Plot Development Revolving Fund - PDRF).* Lengo la Mfuko huu ni kutoa fedha, kwa njia ya mikopo, kwa Halmashauri ili ziweze kupima viwanja vingi kukidhi mahitaji. Mfuko huu unaendeshwa kwa ufanisi mdogo kutokana na sababu mbili kubwa. Kwanza ni kutokana na mtaji mdogo wa Mfuko na pili ni Halmashauri zilizopewa fedha kutorudisha fedha hizo. Mpaka sasa Wizara imekwishatoa jumla ya Sh. 550,216,111/= kwa waombaji 33 na bakaa ya maombi yaliyopo ni 20 yenye jumla ya Sh.4,016,931,466/=. Kati ya mikopo iliyotolewa, fedha iliyokwisharudishwa ni Sh. 21,796,700/= tu. Napenda kutumia nafasi hii kuzishauri Halmashauri zote nchini kutumia Mfuko huu ipasavyo na ziwepo juhudi za kurejesha fedha ili Mfuko uweze kuzunguka. Aidha, maandiko ya Mradi yabainishe njia za urejeshwaji ikiwa ni pamoja na ziada inayowezesha Mfuko kujenga mtaji wake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mradi wa Upimaji Viwanja 20,000 Dar es Salaam umedhihirisha kwamba, kikwazo kikubwa cha upatikanaji viwanja mijini ni ukosefu wa maeneo yaliyo huru kwa ajili ya kupima viwanja. Aidha, imedhihirika kuwa fedha zinazotumika kuzalisha viwanja zinaweza kurejeshwa kutoka kwa wananchi wanaomilikishwa viwanja. Hadi sasa viwanja 27,460 vimepimwa na kukamilika katika maeneo tisa ya mradi ambayo ni Tuangoma, Kisota, Mbweni kuelekea Mto Mpiji, Buyuni, Mbweni JKT, Mtoni Kijichi, Bunju, Mwanagati na Mivumoni. Upimaji katika maeneo ya Boko Dovya na Vijibweni haujatekelezwa kutokana na migogoro iliyojitokeza. Viwanja viligawiwa kupitia Kamati za Kugawa Viwanja za kila Manispaa mara upimaji wa eneo ulipokamilika. Zoezi la kumilikisha viwanja linakwenda sambamba na usajili wa hati za viwanja hivyo. Hadi sasa hati 7,565 zimeshasajiliwa na hati 2,176 ziko katika hatua mbalimbali za utayarishaji.

Mheshimiwa Spika, gharama ya utekelezaji wa mradi huu ilikadiriwa kuwa Sh. 21 bilioni lakini Serikali ilitoa mkopo wa Sh. 8.9 bilioni tu. Ili kukamilisha mradi, Serikali iliruhusu kuzungusha fedha zilizorejeshwa kutokana na mauzo ya viwanja. Hadi sasa gharama ya mradi imefikia Sh. 19.53 bilioni na marejesho yaliyopatikana ni Sh. 17.3 bilioni. Uzoefu uliopatikana katika mradi huu utawezesha kubuni na kutekeleza miradi ya aina hii katika miji mingine nchini pindi fedha ikipatikana.

Hadi mwisho wa mwaka 2003/2004, mradi huu umemilikisha jumla ya viwanja 13,949 katika maeneo yote ya mradi ambamo viwanja vimepimwa. Kati ya hivyo, viwanja 4,179 au asilimia 30 vimemilikishwa kwa wanawake, viwanja 6,978 au asilimia 50 kwa wanaume, viwanja 438 au asilimia 3 vimemilikishwa kwa pamoja kwa mume na mke na vilivyobaki 2,354 au asilimia 17 vimemilikishwa kwa taasisi mbalimbali. Hii inadhihirisha kuwa wanawake wanapata haki kama ilivyo kwa wanaume katika kumilikishwa viwanja nchini kama hali hii ilivyo na inavyozidi kujitokeza. Wizara

yangu inawahimiza wananchi wa jinsia zote kuomba viwanja po pote nchini kwa madhumuni ya kumilikishwa, kwa mujibu wa Sheria za Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kurahisisha uwekezaji nchini, Serikali inaendelea na uanzishaji wa Hazina ya Ardhi *(Land Bank),* kwa lengo la kutenga na kuwapatia wananchi, pamoja na wawekezaji wenye mitaji mikubwa, maeneo kwa ajili ya uwekezaji. Maeneo hayo yatapimwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na yatatumika kwa shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, viwanda na uchimbaji madini. Kati ya hekta milioni 4.1 zilizotambuliwa mwaka 2002/2003 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, uchambuzi umebaini kuwa kuna vipande vya ardhi 743 vyenye jumla ya ukubwa wa hekta milioni 3.1 ambavyo vinafaa kwa uwekezaji. Kati ya vipande hivyo, vipande 357 vyenye jumla ya hekta 695,987 tayari vimepimwa na vipande 386 vyenye jumla ya hekta milioni 2.4 havijapimwa. Vipande vya ardhi vilivyopimwa bado vinahakikiwa ili kubaini wamiliki wake na baadaye vitakabidhiwa Kituo cha Uwekezaji cha Taifa na hivyo kuingizwa kwenye Hazina ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ilifanya upigaji picha wa wilaya yote ya Mbozi katika mwaka 1998/99. Picha hizo zimetumika kutambua na kupima mipaka yote ya vijiji 171 vya wilaya hiyo. Katika vijiji 12, mipaka ya mashamba zaidi ya 12,000 imetambuliwa. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kazi ya upimaji mipaka vijiji kwa *Global Positioning System (GPS)* iliendelea katika Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro. Jumla ya vijiji 799 vimepimwa, ikijumuisha vijiji 95 katika Mkoa wa Manyara, vijiji 255 katika Mkoa wa Arusha, vijiji 425 katika Mkoa wa Kilimanjaro, vijiji 19 katika Mkoa wa Ruvuma na vijiji 5 katika Mkoa wa Iringa. Kazi ya baadaye itakuwa kutambua na kuweka kumbukumbu za miliki ya ardhi ndani ya kila Kijiji. Katika mwaka huu wa fedha wizara yangu itaendelea na upimaji wa mipaka ya vijiji katika Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya na utambuzi wa miliki za mashamba katika vijiji vya wilaya ya Mbozi. Lengo la upimaji wa mipaka ya Vijiji ni kujenga mazingira ya usalama wa miliki za Ardhi katika Vijiji.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inayoikabili sehemu ya Hydrographic Surveys ni kujenga uwezo wa kupata vitendea kazi, kutoa mafunzo kwa wataalam na kujenga ofisi. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, kamati ya kitaifa itakayokuwa inaishauri Serikali juu ya masuala ya kiufundi katika upimaji majini na utayarishaji ramani za majini iliundwa. Katika mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara itaandaa Pendekezo la Mradi *(Project Formulation Proposal)* la upimaji katika eneo la Bahari ya Hindi na kuandaa andiko la mradi *(project write-up)* kwa kuwatumia wataalam waelekezi toka mashirika ya kimataifa yanayojihusisha na masuala haya. Shirika la *International Hydrographic Bureau (IHB)* limeonesha nia ya kushirikiana na Wizara yangu kufanikisha uandaaji wa andiko la mradi.

Mheshimiwa Spika, ramani za msingi za nchi ni nyenzo muhimu na za lazima katika Ujenzi wa Kumbukumbu Kuu na Takwimu za Kitaifa *(Development of a National Spatial Data Infrastructure).* Mfumo huu huonyesha raslimali na miundo mbinu

iliyojengwa juu ya ardhi ambayo ni msingi thabiti wa kuwezesha kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya Taifa katika sekta zote kwa ufanisi. Chini ya Mpango wa Kitaifa wa Utayarishaji wa Ramani za Msingi za Miji, Wizara yangu imepiga picha za anga za miji 38 katika Kanda ya Ziwa Victoria inayojumuisha Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga. Miji husika ni miji mikuu ya Mikoa ya Mara na Shinyanga, miji mikuu ya wilaya 8, miji midogo na vituo vya biashara 28 vinavyokua kwa kasi pia vimepigwa picha. Miji mikuu ya Mikoa na Wilaya iliyoachwa kupigwa picha ni kwa sababu kuna ramani za miji hiyo, ramani zilizotayarishwa katika kipindi chini ya miaka mitano iliyopita na bado zinafaa kwa matumizi. Utayarishaji wa ramani, kutokana na picha zilizopigwa, utaanza mwaka huu wa fedha na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, jumla ya ramani 82 za miji ya Sengerema, Nansio na Bariadi zilizotayarishwa kutokana na picha za anga za mwaka 1982, zimehuishwa kwa kutumia picha zilizopigwa mwaka 2002 kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi. Pia, mwaka huu wa Fedha 2004/2005, Wizara yangu inatarajia kupiga picha za anga za miji 30 katika Kanda ya Magharibi inayohusisha Mikoa ya Tabora, Kigoma, Rukwa, Iringa na Mbeya. Pia, maandalizi ya kutumia picha za *satellite* kuhuisha ramani za msingi za nchi katika uwiano wa 1:50,000 yataanza kwa kuingiza ramani za zamani kwenye kompyuta. Wizara yangu itafanya utafiti wa matumizi ya picha za *satellite* katika utambuzi wa vipande vya ardhi mijini na vijijini kwa lengo la kusajili hati za ardhi za Wananchi na hivyo kuigeuza ardhi kuwa rasilimali ya kujipatia mitaji kwa ajili ya kuwekeza katika maendeleo. Nia kuu ni kufanya ardhi na maendelezo yaliyopo juu yake, kubadilika kutoka mtaji mfu na kuwa mtaji hai katika uchumi wa taifa kama inavyopendekezwa na Mtaalam Bingwa wa masuala ya mitaji Bw. Hernando De Soto katika ushauri wake kwa Serikali ya Tanzania *(Transforming Dead Capital into Live Capital - Hernando De Soto Initiative).*

Mheshimiwa Spika, kupotea kwa mkuza wa mipaka ya Kimataifa ni chanzo kikubwa cha migogoro kati ya nchi mbalimbali. Ni muhimu kwa Serikali kutoa kipaumbele kuwawezesha wataalam wetu kukutana mara kwa mara na Wataalam wenzao wa nchi jirani kwa lengo la kukagua, kufyeka na kurejesha alama za mipaka zinapoharibika, na hivyo kuimarisha usalama wa Taifa na Wananchi wanaoishi karibu na mipaka ya nchi. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka jana, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na nchi za Kenya na Uganda ili kuimarisha mipaka kati ya nchi yetu na nchi hizo. Kwa mpaka wa Tanzania na Uganda, kilomita 110 za mpaka huo zilifyekwa na alama 422 zaidi ziliongezwa ili kurahisisha utambuzi wa mpaka. Kazi ya uthamini wa mali zilizoathirika wakati wa ufyekaji mpaka huo imekamilika na taratibu za kupata makubaliano ya kulipa fidia kwa wananchi husika zinafanyika. Kwa mpaka wa Tanzania na Kenya, kila nchi ilitayarisha ramani ya eneo la Ziwa Jipe na Mto Ruvu/Pangani. Ramani hizo zilifanyiwa ulinganisho na kukubaliana ramani moja kwa nchi zote mbili. Kazi iliyobaki ni kwa nchi zote mbili kuthibitisha na kukubaliana mpaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Jamhuri ya Malawi zilikamilisha Upembuzi Yakinifu wa Kudhibiti Mto Songwe. Kama itakavyo-kumbukwa, Mto Songwe unayo tabia ya kubadilisha mkondo wake na hivyo kubadilisha

mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Malawi. Upembuzi Yakinifu umebainisha kuwa ili kudhibiti mkondo wa Mto huo inahitajika kuimarisha kingo zake katika sehemu zenye kasi kubwa ya mmomonyoko wa ardhi na kujenga mabwawa matatu. Hatua inayofuata ni Usanifu wa Kina *(Detailed Design),* wa miundomsingi itakayodhibiti mafuriko na kuchochea shughuli nyingine za maendeleo. Upembuzi Yakinifu umependekeza kuwa udhibiti wa mto Songwe uwe ni sehemu moja tu ya Programu Kuu ya Kuendeleza Bonde zima la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Program)*. Lengo kubwa la mpango huu ni kuchochea maendeleo ya wananchi na kuwaondolea umaskini kwa kutumia maji ya mto Songwe kiuchumi. Serikali za Tanzania na Malawi zimetiliana saini makubaliano ya kutekeleza Usanifu wa Kina na zinafanya mawasiliano na wafadhili mbalimbali ili kupata msaada wa kutekeleza hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumetokea utata wa mpaka kati ya Tanzania na Zambia katika maeneo ya Tunduma na Isanga Wilayani Mbozi, na Kasesya Wilaya ya Sumbawanga Vijijini. Watalaam wa Tanzania wamekagua maeneo yote na kubaini kuwa katika eneo la Tunduma baadhi ya alama za mpaka zimeharibiwa. Katika eneo la Isanga wakazi wa eneo hilo wameshindwa kutambua mapito ya mpaka. Katika eneo la Kasesya Tanzania inajenga madaraja upande unaodhaniwa ni wa Zambia. Katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu itashirikiana na jirani zetu wa Zambia kuondoa utata huo.

Mheshimiwa Spika, makazi yaliyopangwa yanasaidia kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi bora na endelevu ya rasilimali za ardhi. Makazi yaliyopangwa na yenye huduma muhimu yanachangia katika kuongeza tija na kuendeleza uchumi wa watu wanaoishi katika maeneo hayo na hatimaye kupunguza umaskini. Idadi ya watu mijini imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa tangu tupate uhuru. Mwaka 1967, Tanzania ilikuwa na jumla ya watu 11,959,000 na asilimia 5.7 ya watu hao walikuwa wanaishi mijini. Aidha, kufuatana na sensa ya mwaka 2002, Tanzania ilikuwa na watu 34,443,603 na asilimia 23 kati ya hao wanaishi mijini. Idadi ya watu mijini imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 4.5 kwa mwaka. Kutokana na ongezeko kubwa la watu mijini, miji mingi imeshindwa kujitosheleza katika kupanga makazi, kupima viwanja na kuweka miundo mbinu na huduma muhimu kwa wakazi wake kutokana na ukosefu wa rasilimali za kutosha. Nchini Tanzania hali ya nyumba hairidhishi kwani katika maeneo ya miji kuna uhaba mkubwa wa nyumba na katika maeneo ya vijijini nyumba ni duni na si za kudumu. Nyumba ni muhimu katika maendeleo ya mwanadamu kwani nyumba bora huchangia katika kuwa na afya bora na hivyo kumwezesha mwananchi kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, vile vile mabadiliko ya sera na sheria mbalimbali za nchi, tabia za jamii, mabadiliko ya kiuchumi, utamaduni, sayansi na teknolojia, utandawazi na utekelezaji wa sera za uwekezaji yamesababisha mahitaji ya ardhi kuongezeka kwa kasi kubwa kwa matumizi mbalimbali na hivyo kuongeza matatizo ya makazi mijini na vijijini. Hali hii imeifanya Serikali kutafuta mbinu na mikakati mbalimbali ya kutatua matatizo haya. Wizara imeandaa Sera ya Maendeleo ya Makazi ambayo inasimamia uendelezaji wa Makazi nchini. Aidha, imekuwa ikiandaa mipango ya kimkakati ya uendelezaji miji, mipango ya uendelezaji upya maeneo ya kati ya miji, mipango ya

kuendeleza nyumba, mipango ya matumizi bora ya ardhi, pamoja na kutunga na kusimamia sheria na kanuni za udhibiti wa ukuaji wa miji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kuzingatia dhana ya ushiriki na ushirikishwaji, imeendelea kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya katika kuandaa mipango ya kimkakati ya kusimamia na kuratibu ukuaji na uendelezaji wa miji. Mipango hii huandaliwa pale tu ambapo Halmashauri husika imeonyesha uhitaji wake na kutenga fedha za utekelezaji wake. Kwa utaratibu huo, miji ya Makambako, Kibaha, Shinyanga, Songea, Karatu, Vwawa na Tunduma tayari imeandaliwa mipango ya kimkakati. Mipango ya miji ya Masasi na Lushoto iko katika hatua mbalimbali za maandalizi na inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha. Natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kuandaa mipango ya kimkakati ambayo inahusisha wadau katika kutatua matatizo ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili miji yetu kutokana na ukuaji wake wa kasi. Wizara yangu itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika upangaji na utekelezaji wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kati ya miji mingi hapa nchini yanahitaji kuendelezwa upya kwa vile majengo na miundombinu iliyopo imechakaa, haitoshelezi na haifanyi kazi kama inavyotarajiwa kutokana na idadi ya watu waliokusudiwa kuhudumiwa na miundo mbinu hiyo kuongezeka na hivyo imeelemewa. Wizara yangu imekuwa ikijishughulisha katika maandalizi ya mipango ya maeneo haya ya kati kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2003/2004, Wizara yangu iliahidi kukamilisha mipango ya uendelezaji upya wa maeneo ya kati ya miji ya Mbeya na Tabora. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu ya kuwa mipango hiyo imekamilika. Katika kipindi cha mwaka huu wa Fedha 2004/2005, mipango ya uendelezaji upya wa maeneo ya kati ya miji ya Sumbawanga, Kigoma, Singida na Tanga itatayarishwa. Kutokana na umuhimu wa kuendeleza upya maeneo ya kati ya miji, nazikumbusha Halmashauri za miji ambazo hazijawasilisha ramani za mipaka ya maeneo chakavu yanayohitaji kuendelezwa upya, kukamilisha kazi hiyo mapema ili ziweze kuwekwa katika mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara yangu iliidhinisha michoro 147 kutoka katika Halmashauri za Jiji, Manispaa na Miji mbalimbali hapa nchini yenye jumla ya viwanja 55,751 vya matumizi mbalimbali. Michoro ya mipangomiji ina umuhimu wa kipekee katika kutoa uelekeo na utaratibu mzuri wa uendelezaji wa viwanja katika miji. Michoro ikisimamiwa vyema inachochea ukuaji mzuri, hifadhi ya mazingira ya miji na kuleta mandhari nzuri kama ilivyopangwa. Wizara yangu inahimiza Halmashauri ziendelee kuandaa michoro ya maeneo mapya na kurejea *(revise)* michoro katika maeneo ya miji ambayo imepitwa na wakati na kuiwasilisha Wizarani kwa kuidhinishwa. Aidha, Wizara yangu imekusanya takwimu kwa ajili ya kuboresha viwango vya maeneo na upangaji *(Space and Planning Standards)* ambavyo katika kipindi cha mwaka huu vitachapishwa na kutangazwa kwa ajili ya kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ardhi kwa matumizi mbalimbali yamekuwa yakiongezeka kwa haraka na upungufu wa rasilimali za kuandaa maeneo ya kutosheleza

mahitaji hayo yamesababisha wimbi kubwa la maombi ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Mengi ya maeneo yanayofanyiwa mabadiliko ni yale ya maeneo ya wazi, makazi, shule, vituo vya afya, ibada, burudani na michezo. Maeneo hayo yamekuwa yakifanyiwa mabadiliko ya matumizi ya ardhi bila kuzingatia taratibu. Kwa kawaida ujenzi kwa ajili ya mabadiliko hayo siyo yote yenye madhara hasa yale yanayofanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Tangazo la Serikali Na. 678 la Mwaka 1964, linaelekeza hatua za kufuata kupata kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Nasisitiza kuhusu umuhimu wa Halmashauri kuheshimu utekelezaji wa mipango iliyoidhinishwa kwani inalenga katika kuwa na makazi bora yenye tija, afya na salama.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu inaendelea na zoezi la kuhuisha Sheria ya Mipangomiji na Vijiji (Sura 378) ya Mwaka 1956. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu imekamilisha rasimu za mapendekezo ya Sheria mbili mpya kutokana na sheria hiyo. Mapendekezo ya rasimu za Sheria hizo, moja ya Mipangomiji na nyingine ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Vijijini, zimekamilishwa baada ya kujadiliwa katika warsha za wadau. Katika mwaka huu wa Fedha Miswada husika itaandaliwa na, kwa wakati muafaka, kuwasilishwa Bungeni. Wizara yangu vile vile inaandaa mapendekezo ya Sheria ya Kusajili Wataalam wa Fani ya Mipangomiji na Vijiji kwa lengo la kusimamia taaluma hii na kujenga maadili bora ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ingekamilisha maandalizi ya Kanuni za Ujenzi *(Building Regulations).* Napenda kutoa taarifa kuwa kanuni hizo zilikamilika na zimewasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuzitangaza katika Gazeti la Serikali. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi mpya zitasaidia katika kuendeleza miji hapa nchini. Vilevile katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara itaendelea kukamilisha marekebisho ya Sheria Na. 2 ya Shirika la Nyumba la Taifa ya Mwaka 1990 ili kuboresha ukusanyaji wa kodi, kurahisisha upatikanaji wa maeneo yenye majengo chakavu yasiyofaa kukaliwa na binadamu kwa ajili ya kuyaendeleza na kuongeza uwezo wa Shirika wa kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, tangu Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali uanzishwe mwaka 1992, umepokea jumla ya maombi ya watumishi 1,642 wanaoomba mikopo ya nyumba yenye thamani ya jumla ya Sh.8,013,853,196.75. Hadi Juni, 2004 watumishi 502 ambao ni sawa na asilimia 30.6 ya waombaji wote wamekwisha idhinishiwa na Bodi ya Mfuko mikopo yenye jumla ya Sh.1,573,533,208.75. Kati ya watumishi hao 502 waliopewa mikopo, watumishi 85 waliidhinishiwa mikopo yenye jumla ya Sh. 310,918,445.45 katika mwaka wa fedha uliopita 2003/2004. Kwa hiyo, hadi Juni, 2004 kulikuwa na bakaa la maombi 1,140 yanayohitaji zaidi ya Sh. 6.1 bilioni ambayo hayajashughulikiwa kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, juhudi kubwa zimefanywa kukusanya marejesho ya mikopo ili Mfuko uweze kupata fedha za kukopesha watumishi wengine. Tangu Julai 2003 hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2004 marejesho

yalikuwa yamefikia Sh. 78,139,443.05/= ikiwa ni pamoja na makusanyo ya malimbikizo. Marejesho halisi tangu 1994 yamefikia Sh. 294,427,434.25 ambazo ni sawa na asilimia 103.5 ya marejesho tarajiwa ya Sh. 284,447,189.30. Marejesho yamekuwa yakiongezeka hasa tangu mwaka 2001/2002, kutokana na kuboresha kumbukumbu za Mfuko na kuongeza juhudi za kuwafuatilia wakopaji. Mfuko huu ni mmoja wa mifuko michache ya Umma inayotoa mikopo ambayo imekuwa na historia nzuri ya marejesho ya mikopo. Wizara yangu inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha ili mfuko huu upatiwe fedha zitakazotumika kutoa Mikopo ya nyumba kwa watumishi wa umma wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi inaendelea kutambuliwa na wadau mbalimbali na wananchi kwa jumla kama njia muhimu katika harakati za kupunguza umaskini na kuhifadhi mazingira kwa kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi na rasilimali zake. Hivi sasa mipango hii inahitajika zaidi kuliko ilivyokuwa awali kutokana na ongezeko kubwa la watu na wanyama. Pia, kuna ongezeko kubwa la mahitaji mbalimbali ya matumizi ya ardhi kama vile kilimo, ufugaji, misitu na makazi. Ardhi hiyo haiongezeki na inaharibika kwa sababu ya matumizi mabaya kama vile ukataji misitu na uchimbaji madini holela, kilimo kisichozingatia utaalamu na uvunaji maliasili kiholela. Ushindani wa matumizi unaongezeka, migogoro inaibuliwa na matumizi mabaya ya ardhi yanashamiri. Wizara yangu itaendelea kuweka mazingira yanayofaa na kujenga uwezo wa wadau na taasisi mbalimbali, hususan Halmashauri za Wilaya na Vijiji, wa kuandaa utekelezaji na usimamizi wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewezesha Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mafia na Karagwe, kuunda timu za wilaya za upangaji wa matumizi bora ya ardhi ambazo hivi sasa zinaendelea na kazi ya uwezeshaji kwa vijiji vyao. Timu za wilaya za Masasi, Songea (Namtumbo), Morogoro (Mvomero), Kibaha, Hai, Ileje, Mwanga, Handeni na Lushoto zimejengewa uwezo zaidi kwa kupewa mafunzo ya ziada ili kuziwezesha kukamilisha hatua zote za upangaji shirikishi wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia wajibu wa Wizara wa kutoa sera na miongozo na kujenga uwezo wa wadau katika usimamizi wa ardhi, katika mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara, itaendelea kuwaelekeza wananchi kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi za Vijiji, Wilaya, Mkoa, Kanda na Taifa. Katika kutekeleza hayo, kazi zitakazofanyika ni pamoja na:-

(i) Kuweka misingi ya utayarishaji wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Taifa *(National Land Use Plan).*

(ii) Kurejea na kuchapisha nakala 10,000 za Miongozo ya Ushirikishwaji Katika Mipango ya Usimamizi na Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini, Toleo la II.

(iii) Kuchapisha miongozo ya utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ngazi ya wilaya.

(iv) Kukamilisha Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Vijijini na kuitafsiri katika Kiswahili.

(v) Kuandaa viwango vya upangaji chini ya utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini.

(vi) Kuanzisha na kujenga uwezo wa timu za wilaya za upangaji wa matumizi bora ya ardhi katika Halmashauri 10 za wilaya.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyobainishwa katika Sheria Nambari 2 ya Mwaka 1990. Majukumu hayo ni kutoa huduma za usimamizi wa miliki, ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ujenzi wa nyumba, kujenga nyumba au majengo ya aina mbalimbali ya kupangisha na kuuza, na kutekeleza shughuli za ukandarasi.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda na kutunza rasilimali ya Taifa, Shirika limeendelea kuzifanyia matengenezo nyumba zake kulingana na uwezo uliopo. Katika mwaka wa Fedha 2003/2004 hadi kufikia Juni, 2004, jumla ya nyumba 1,685 zimefanyiwa matengenezo kwa gharama ya Sh. 1,367,059,247/=. Aidha, elimu inatolewa kwa wapangaji na wananchi kwa jumla juu ya utunzaji wa nyumba na mazingira yake moja kwa moja au kupitia kipindi chetu cha radio. Pia, upo mkakati wa kuzuia moto ambao umeshaanza kutekelezwa kwa kushirikiana na Kikosi cha Zima Moto.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba linategemea kodi ya pango kama chanzo kikuu cha mapato katika kuendesha shughuli zake. Katika mwaka wa Fedha 2003/2004, Shirika lilipanga kukusanya Sh.13,479,893,742/=. Hadi kufikia mwezi Juni, 2004 limeweza kukusanya Sh. 11,862,271,293/= sawa na asilimia 88 ya lengo. Hata hivyo, kiasi hiki hakitoshelezi kugharamia shughuli muhimu za shirika. Hii inatokana na viwango vya kodi kuwa vya chini sana, wapangaji kutolipa kodi, kufilisika kwa makampuni mbalimbali, na kesi za mahakamani zinazochukua muda mrefu hususani Moshi na Mwanza jambo ambalo limeisababishia Shirika kuwa na malimbikizo ya madai makubwa ya pango yanayofikia Sh. 11,011,691,479.96 hadi Juni, 2004. Ni nia ya Wizara yangu kuondoa tatizo hili kwa kurekebisha viwango vya sasa vya kodi hatua kwa hatua tukianzia mwaka huu wa Fedha. Aidha, Wizara yangu inaandaa mapendekezo ya kurekebisha Sheria Na. 2 ya Mwaka 1990 kwa lengo la kuwabana wapangaji wanaokwepa wajibu wao. Ningependa kutoa wito kwa wapangaji wanaoishi katika nyumba za Shirika kulipa kodi zao kwa wakati. Ni vema waelewe kuwa nyumba hizo ni za watanzania wote. Wakati huo huo, Shirika la Nyumba la Taifa hadi kufikia mwezi Juni, 2004 limeweza kulipa kodi Serikalini ya jumla ya Sh. 1,143,637,123/=.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa zoezi la kuuza nyumba za gharama ndogo na kati liliongezewa muda zaidi kutoka mwezi Novemba, 2003 hadi Aprili, 2004. Wanunuzi waliokwisha kulipia kiasi wameongezewa muda hadi mwezi Agosti, 2004 na wenye maombi maalumu ya nyumba 195 wameongezewa muda hadi Desemba, 2004. Wale ambao hawakuweza kulipia hata kidogo, nyumba hizo ziliuzwa na Shirika katika mnada wa hadhara. Hadi kufikia mwezi Juni, 2004 jumla ya nyumba 4,928 zilipangwa

kuuzwa. Kati ya hizo, nyumba 3,850 zimelipiwa kikamilifu na kulipatia shirika mapato ya Sh. 5,324,251,926.15.

Mapato hayo yameliwezesha Shirika kutekeleza miradi ya ujenzi iliyokwisha anzishwa. Shirika limeendelea na juhudi za kujenga nyumba mpya za kuuza na za vitega uchumi kwa kushirikisha sekta binafsi. Nyumba za kuuza zinajengwa lakini kutokana na tatizo la kutokuwepo chombo cha kutoa mikopo ya kujengea na kununua nyumba, mafanikio yaliyokusudiwa hayakufikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata sera ya Serikali ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, Shirika limefanikiwa kuwapata wawekezaji wa ndani wanaowekeza katika ujenzi wa majengo makubwa ya vitega uchumi katika miji yetu. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Shirika liliendelea na ujenzi wa nyumba 218 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Kati ya nyumba hizo, ujenzi wa nyumba 144 katika eneo la Boko (Dar es Salaam) unaendelea, nyumba nne Mbezi Beach (Dar es Salaam), nyumba moja katika eneo la Kijenge (Arusha) na majengo sita ya vitega uchumi yamejengwa kwa njia ya ubia. Katika mwaka 2004/2005, Shirika litaendelea na ujenzi wa nyumba 258 za kuuza na majengo 21 ya vitega uchumi katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha. Kati ya majengo hayo, majengo mawili yatajengwa na Shirika lenyewe, na majengo 19 yatajengwa kwa njia ya ubia. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza wawekezaji wote wanaoshiriki katika programu hii na kuwataka wawekezaji wengine wajiunge na Shirika katika uwekezaji huu ambao ni wa manufaa makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka 2003/2004, niliahidi kuwa Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi *(National Housing and Building Research Agency-NHBRA),* ungejizatiti zaidi katika usambazaji wa matokeo ya utafiti wake kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, watu binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya dini, Wahisani na Serikali, hususan TAMISEMI. Wakala ulitekeleza ahadi hiyo kwa kuendesha semina na mafunzo kwa vitendo kwa washiriki 175 katika Halmashauri nane. Pia, Wakala ulihamasisha viongozi 304 wa Maendeleo ya Jamii wa kata, tarafa na wilaya, madiwani na wataalamu wengine katika Halmashauri 18 na Manispaa moja. Aidha, Wakala ulishiriki katika maonyesho na kuhudhuria mikutano mbalimbali ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, Wakala uliandaa kitabu cha “Mwongozo wa Ujenzi wa Nyumba Zisizo za Ghorofa” ambacho kiliidhinishwa na Wizara ya Elimu na Utamaduni ili kiwe kitabu cha kiada kwa shule za Sekondari na Vyuo vya Ufundi nchini. Mashine za kufyatua matofali zimeboreshwa na zinaweza kutengeneza aina tatu ya matofali yanayofungamana. Matofali hayo ni ya udongo ulioimarishwa kwa saruji na mengine ya udongo wa mfinyanzi ya kuchoma. Pia, wakala ulitoa huduma ya ushauri wa ujenzi, ukarabati na ujenzi kwa taasisi za dini, serikali na watu binafsi. Aidha, wakala uliwahudumia wateja wapatao 1,124 waliotembelea ofisi zake kutaka ushauri kuhusu ujenzi. Pia, Wakala ulihamasisha umma kwa njia ya Televisheni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, wakala utafanya kazi zifuatazo:

(i) Kuendesha semina za uhamasishaji juu ya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika wilaya za Ileje, Mbozi, Uyui, Temeke, Ilala na Kinondoni;

(ii) Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vikundi vya ujenzi juu ya utengenezaji na utumiaji wa vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu na teknolojia yake katika Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni ambako ni sehemu zitakakojengwa nyumba tatu za mfano katika Mkoa wa Dar es Salaam;

(iii) Kuhakikisha kuwa teknolojia ya ujenzi ipo tayari kwa kutolewa kwa wateja kwa muda wanapoihitaji na kuitangaza kwa njia mbalimbali ili kuhakikisha kuwa inafahamika; na

(iv) Kuendelea na kazi za msingi za wakala za Utafiti, uhifadhi, usambazaji na upimaji wa uimara na ubora wa vifaa mbalimbali vya ujenzi katika maabara ya wakala na katika maeneo ya ujenzi.

Napenda kutoa rai kwa Halmashauri ambazo hazijaomba kupelekewa mafunzo ya ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu ziwasiliane na Wakala.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutoa huduma bora kwa wananchi, Wizara yangu imekuwa ikijiwekea malengo ya kuwajengea watumishi wake mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Juhudi zilizofanyika katika kutimiza malengo hayo katika mwaka wa Fedha 2003/2004, ni pamoja na kutoa mafunzo, kuboresha mazingira ya ofisi, kuwapatia watumishi stahili zao na kudumisha utawala bora ikiwa ni pamoja na kusisitiza nidhamu, kupiga vita rushwa na kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI. Aidha, Wizara yangu ni moja kati ya Wizara zilizoingia katika Mfumo wa Usimamizi Unaozingatia Utendaji *(Performance Management System).*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana watumishi wa Wizara yangu walihudhuria mafunzo mbali mbali yaliyogharamiwa na Wizara. Mafunzo yalihusu Uongozi, Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma na Sheria za Ardhi za Mwaka 1999. Jumla ya watumishi 524 walishiriki mafunzo hayo. Aidha, watumishi 100 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika vyuo mbalimbali, ndani na nje ya nchi. Katika hotuba yangu ya mwaka jana niliahidi kuwa wizara yangu ingetoa mafunzo kwa Maafisa Ardhi Wateule 50 baada ya Halmashauri kuajiri maafisa hao. Ninasikitika kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, pamoja na Halmashauri kuajiri Maafisa Ardhi, bado idadi yao haijatosheleza kuendesha mafunzo hayo hivyo kuifanya Wizara ishindwe kuendesha mafunzo hayo. Iwapo idadi itatosheleza, mafunzo hayo yatafanyika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ni moja kati ya Wizara zinazopokea wageni wengi. Wastani wa wageni 534 wamekuwa wakipokelewa na kuhudumiwa kwa siku. Katika mwaka wa Fedha wa 2003/2004 Wizara iliweza kuwapatia watumishi wake

vitendea kazi vya kisasa ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi hao. Aidha, huduma mbalimbali zimeendelea kutolewa haraka kwa kutumia mawasiliano ya kisasa yakiwemo nyaraka umeme, posta, barua pepe na simu za mdomo. Jumla ya barua 11,788 zilipokelewa na kushughulikiwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2003 hadi Juni, 2004. Lengo la Wizara ni kuboresha utoaji wa huduma ili kuondoa kero mbalimbali kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Miundo mipya ya Utumishi ya Kada mbali mbali Serikalini, watumishi wa Wizara yangu walipewa barua zinazoonyesha vyeo halisi kulingana na mabadiliko hayo. Aidha, malipo mbalimbali yalitolewa kwa watumishi wenye stahili na watumishi waliokwenda likizo walilipwa nauli kulingana na stahili zao. Watumishi ambao walistahili kupandishwa vyeo kufuatana na miundo yao ya zamani, walipandishwa na kuingizwa katika vyeo vipya bila kupoteza stahili zao. Upatikanaji wa stahili za watumishi kwa wakati unawaongezea watumishi ari ya kufanya kazi

Mheshimiwa Spika, vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro ni vyuo pekee nchini vinavyotoa mafunzo ya cheti na *diploma* katika fani za Urasimu Ramani, Umiliki Ardhi na Uthamini, Uchapaji na Upimaji Ardhi ambayo hayatolewi katika vyuo vingine hapa nchini. Katika mwaka wa Fedha 2003/2004, idadi ya wahitimu kutoka Vyuo vya Ardhi ilikuwa 75. Chuo cha Ardhi Morogoro kilitoa wahitimu 29 na Chuo cha Ardhi Tabora kilitoa wahitimu 46. Hivi sasa Chuo cha Ardhi Morogoro kinatambuliwa na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi *(National Council for Technical Education - NACTE)*. Aidha, Chuo cha Ardhi Tabora nacho kinatathminiwa kwa lengo la kutambuliwa na Baraza hilo. Kutambuliwa kwa vyuo hivi na Baraza hilo kutawafanya wahitimu wa *Diploma* kutoka katika vyuo hivi kuweza kuingia vyuo vikuu kwa mafunzo ya shahada ya kwanza. Lengo la Wizara ni kuendelea kuviimarisha vyuo hivi ili viweze kuendelea kutoa elimu bora zaidi inayoendana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma bora hufanikiwa kama kuna nidhamu mahali pa kazi. Wizara yangu imechukua hatua kadhaa ili kuhakikisha nidhamu inadumishwa. Hatua hizo ni pamoja na kuwapatia watumishi mafunzo ambayo yanasaidia kujenga nidhamu. Aidha, Wizara ililazimika kuchukua hatua kali kwa watumishi ambao walikiuka maadili na kuonyesha utovu wa nidhamu. Katika mwaka 2003/2004, watumishi 15 walisimamishwa kazi na hatimaye sita kati yao walifukuzwa, watano wana kesi za kujibu mahakamani na wanne wameundiwa Tume za uchunguzi. Nia ya wizara yangu ni kuhakikisha kuwa nidhamu inakuwepo mahali pa kazi na watumishi wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Hatua zilizochukuliwa zitasaidia kuwakumbusha watumishi wengine kufanya kazi zao kwa uadilifu.

Mheshimiwa Spika, Rushwa ni moja kati ya kero kubwa kwa wananchi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imeendelea kubuni mikakati mbalimbali zaidi ya ile niliyoitaja mwaka jana ili kuziba mianya ya rushwa. Mikakati hiyo ni kutoa elimu kwa umma kwa njia ya redio, televisheni na vipeperushi ili watambue haki na wajibu wao na kudhibiti mwenendo wa majalada kwa kutumia kompyuta ili kuharakisha maamuzi.

Kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa, mwaka 2003 nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya tatizo la kuwepo rushwa katika baadhi ya maeneo ya Shirika na yalikuwa yakifanyiwa utafiti na Taasisi ya Kuzuia Rushwa. Utafiti huo ulikamilika na taarifa yake iliwasilishwa kwa Uongozi wa Shirika. Hivi sasa uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa umeanza kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotokana na utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya janga la UKIMWI Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya UKIMWI ya Taifa *(TACAIDS),* imeendesha semina za uhamasishaji juu ya maambukizi na athari za janga la UKIMWI kwa wafanyakazi wa Makao Makuu. Watumishi na wanafunzi wa Vyuo vya Ardhi vya Morogoro na Tabora, Mabaraza na Ofisi za Kanda za Usajili wa Hati watapatiwa mafunzo hayo katika mwaka huu wa fedha. Vilevile, Wizara imeandaa Mkakati wa miaka mitatu wa mapambano dhidi ya janga la UKIMWI kwa matarajio kuwa utatumika kama mwongozo wa kudhibiti janga hilo kwa kuhakikisha kila idara inajadili katika vikao vyake vya kawaida hatua za utekelezaji wa mapambano hayo.

Hatua hiyo itahamasisha wafanyakazi kuzingatia hatua za kujikinga na maambukizi. Sambamba na Mkakati huo, utafanyika utafiti wa hali halisi ili kubaini namna ambavyo Wizara imeathirika na janga la UKIMWI ili kuweza kutoa huduma ya karibu kwa walioathirika ikiwa ni pamoja na kuwapatia dawa za kuwaongezea muda wa kuishi. Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa waelimisha rika ili kuwakumbusha kwa karibu wenzao juu ya hatua za kujikinga na maambukizi wanapokuwa nje ya ofisi kikazi. Ni matumaini yangu kuwa kwa kutekeleza mkakati huo tutapunguza maambukizi na unyanyapaa kwa wafanyakazi walioathirika pamoja na familia zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya maboresho kwa lengo la kutoa huduma bora. Miongoni mwa maboresho hayo ni kuweka Mfumo wa Usimamizi Unaozingatia Utendaji. Mfumo huu unawezesha kupima uwajibikaji wa watumishi Serikalini ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa kwa madhumuni ya kutoa huduma bora kwa ufanisi. Mfumo unaonyesha mkakati wa Wizara *(Strategic Plan),* ahadi za Wizara kwa wateja *(Client Service Charter),* mkataba wa utendaji kazi kati ya msimamizi na msimamiwaji *(Individual Performance Agreement)* na namna ya kupima utendaji kwa njia ya uwazi *(Open Performance Review and Appraisal System).* Aidha, mfumo huu unatoa fursa ya kufanya marejeo, kufuatilia na kutathmini *(Monitoring and Evaluation)* utendaji kazi. Hadi sasa Wizara imetayarisha nyaraka zilizotajwa hapo juu na utekelezaji wake utaanza katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, jitihada zetu zitaendelea kuelekezwa katika kuwawezesha Wananchi kutumia rasilimali ardhi kujiongezea mapato, kujipatia mitaji itakayowawezesha kuendesha shughuli za kiuchumi na hivyo kupunguza umaskini. Pia, kuleta amani na utulivu kwa kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba. Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Sera na Sheria za Ardhi ambao umeanza kutekelezwa, utaendelea kutekelezwa kwa kasi zaidi. Jitihada za pekee zitatumika katika matumizi ya teknolojia za kisasa katika utoaji huduma kwa wateja. Ningependa kutoa rai kwa Wananchi kwamba mikakati hii iliyowekwa na Wizara itafanikiwa tu iwapo Wananchi

watashirikiana na Wizara katika kufuata utaratibu wa kupata huduma zinazotolewa na Wizara na kuwafichua wale wote wanaokiuka taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Hajat Tatu Ntimizi, Naibu Waziri, Bibi Salome Sijaona, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara/Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara yangu na kwa wote waliotoa misaada kwa Wizara. Napenda kutumia fursa hii pia, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamisheni ya Umoja wa Ulaya *(European Commission)*, Serikali ya Uholanzi, Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GTZ)*, Shirika la Maendeleo la Norway *(NORAD),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi *(UN-HABITAT),* pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali yaliyoshirikiana na Wizara katika kutoa elimu ya Sheria za Ardhi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi Vijijini. Mashirika hayo ni *Tanzania Home Economics Association (TAHEA),* Hifadhi Bahari Mafia (HIBAMA), *CONCERN, Makondenet-Masasi* na *Women Advancement Trust (WAT)*. Wote hawa wameisaidia Wizara katika kutoa elimu kwa umma na kuendeleza mipango ya matumizi ya ardhi vijijini. Kwa kuwa Wizara bado ina kazi kubwa katika harakati za kueneza elimu kwa umma, nawaomba wadau wengine zaidi kujitokeza hasa wale wanaoshughulika vijijini, kusaidia jitihada za Serikali za kutoa elimu sahihi kwa umma na kupanga matumizi bora ya ardhi. Namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapa kwa wakati nyaraka zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza yote hayo niliyoyaeleza, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa Fedha wa 2004/2005 kama ifuatavyo:-

(i) Sh. 5,896,650,000/= kama Makusanyo ya Mapato ya Serikali.

(ii) Sh. 1,670,195,800/= kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

(iii) Sh. 4,020,476,600/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

(iv) Sh. 673,000,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Jumla ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni Sh. 6,363,672,400/=.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe na pia Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nadhani tutakuwa na nafasi ya kusikiliza wachangiaji watatu, kwa hiyo, watakuwa ni Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Hadija Kusaga, hao watatufikisha saa 7.00 mchana, wengine wataanza saa 11.00 jioni mpaka saa 12.00 kama kawaida yetu. Sasa namwita Mwakilishi wa Kamati ya Kilimo na Ardhi.

**MHE. SALAMA KHAMIS ISLAM (k.n.y. MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004 , naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2003/2004, pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Danhi B. Makanga, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutoa pole ka Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, ndugu na jamaa wa Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, kwa msiba mkubwa uliotokea. Pia naomba kutoa mkono wa rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, kwa kifo chake cha ghafla, Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Eliachim Simpasa Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa John E. Singo, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Edward Ndeka na mwisho ni mimi mwenyewe niliyesimama hapa mbele yenu *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana.

Hata hivyo, katika maeneo ambayo Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika tumeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata maelezo ya kina juu ya majukumu ya Wizara, malengo na utekelezaji wake kwa mwaka uliopita.

Aidha, Kamati ilifahamishwa kwamba, katika utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa mwaka wa fedha uliopita yalipatikana mafanikio mengi ya kuridhisha. Miongoni mwa mafanikio hayo ni:-

- Kufanya jaribio la kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Vijiji kwa kutoa vyeti saba vya Ardhi katika Vijiji vifuatavyo vya Wilayani Mbozi Mkoa wa Mbeya, Vijiji hivyo ni Halungu, Ibembwa, Msia, Iganduka, Shasya, Halambo, Malolo na kutambua mashamba 1,400 ya Wananchi na kutoa hati ya haki ya kimila katika Kijiji cha Halungu. *(Makofi)*

- Kuweka kumbukumbu za viwanja katika kompyuta ambako kumewezesha Wizara kubaini wamiliki na walipa kodi wa viwanja na mashamba katika Jiji la Dar es Salaam, Kanda ya Ziwa na ya Kaskazini.

- Kuwepo ongezeko la uelewa wa Sheria za Ardhi nchini unaotokana na elimu kwa umma inayotolewa juu ya Sheria hizo kwa njia mbalimbali.

- Kukamilisha uteuzi wa Kamati za kugawa Ardhi kwa Halmashauri 113 na Kamati hizo kuanza kufanya kazi.

- Kumilikisha viwanja vilivyopimwa chini ya mradi wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Kamati ilifahamishwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2004 idadi ya viwanja vilivyomilikishwa imefikia 18,105.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, Kamati yangu pia ilielezwa matatizo yaliyoikabili Wizara ambayo baadhi yake ni:-

- Ubovu na uchakavu wa jengo lenye mitambo ya kutengeneza ramani kwani lilijengwa tangu enzi za Utawala wa Wajerumani. Ubovu huu unatishia usalama na mazingira yanayotakiwa katika kutunza na kutumia mitambo, zana na kompyuta.

- Mipaka kati ya nchi yetu na nchi za jirani kutotambulika kutokana na alama kuharibika au kung'olewa, kwa mfano, mpaka kati ya Tanzania na Uganda Mkoani Kagera.

- Halmashauri nyingi kutoajiri wataalamu wenye sifa za kusimamia na kutoa huduma za ardhi. Aidha, ofisi za ardhi kwenye Halmashauri hizo hazipewi kipaumbele katika kugawiwa rasilimali.

- Maeneo ya makazi kujengwa vituo vya mafuta bila kufuata sheria na taratibu za mipango miji.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa pongezi kwa jitihada za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika kufanikisha malengo yake licha ya matatizo wanayokabiliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2003/2004 na malengo ya bajeti kwa mwaka 2004/2005, kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kamati ilipata maelezo ya kina ya majukumu ya Wizara, malengo ya Wizara na utekelezaji wake kwa mwaka uliopita na mipango iliyowekwa kwa mwaka ujao wa fedha.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kutekeleza malengo na miradi mbalimbali ya kuboresha makazi nchini na pia kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati kama ilivyofafanuliwa kwenye maelezo ya Waziri. Hata hivyo, katika kuzidi kuboresha utendaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2004/2005, Kamati yangu inatoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Wizara imepangiwa kutumia Sh. 673,000,000/= kwa miradi ya maendeleo. Kamati inaona kiasi hiki ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu makubwa ya Wizara ya kuboresha makazi nchini. *(Makofi)*

Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kuboresha makazi nchini na hasa Mipango Miji ili kuwanusuru Wananchi na Taifa dhidi ya maafa yanayotokana na ujenzi holela hasa yanapotokea mafuriko, magonjwa ya milipuko kama kipindupindu na kadhalika. Aidha, Wizara inatakiwa iandae Mpango wa Utekelezaji *(Action Plan)* ili utumike katika kuombea fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa ubunifu wake wa kufufua Mtaji Mfu kuwa Mtaji Hai kwa kuipa thamani ardhi. Hili litafanyika kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji ambapo Vijiji vitapimwa na Wananchi watamilikishwa maeneo. Kamati imearifiwa kwamba, Wizara imepanga kupima viwanja katika Vijiji 750.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mijini, Kamati ilifahamishwa kuwa Wizara inalenga kutambua maeneo ambayo hayakupimwa ili yapimwe na wenye ardhi wapatiwe leseni ya makazi *(Residential Licence),* ambazo zitawawezesha kutumia ardhi hiyo kama dhamana ya kuweza kupatia mikopo. Kamati yangu inapongeza sana ubunifu huu ambao utawawezesha Wananchi kunufaika na ardhi wanayomiliki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara na Halmashauri husika ziwashirikishe Wananchi wa maeneo hayo kikamilifu ili kuondoa migongano na uhasama unaoweza kujitokeza wakati wa zoezi zima la upimaji na umilikishwaji wa viwanja.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro ya ardhi karibu kila Wilaya na Vijiji hapa nchini. Uanzishwaji wa Mahakama ya Ardhi katika ngazi za Wilaya na Kata ili kutatua migogoro ya ardhi kwa kutumia Sheria Na. 2 ya mwaka 2002 *(The Land Disputes Courts Act, 2002)* ni hatua kubwa ambayo itasaidia kutatua migogoro hii. Pia Mahakama hizi zitapunguza gharama kubwa walizokuwa wakitumia wanavijiji kwenda mijini kuhudhuria kesi zinazohusu migogoro ya ardhi, kesi ambazo huchukua muda mrefu kumalizika. Kamati inashauri zoezi hili la kuanzisha Mahakama za ardhi katika Wilaya na Kata likamilishwe mapema katika maeneo yaliyosalia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa katika kutekeleza mradi wa kupima viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam, Wizara ilikopa shilingi bilioni 8.9 kutoka Hazina na marejesho yake yalitakiwa yafanyike mwezi Juni, 2004. Aidha, Kamati imejulishwa kuwa mradi huu bado unaendelea. Kwa kuwa makazi kwa binadamu ni muhimu sana na ni hatua mojawapo katika dhana nzima ya kuondoa umaskini na kwa kuwa mradi wa ufufuaji Mtaji Mfu kuwa Mtaji Hai, unahitaji fedha za kutosha, Kamati inashauri kuwa badala ya mkopo huu kurudishwa Hazina, Wizara iruhusiwe kutumia fedha hizo kama *revolving fund* ya kuendeleza upimaji wa viwanja zaidi ili mradi huu uwe endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha Wananchi kujenga nyumba bora katika viwanja vinavyopimwa na kununua nyumba zinazojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha chombo maalum cha kutoa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kama invayofanyika katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi ya miji mikubwa hapa nchini kumekuwa na tabia ya ujenzi holela wa kujenga majengo bila kufuata taratibu zilizowekwa za Mipangomiji. Mfano yapo maeneo maalum *(Prime Areas),* yanayotakiwa kujengwa majengo yasiyo ya ghorofa lakini watu wanajenga maghorofa. Hali hii huharibu dhana nzima ya Mipangomiji na hata masuala ya usalama wa makazi. Kamati pia imebaini kuwa yapo maeneo yaliyopimwa vizuri, kwa mfano, *Mbezi Beach,* lakini usimamizi wa ujenzi ukawa mbovu na hivyo kuvuruga kabisa mpango uliokuwepo.

Aidha, limejitokeza tatizo la maeneo ya makazi kugeuzwa ya viwanda na ujenzi holela wa vituo vya mafuta, jambo ambalo ni hatari na sio la kufumbiwa macho. Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu ujenzi wa Makazi Mijini ili kuhakikisha kwamba, vibali vya ujenzi vinatolewa kwa kuzingatia sheria na taratibu za Mipango Miji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo la baadhi ya watu wanaopewa viwanja kushindwa kuviendeleza kwa muda mrefu na hivyo kuziba nafasi kwa wale wenye nia nzuri. Kamati inashauri kuwa Wizara ifuatilie kwa karibu suala hili kwa kutoa muda maalum kwa wale wanaopewa viwanja kuviendeleza kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha Wananchi wanapatiwa huduma bora kuhusiana na masuala ya ardhi, Kamati inaishauri Wizara iajiri wataalamu wenye sifa na wapatiwe vitendea kazi vya kuwawezesha kuwahudumia Wananchi ipasavyo. Aidha,

wataalamu hao wawe wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kuongeza tija katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetambua kuwa Wizara imetenga fedha kwa ajili ya masuala ya UKIMWI. Hata hivyo Kamati inaamini wafanyakazi wa Wizara hii ni miongoni mwa Watanzania wale ambao tayari wanao uelewa juu ya masuala mbalimbali ya UKIMWI, hivyo, badala ya fedha hizo kutumika kwa warsha na makongamano ya maambukizi na namna ya kujikinga na UKIMWI, fedha hizo zilenge kuwapatia huduma wafanyakazi ambao wameathirika ili kulinda nguvukazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara iwe makini katika suala zima la ulipaji fidia kwa watu wanaoathirika katika miradi mbalimbali ya Wizara. Viwango vya fidia vilingane na thamani halisi ya mali iliyopo, pia malipo yafanyike kwa wamiliki halali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na Wizara katika mapambano dhidi ya rushwa hasa katika maeneo ya ugawaji na upimaji wa viwanja. Hata hivyo Kamati inasisitiza jitihada hizi ziongezwe kwa kuziba kabisa mianya ya rushwa katika sekta zote za Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilipata fursa ya kutembelea miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa Jijini Dar es Salaam mathalan mradi wa ujenzi wa nyumba 191 za gharama ya kati huko Boko, mradi wa nyumba 43 *Mbezi Beach,* miradi ya ubia wa nyumba za ghorofa zaidi ya kumi, pamoja na mradi binafsi wa Shirika huko Mwananyamala Komakoma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na *NHC* hususan miradi hii ambayo imelenga kupunguza tatizo la makazi Jijini Dar es Salaam. Ili kuongeza ufanisi Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

- Shirika lizidishe elimu kwa wapangaji wake juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati ili huduma ziboreshwe zaidi na Shirika liweze kujiendesha kibiashara.

- Hatua za kisheria zichukuliwe kwa wadaiwa sugu. Kwa kuwa sheria husika zimeonekana kuwa na mapungufu hasa kwa kuegemea zaidi upande wa wapangaji na kuumiza wamiliki, Kamati inashauri sheria hizo zipitiwe upya na ikibidi marekebisho yafanyike.

- Kuwe na mahusiano ya karibu kati ya Shirika na taasisi zinazoshughulikia utoaji wa huduma za maji, umeme na ujenzi wa barabara ili huduma hizi zitolewe sambamba na miradi ya ujenzi wa nyumba na hivyo kuvutia wateja.

- Shirika litafute uwezekano wa kujipanua hadi Vijijini ili kuwawezesha wakazi wa maeneo hayo nao kumiliki nyumba bora kulingana na uwezo wao.

- Wizara isaidie Shirika kupata mikopo yenye riba nafuu ili kuliwezesha kukamilisha malengo yake kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kumpongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Hajat Tatu Ntimizi, kwa ushirikiano mkubwa tulioupata kutoka kwao kuanzia wakati wa ziara ya Kamati katika taasisi zao hadi vikao vya Kamati kuchambua bajeti ya Wizara. Aidha, nawashukru Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu wao Mkuu, Bibi Salome Sijaona, kwa michango na ushirikiano wakati wa Vikao vya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hii, kwa umakini na ushirikiano wao wakati wa kuchambua na kupitia vifungu mbalimbali vya bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Aidha, natoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka M. Mussa, pamoja na wasaidizi wake hasa Makatibu wa Kamati hii, Bi Nenelwa Mwihambi na Ndugu Abdallah Hancha, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi kutoka kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliombwa iidhinishe shilingi 6,363,672,400.00. Shilingi 5,690,672,400.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 673,000,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi uliofanyika na ushauri uliotolewa, Kamati kwa ujumla imekubaliana na Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 na kuupitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati napenda kutamka kuwa, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kama kawaida yangu kumshukuru Mwenyezi Mungu, kuweza kunijalia asubuhi hii baada ya kumaliza shughuli ya kumuaga Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, tukaweza kushiriki katika shughuli za Bunge kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza hotuba yangu, nataka niseme kwamba, kwa kweli hali yangu sio ya kawaida asubuhi hii hasa kutokana na msiba wa mwenzetu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Hapa nasimama bado kwa kweli moyo wangu unakwenda kasi sana.

Mheshimiwa Spika, inawezekana basi katika kuwasilisha hotuba hii nikakosea au nikateleza sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, mnivumilie kwa hili.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu bajeti ya

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (b), (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu mimi binafsi na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Ziwani ninaowawakilisha, ninapenda kuwapa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, kutokana na msiba uliowakumba kwa kifo cha Mbunge huyo mwezi uliopita. Vile vile ninawapa Pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao hivi karibuni. Aidha, ninawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao. Ninawapa pole pia wale wote waliofikwa na masahibu mbalimbali kama vile ajali na kadhalika. Kwa namna ya kipekee naomba niwape pole Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, kilichotokea ghafla usiku wa kuamkia jana. Mungu aziweke peponi roho za Marehemu. *(Amina)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, kwa ushirikiano walionipa, ambao umeniwezesha kupata urahisi wa kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, imeweka Dira Maalum (mwelekeo), ya kuweza kuongoza uendeshaji wa shughuli za Wizara hiyo. Dira ya Wizara ni kuwa na huduma bora zaidi za uendelezaji ardhi na makazi, mijini na vijijini, ardhi iliyopimwa na ramani kutayarishwa vizuri kwa matumizi mbalimbali na uwekaji mzuri na upatikanaji wa haraka wa kumbukumbu za ardhi kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona utekelezaji wa dira hiyo utafanikiwa tu ikiwa Wizara husika itazingatia ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa Kitabu cha Kiongozi cha Mwanakijiji katika utumiaji wa Sheria ya Ardhi Vijijini Namba 5 ya mwaka 1999, si wa kuridhisha. Kitabu hicho hakijasambazwa katika mikoa yote nchini kama ilivyooneshwa katika jedwali namba 1 katika Kitabu cha Bajeti cha Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi katika mwaka wa 2001/2002 kwa Mikoa kama Kagera, Kigoma, Rukwa, Lindi na Shinyanga. Ili kuleta maendeleo na kupunguza mizozo isiyo na sababu katika sekta ya ardhi, ni vyema vitabu vya sheria hiyo vikasambazwa mikoa yote na wilaya zote na idadi ikaongezeka.

Mheshimiwa Spika, dira hiyo iliyowekwa na Wizara, itashindwa kutekelezeka kama suala la ada za viwanja halitafanyiwa marekebisho yenye kuleta manufaa kwa Wananchi, kwani hiyo ada ya kiwango cha Sh.500,000/= ni kubwa sana ukilinganisha na kipato cha Wananchi wengi, ambacho hakifikii hata Sh.100,000/= kwa mwaka. Hali hii inaweza kusababisha viwanja hivyo kunyang'anywa na hatimaye kuchukuliwa na watu wachache sana wenye uwezo wa kipesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kushirikiana na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ihakikishe kuwa watu hawaweki makazi katika sehemu zilizo mabondeni, ambazo ni rahisi kukumbwa na mafuriko, hivyo kuleta hasara kubwa kwa Wananchi hao. Ada kubwa za kulipia viwanja na urasimu katika kupata viwanja ni kichocheo kikubwa cha watu kujenga mabondeni.

Mheshimiwa Spika, Hati za umilikaji ardhi wa miaka 33, zitolewazo kwa wazawa, zibadilishwe na umiliki uwe ni wa miaka 99 kama ilivyo kwa wageni. Kwa kuendeleza utaratibu huo wa zamani, wazawa wanakandamizwa, wakati wageni wananeemeka. Wakulima na wafugaji kugawiwa ardhi sehemu moja huleta migongano ambayo inafanya utekelezaji wa dira ya Wizara hiyo usiweze kupata mafanikio mazuri kama vile ilivyotokea katika Wilaya ya Kilosa mwaka 1999. Hivyo, ugawaji wa maeneo tofauti ya ardhi kwa wakulima na wafugaji ukitiliwa maanani, utaepusha migogoro na mizozo isiyo na lazima. Aidha, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa utaratibu na sheria zilizotumiwa katika kunyang'anya ardhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam waliokuwa wanamiliki mashamba makubwa na mafao yao yalikuwaje? Tunahisi zoezi zima lilikuwa ni kuwanufaisha baadhi ya watu tu, kuwafanya kuwa na miliki ya viwanja zaidi ya kumi kwa mtu mmoja maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inaomba maelezo kwa hili na ni watu wangapi wameathirika na zoezi hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sakata ya Shamba Namba 39/203.5/99790 katika Kijiji cha Mapinga Wilaya ya Bagamoyo. Kihistoria ardhi iliyokuwa shamba Namba 39 ikiwa na hatimiliki namba 32968 na *LO* Na. 99760, ilimilikiwa na Bwana Babri Singh Malik tangu mwaka 1987. Kwa kuwa pamoja na kuvunja masharti mengine ya kumiliki ardhi hiyo, alishindwa kuiendeleza hata kidogo. Hivyo, katika mwaka 1957, Serikali ya Kijiji ilipendekeza mmiliki huyo afutiwe hati ya kumiliki shamba hilo. Mapendekezo ambayo yalifanyiwa kazi vizuri na hatimaye mnamo tarehe 6 Septemba, 2001 mmiliki huyo alinyangw’anywa shamba hilo. Baada ya Serikali kupata taarifa za ubatilisho wa hati hiyo, Serikali ya Kijiji hicho iligawa kwa wanakijiji maeneo madogo madogo, ambayo Wananchi walianza kuendeleza maeneo hayo kwa shughuli za kilimo, ufugaji, makazi na huduma za jamii kama shule na makanisa na kadhalika. Wananchi waliogaiwa maeneo hayo ni pamoja na Maafisa wa Jeshi la Ulinzi na Usalama, Walimu wastaafu mbalimbali na Wananchi wa kawaida wenye shida na hali ya kujipatia makazi ya kujihifadhi na kujipatia maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha na kushangaza ni jitihada za baadhi ya Watendaji wa Wizara ya Ardhi hasa Afisa Ardhi wa Wilaya ya Bagamoyo, Bwana D. L. Kilungu, kupendekeza shamba hili sasa lirejeshwe kwa mmiliki wa zamani kwa ushahidi wa barua yenye Kumbukumbu Namba BAG/4625/24 ya tarehe 15 Aprili, 2004, ambayo imeandikwa kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Bagamoyo na Afisa Maendeleo wa Ardhi wa Wilaya ya Bagamoyo kwenda kwa Kamishna wa Ardhi Dar es Salaam na naomba kuinukuu:

Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo,
Idara ya Ardhi,
S.L.P. 11,
**BAGAMOYO**.
5 Aprili, 2004.

Kumb. Na. BAG/4625/24

Kamishna wa Ardhi
S.L.P. 9230,
**DAR ES SALAAM.**

**Yah: Kurudisha Shamba Na. 39 lenye *LO*. Na. 99790**
**Kijiji cha Mapinga Wilaya ya Bagamoyo**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Maagizo ya barua Kumb. Na. CBC/156/171/01/25 ya tarehe 22 Mei, 2003 yamezingatiwa na Halmashauri ya Wilaya katika kikao cha kugawa ardhi cha tarehe 15 Desemba, 2003, kililiona suala hili na kutoa mapendekezo kwamba, mwenye milki hii arudishiwe. Napenda kuchukua fursa hii kukuomba ufanye *rectification* ya kumrudishia mmiliki yule yule bila mabadiliko mengine.

Nakutakia kazi njema.

MKURUGENZI MTENDAJI
k.n.y. AFISA MAENDELEO YA ARDHI WILAYA YA BAGAMOYO

Nakala: *Tanzania Investments Centre*
*P.O. Box 938,*
**DAR ES SALAAM.**

" Mkuu wa Wilaya,
**BAGAMOYO.**

" Mkuu wa Mkoa
**KIBAHA.**

" Afisa Mtendaji wa Kijiji,
Kijiji cha Mapinga
**WILAYA YA BAGAMOYO.**

" Ndugu B. S. Matiki,
S.L.P. 5767,
**DAR ES SALAAM.**

Wanakijiji hawa wa Mapinga walimwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kueleza malalamiko yao, lakini hadi leo hii bado hawajapata jibu lolote. Barua hiyo aliandikiwa tarehe 21 Aprili, 2004. Naomba kuinukuu barua hiyo:

Wanakijiji,
Kijiji cha Mapinga,
S.L.P. 274,
**BAGAMOYO.**

21 Aprili, 2004

Mheshimiwa Waziri,
Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi,
**DAR ES SALAAM.**

k.k. Mtendaji wa Kijiji,
Serikali ya Kijiji cha Mapinga
**BAGAMOYO.**

**YAH: MGOGORO WA ARDHI**

Rejea kichwa cha habari hapo juu.

Mheshimiwa Waziri, sisi wanakijiji wakazi wa Kijiji cha Mapinga, kwa heshima na taadhima tunapenda kufikisha kwako malalamiko yetu dhidi ya baadhi ya Watendaji wako ambao wanasababisha mgogoro mkubwa wa ardhi miongoni mwetu.

Kwa ufupi sisi ni Wananchi wapatao mia moja tunaomiliki sehemu ya ardhi iliyokuwa Shamba Na. 39 lenye hatimiliki Namba 32968 na Na. 1997990 ambayo ilimilikiwa na Bwana Babir Singh Malik wa *Rego Cashewnuts Provision Ltd.* Kwa historia mmiliki huyo wa zamani alimilikishwa shamba hilo mwaka 1987, kama mwekezaji katika kilimo cha korosho na viwanda vya kubangua korosho. Hata hivyo, mwekezaji huyo hakuwahi kuliendeleza hata kidogo.

Baada ya Wananchi kukerwa na pori nene lililohatarisha usalama wa raia na mali zao, pamoja na Serikali ya Kijiji, ilipendekezwa kwa Mamlaka husika ifute hati ya kumiliki ili Wananchi wengine wenye shida na kiu ya maendeleo wapewe. Kwa bahati Mamlaka husika waliyafanyia kazi mapendekezo hayo na tarehe 6 Septemba, 2001, wewe Mheshimiwa Waziri, kwa amri ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hati ya kumiliki ilibadilishwa kwa mujibu wa Gazeti la Serikali Na. 46 tarehe 16 Novemba, 2001 na barua ya Kamishna wa Ardhi ya tarehe 23 Oktoba, 2001 yenye kumbukumbu Na. ID/127954/21 iliyotoa taarifa ya ubatilisho kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Bagamoyo.

Baada ya ubatilisho huo, Serikali ya Kijiji iligawa eneo hilo kwa Wananchi walioomba, ambao wameweza kuliendeleza kwa shughuli za kilimo, makazi ya kudumu na hata uwekezaji kwa huduma za jamii kama shule, makanisa na kadhalika. Jambo la kushangaza na ambalo ndilo chanzo cha mgogoro unaonukia ni taarifa na mapendekezo ya baadhi ya Watendaji wako hapo Wizarani na hasa Afisa Ardhi wa Wilaya ya Bagamoyo, Ndugu D. L. Kilungu, yanayopingana na amri ya Rais ya kutaka ardhi hiyo irejeshwe kwa Bwana Maliki na kitendo cha Bwana Maliki kuja shambani kwetu kutufanyia fujo tena sasa kwa jina la *Mega Cashewnut Ltd,* sisi kama Wananchi wa kawaida, tumeona kwamba hapa kuna mazingira ya kutatanisha na pengine ipo misingi ya ulaji rushwa hasa, kwani hata Serikali ya Kijiji haikuridhishwa katika matendo hayo.

Sasa sisi tunauliza, wewe Mheshimiwa Waziri, jambo hili unalifahamu undani wake, je, unafahamu madhara yake kama kweli sisi Wananchi wako tutaporwa jasho letu? Mheshimiwa Waziri, tunaomba ufuatilie jambo hili kwa makini. Sisi kwa maandishi haya tunakujulisha kuwa, tumetangaza rasmi mgogoro dhidi ya udhalimu wowote utakaofanywa. Ahsante sana.

Ni sisi watiifu wako Wanakijiji,

Nakala: Mheshimiwa Rais.

" Taasisi ya Kuzuia Rushwa.

" Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

" Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri atoe mbele ya Bunge hili, taarifa kamili juu ya sakata hili na hatima ya Wanakijiji cha Mapinga juu ya nyumba zao na mashamba yao pindi shamba hili likirejeshwa kwa mmiliki wa zamani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nichukue nafasi hii kulipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa juhudi wanazochukua katika kupunguza tatizo la makazi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kusaidia kuinua maisha ya Wananchi wa Tanzania, hasa katika kuwa na nyumba bora na salama, ni vyema Serikali ikafanya juhudi za makusudi za kuhamasisha uundaji zaidi wa Mashirika ya Ujenzi wa Nyumba na Vyama vya Ushirika vya Ujenzi wa Nyumba za Bei Nafuu. Serikali ilianzisha Shirika la Nyumba la Taifa kwa lengo la kujenga nyumba au majengo ya aina mbalimbali kwa ajili ya kuishi au ofisi kwa madhumuni ya kupangisha na kuuza moja kwa moja kwa watu binafsi au Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Shrika la Nyumba la Taifa linafanya kazi, ukusanyaji wa kodi za pango ni muhimu na lazima, cha ajabu ni pale walipofungua kesi ya madai dhidi ya wateja wao. Mfano ni kesi ya hoteli ya *Etiens* ya Upanga Dar es Salaam, ambayo inadaiwa Sh.205,114,920/=. Baada ya kupelekwa Mahakamani na hukumu iliyotolewa ni kwamba, *NHC* wailipe hoteli hiyo jumla ya Shilingi milioni 600. Kambi ya Upinzani inaona hapa kuna kitu kilichojificha na kitaendelea kuitesa jamii nzima ya Kitanzania, hivyo, inamtaka Waziri atoe maelezo ya kina kuhusu hili kwa manufaa ya *National Housing* na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi na utaratibu wa Mashirika ambayo uanzishwaji wake ni kutoa huduma nyingine tofauti na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya watu kuishi au kupangisha, yanafanya kazi ya kutafiti na kujenga nyumba bila ya Shirika la Nyumba la Taifa kuhusishwa wakati ujenzi na utafiti wa nyumba za bei nafuu ni kazi ya Shirika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri alieleze Bunge kama kazi ya ujenzi wa majumba unaofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* imepewa baraka zote katika ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Hali hii ni kuliua kabisa Shirika la Nyumba lenye dhamana hiyo kutokana na uanzishwaji wake, kwani Mashirika hayo kuingia kwenye biashara ya *Real Estate* ni kuwa mshindani wa *National Housing* kwa kuruhusu Mashirika hayo yafanye biashara kama ya *National Housing.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi na miradi mingi ya nchi yetu inashindwa kutokana na tabia ya kutaka kufanya vitu vyote kwa wakati mmoja na kusahau ni lipi la msingi na linalotakiwa kupewa kipaumbele. Hivyo, mgawanyo wa shughuli ni muhimu katika uchumi wa karne hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke msukumo mkubwa kwa Shirika lake la Taifa la Nyumba kuendelea kujenga nyumba za kununua au kupangisha kwa Wananchi. Ni ishara kubwa kwa Wizara hiyo kuwa inatekeleza vyema dira yake. Wizara ishikamane zaidi na *National Housing* kuhakikisha ujenzi wa nyumba nyingi zilizo bora na za bei nafuu kwa ajili ya kuuza na kupangisha haziishii kule Boko Dar es Salaam tu, nyumba hizo zinahitajika nchini kote, kuanzia *Mbamba Bay* mpaka Kyaka, Tandahimba mpaka Namanyere, Ziwani mpaka Micheweni na Kiembesamaki mpaka Sirari. Bei za nyumba zinazouzwa zitilie maanani umaskini mkubwa wa Watanzania. Lengo liwe kuwapa makazi bora walalahoi wa nchi hii na siyo kuwaneemesha zaidi wenye nacho tayari.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizopo hivi sasa zinawalinda wadaiwa sugu wa Shirika hilo, kwani pindi wanapofikishwa kwenye vyombo vya sheria, wanatakiwa wakae bila kulipa kodi mpaka kesi itakapomalizika wakati chanzo cha kesi ni kudaiwa. Sasa hiyo si ni kuliongezea hasara Shirika hilo? Kambi ya Upinzani kwa hili, inamtaka Waziri pamoja na timu yake wafanye utaratibu wa kuziangalia upya sheria za upangaji na upangishaji ili kukabiliana na tatizo la wadaiwa sugu. Aidha, katika orodha hiyo ya wadeni sugu ni pamoja na Shirika la Magazeti ya Chama ambapo wanadaiwa deni la zaidi ya miaka saba. Inasikitisha kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo litawezesha dira ya Wizara itekelezeke kwa urahisi ni kwamba, upimaji wa viwanja na hasa vijijini, unaendelea kwa kasi ndogo sana kutokana na Serikali kutokuwa na wataalam wa kutosha wa shughuli za upimaji wa ardhi. Suala hilo linaweza kurekebishwa kwa Serikali kuruhusu wapimaji binafsi kupima viwanja. Serikali iwe na kazi ya kufuatilia utendaji kazi wa wataalam hao binafsi kama ni sahihi na unafuata maadili ya kazi ya upimaji au la. Kwa kuruhusu wataalam binafsi kupima viwanja, watu wengi wataweza kupatiwa viwanja vilivyopimwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, zimekuwa na uelewa wa kuweza kutenga fedha maalum za upimaji na uendelezaji shughuli za viwanja. Bado Wizara inalo jukumu la kusimamia kwa karibu zaidi zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kuweka mikakati ya kutokomeza adui rushwa na kupiga vita Ugonjwa wa UKIMWI ni suala lenye kuonesha mwelekeo wa Wizara kutekeleza dira yake kwa mafanikio mazuri na yenye matumaini. UKIMWI usipodhibitiwa kwa makusudi, utamaliza wataalam wote wa Wizara, ambao wamesomeshwa kwa gharama kubwa. Kuwapunguzia shida Wananchi ni pamoja na kuwa na sera za kulinda maisha ya wataalam wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara kuweka mikakati mizuri ya kuhakikisha kuwa Ofisi za Ardhi Wilayani zinaimarishwa ni suala lenye kutia moyo, kwani huko ndiko kwenye matatizo makubwa na ndiko Wananchi wengi waishiko. Utekelezaji huo utawezesha matatizo ya ardhi huko Wilayani na vijijini kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Wizara kupambana na rushwa ndani ya Wizara, ieleweke wazi bado rushwa haijamaliza katika Wizara hiyo. Juhudi za kufutilia mbali virusi vyote vya rushwa ni lazima zipambe moto zaidi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Benki ya Ardhi ni jambo zuri na la kimaendeleo ila kitu kikubwa cha kukiangalia ni Mkataba na masharti yepi, yasije yakawa kama yale yaliyomo kwenye Mikataba ya madini ambapo Wananchi hawanufaiki na chochote kwenye uwekezaji kwenye Sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri Wananchi wanaomiliki maeneo mazuri kwa uwekezaji wa kilimo au uwekezaji wowote, wapewe nafasi ya wao kuingia Mikataba kama *partners* na wawekezaji na wao wawe ndio na uwezo wa kutafuta Wanasheria kuangalia Mikataba hiyo na Wanasheria wa Serikali kuangalia maslahi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo habari kwamba, Wazungu wanaokimbia Sera ya Ardhi kupewa wazawa huko Zimbabwe ya Rais Robert Mugabe wanaikodolea macho Tanzania wakidai wao ni wawekezaji. Tunaiomba Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iwe makini sana na wawekezaji hao. Tanzania iwe makini kabisa na wawekezaji wageni katika ardhi ili kukwepa yanayoikabili Zimbabwe sasa hivi kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuishi katika nyumba bora ni haki ya msingi ya kila binadamu. Hata hivyo, bado kuna Watanzania wengi sana wanaoishi katika nyumba duni mno, mijini na vijijini. Lipo pia tatizo hasa katika miji, la watu wengi kutumia chumba kimoja, jambo ambalo ni hatari kwa afya, lakini pia linazo athari za kimaadili. Wapo pia Watanzania wengi tu wanaoishi viambazani na hata pembezoni mwa barabara na kwenye maeneo mengine mengi yasiyopendeza mwanadamu kuishi. Tatizo kubwa ni umaskini uliokithiri. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali ichukulie kuwa na nyumba bora ni sehemu ya kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ilivalie njuga tatizo la watu kukosa makazi bora. Kati ya mbinu zinazopendekezwa na Kambi ya Upinzani ni pamoja na Sekta binafsi kuwezeshwa na kuhamasishwa kujenga nyumba nyingi hasa mijini, ambazo zitapangishwa kwa watu wenye vipato vya kawaida na zitakuwa na gharama ndogo kwa sababu ya ruzuku itakayotolewa na Serikali kwa wajengaji na pia vifaa vyote vya ujenzi ikiwa ni pamoja na mabati, misumari, saruji na mbao na mazao yake vipunguziwe sana kodi ili vipatikane kwa bei za kawaida na hali hii imuwezeshe mwananchi wa kipato cha chini, angalau kumudu kujenga nyumba ya kawaida, lakini iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengi wanaofanya biashara ya kufyatua na kuuza matofali ya saruji, hasa katika miji mikubwa. Juhudi yao si mbaya, japokuwa mara nyingi wanaingilia maeneo ya barabara za mijini. Tatizo kubwa na linalohitajika kutupiwa macho haraka ni utengenezaji wa matofali yenye ubora wa chini sana, huku mchanga ukiwa mwingi na saruji ikiwa ni ya kubabaishia tu. Watu wengi huyanunua matofali hayo bila kujua ubora wake wa chini na matokeo yake yamekuwa ni nyumba zilizojaa nyufa na wakati mwingine nyumba kubomoka na kuumiza kama si kuua watu. Wizara ihakikishe watu wanaofanya biashara ya matofali na kadhalika, wanafanya shughuli hiyo siyo tu kwa lengo la kuganga njaa, bali pia kuzingatia viwango sahihi na kulinda maisha ya watu na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaendelea kuishauri Wizara ihakikishe kuwa, mikakati yake iliyowekwa inasimamiwa vizuri na inatekelezwa. Vile vile, inashauriwa iufanyie kazi kwa makini ushauri wa mara kwa mara unaotolewa na Kambi ya Upinzani. Lengo la jumla ni maendeleo ya kisasa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza kabisa katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita tumeondokewa na Wabunge wenzetu wawili, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na Mheshimiwa Yete Mwalyego. Kwa kweli ni pigo kubwa kwa Bunge letu kuondokewa na ndugu zetu hawa wawili katika muda mfupi namna hiyo. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu,

kutoa rambirambi kwa familia, ndugu na Wananchi wote wa Majimbo yote mawili ya Ulanga Mashariki na Mbeya Vijijini. Sote tunamwomba Mwenyezi Mungu, awalaze marehemu hawa wote wawili mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, napenda nirudi kwenye hoja nikimpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba yake nzuri kabisa, yeye pamoja na wasaidizi wake wote. Nawapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri. Kwa kweli hotuba ya Waziri imeeleza kwa kina kabisa mafanikio na matatizo mbalimbali ndani ya Wizara na mojawapo ya mafanikio hayo ni pamoja na mradi wa upimaji viwanja 20,000 kule Dar es Salaam. Huo ni mfano wa kuigwa kwa maana ya kuendeleza miji yetu. Narudia tena kusema nawapongeza kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijajisahau, napenda niunge mkono hoja ya Waziri kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanyika ndani ya Wizara, lakini bado pia kuna changamoto kubwa kwa kazi kubwa iliyoko mbele yao. Ni changamoto kubwa ambayo wenzetu hawa wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi wanapaswa kuwa nayo.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika ardhi ni *component* moja muhimu kabisa katika maendeleo ya binadamu na hasa maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote duniani na kwa bahati mbaya ardhi haiongezeki, lakini sisi binadamu tunaongezeka. Kwa hiyo, shughuli mbalimbali zinazofanyika juu ya ardhi hii zinahitaji basi kupangwa vizuri ili kuweza ku-*accommodate* ongezeko la watu na shughuli nyingi zinazoongezeka juu ya ardhi isiyoongezeka. Lakini kinyume chake inakuwa ni mgogoro mkubwa ambao unafanya Wananchi wasielewane.

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mizuri. Wengi wetu wamesikia au kuona migogoro katika nchi jirani au nchi mojawapo rafiki katika nchi hizi za *SADC*. Sina sababu kuitaja, kwamba, kulikuwa na mgogoro mkubwa kutokana na ugawaji uliokuwa siyo wa halali au wa haki wa ardhi. Kwa hiyo, sisi tunapaswa kuwa macho na nasema Wizara iwe makini katika kuangalia inahakikisha ugawaji wa ardhi na mipango yake, matumizi sahihi na matumizi bora yanakuwa makini na endelevu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kidogo juu ya migogoro. Migogoro mingi ya ardhi inatokana na mipango mibovu ama ya utekelezaji katika kugawa na kumilikisha Wananchi au mara nyingine kutokuwa makini katika suala zima hilo. Mipango hiyo inaweza kuwa ni ya makazi ya watu, mashamba, maeneo ya mifugo na kadhalika. Migogoro hiyo imekuwepo baina ya mtu na watu, mtu na Taasisi au wawekezaji na Wananchi. Mara nyingi kutochukua hatua sahihi kwa wakati imekuwa ni tatizo kubwa katika kuendeleza migogoro katika nchi yetu. Kwa mfano, kule kwangu Babati, katika Jimbo la Babati Magharibi hata hivi karibuni niliuliza swali Bungeni nikihitaji fafanuzi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nitoe mifano miwili ambayo ningeomba Serikali iweze kuiangalia. Nitoe mifano ya Kata mbili. Kuna Kata moja inaitwa Kata ya Arri ambapo kuna migogoro kati ya wamiliki na wanavijiji. Pale kuna *RIVACU* ni *Cooperative Union* hawaelewani vizuri na watu walioko pale jirani. Pia, kuna wawekezaji ambao ni *Breweries* hawaelewani na Wanavijiji. Wanavijiji wanapoona ardhi imekaa pale, mapori makubwa yamekaa bila matumizi wanaona kama vile hawatendewi haki. Kwa hiyo, ni vizuri wenye ardhi hiyo basi wakawa na ushirikiano mzuri na jirani zao.

Vile vile, kumekuwa na zoezi la umegaji wa sehemu ya ardhi au mashamba ambapo Wananchi walioko pale jirani wameweza kuwa na muafaka wa kuishi pamoja na hao wawekezaji au Taasisi kama hiyo niliyosema ya *RIVACU.* Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikahakikisha kwa mfano Halmashauri ya Wilaya wakashirikiana na Wizara ya Ardhi kutatua matatizo hayo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kutosha ili Wananchi hao wajue namna ya kuweza kuji-*integrate* pamoja na hao wamiliki wa mashamba makubwa.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni katika Kata nyingine inayoitwa Kata ya Ufana, ambapo migogoro ya ardhi ya mashamba inahusu zaidi mtu na mtu hususan wenye nguvu na wanyonge na pengine Serikali ya Kijiji au Kata wamekuwa *biased* katika maamuzi ya kugawa ardhi au kugawa mashamba au mara nyingine Serikali ya Kijiji imekuwa haina upande. Sasa yule mwenye nguvu ndiyo anamkandamiza mnyonge na mnyonge anajua hawezi kumpeleka Mahakamani au mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine tulilonalo katika Wilaya ya Babati limekuwa ni kutokuwepo na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na ya Kata. Hili limeweza kufanya tatizo la ugawaji ardhi au migogoro ya ardhi kwa pamoja kutotatuliwa katika muda muafaka. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali sasa ikafikia mahali ikafikisha migogoro hii kwenye tamati yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nizungumzie suala la Mipango Miji. Hapo mwanzoni nilizungumza habari ya kazi nzuri walizofanya Wizara hii katika kugawa au kupima viwanja 20,000 kule Dar es Salaam. Huu mpango kwa kweli ni wa kuupongeza. Sisi tuliwahi kutembelea mradi ule na tuliona kwa kweli ulikuwa ni mradi *comprehensive*, wamepanga maeneo yale vizuri kabisa, barabara zimetengenezwa na kadhalika.

Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Serikali ikaiga mfano ule au ikatoa *replica* ya mpango ule katika Miji mbalimbali hapa nchini na mimi ningeomba Mji wetu wa Babati ambao ni Makao mapya ya Mkoa mpya wa Manyara kazi hiyo au zoezi hilo likafanyika mara moja kadri inavyowezekana. Angalau basi siyo kwa *scale* ile ya Dar es Salaam, hatuwezi kusema viwanja 20,000 katika Mji wa Babati, lakini hata viwanja 2,000 itasaidia sana ku-*enhance master plan* ya Mji mpya kama ule. Kwa hiyo, naomba Wizara ilipokee hili na hususan hii Miji mipya ambayo inachipukia katika nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini vile vile, suala zima la kupima *plots* katika Miji *(surveys),* ni vizuri likafanyika kwa wingi zaidi kuliko kufanyika *individually,* kwa sababu tatizo kubwa ni gharama ambayo mtu mmoja mmoja inakuwa vigumu kuistahimili. Nitoe mfano jinsi gharama ilivyo kubwa sasa. Kupima eneo la nusu ekari, kwa mfano, pale Mji wa Babati

inagharimu Shilingi milioni 1.1 ili kuweza kupimiwa halafu pia na kupata hatimiliki. Ukiangalia gharama kama hiyo, siyo rahisi ku-*afford* kwa Wananchi wetu *individually.* Kwa hiyo, inaonesha kwamba, tatizo hili bado linahitaji kuangaliwa katika namna yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, unapopima kiwanja kimoja kimoja pale Babati inabidi Afisa wa Ardhi afuatilie *reference points* Mjini Arusha na ataku-*charge* Sh.200,000/= kwa gharama hizo. Lakini kama ni kikundi cha watu au viwanja hivyo vinapimwa kwa wingi mfano viwanja ishirini au thelathini, gharama ya kumtuma mtu huyo ni gharama hiyo hiyo peke yake ya Sh.200,000/=. Lakini kama leo mimi nikimtuma mtu awe anaenda Arusha, kwa mfano, kutoka pale Babati kufuata *reference points* Arusha kwa Sh.200,000/= na mwingine hivyo hivyo na mwingine tena hivyo hivyo, inakuwa ni gharama ambayo ni *inflated unnecessarily.* Kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Serikali kwa kusaidia Wananchi wake katika miji ikajaribu kufanya jambo hili la kupima viwanja *collectively. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni nilivyoanza nilisema Wizara hii imefanya kazi nzuri, Wizara hii imeainisha matatizo mbalimbali, kwa hiyo, inajua inaenda kufanya nini. Nafikiri nizidi kuwaunga mkono, tutawapa hizi fedha wanazoomba ili wafanye hii kazi yao vizuri ambayo wametuletea kama mipango yao na basi niendelee tena kuwaunga mkono ili wawe na moyo wa kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru kwa nafasi hii ya kwanza uliyonipa asubuhi ya leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kabisa kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji wa pili katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, kaka yangu, Mheshimiwa Gideon Cheyo.

Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na wenzangu ambao wametangulia kuchangia hotuba hii kwa kutoa pole kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kuondokewa na ndugu yetu mpendwa, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, nitangulie tu kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ninachangia hapa mara ya tatu na kila nikisimama nasema kwamba, hatuna matatizo kabisa na shughuli ambazo wanazifanya wenzetu kutoka kwenye Wizara mbalimbali. Kwa hiyo, nirudie tu kusema ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa kazi nzuri anayoifanya toka amekuwepo katika Wizara hii, kwa kweli ina mabadiliko makubwa sana. Ametusaidia sana kuweza kupunguza kero ambazo zilikuwa zikitukera huko majimboni kwetu tunakotokea. Nimpongeze Naibu Waziri, dada yangu, Mheshimiwa *Al-hajat* Tatu Ntimizi, kwa kazi

nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na ndiyo maana anapata mafanikio haya. *(Makofi)*

Lakini vile vile, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana na hasa Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Ardhi, dada yangu mpendwa, Mama Salome Sijaona, kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa kweli kwanza ameacha milango yake wazi, wakati wowote utakapomhitaji yuko tayari kukusikiliza na kuacha shughuli zake zote ili ahakikishe ...

**WABUNGE FULANI:** Milango wazi!

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Eeh, milango ya ofisi zake, hata ya nyumba yake. Kwa hiyo, tunaingia kwa mapana na marefu kuweza kuelezea shida zetu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msinielewe vibaya nina nia nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yeye pia anasaidiwa na watendaji wa Wizara hii kwa maana wanafanya kazi nzuri, Mungu awabariki sana. Kama nilivyosema, sina tatizo kabisa na hotuba hii, lakini kama kawaida yetu Waheshimiwa Wabunge, tunahitaji kumsaidia Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla. Kwa hiyo, pale ambapo tunaona yapo mapungufu kidogo ni lazima tusimame na kuyasemea ili na sisi tuweze kuweka michango yetu kwa nia ya kuboresha na kuweza kuona kwamba Wizara inakwenda vizuri. Leo nina mambo mawili tu ambayo nitayazungumzia katika mchango wangu. Jambo la kwanza ni haya matatizo ama sijui niite migogoro ambayo imekuwepo na kwa kweli nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri kwamba, migogoro mingi ya ardhi iliyopo na inayoendelea, Mheshimiwa Gideon Cheyo ameikuta, imekuwa ni ya muda mrefu sana, kabla hajapewa Wizara hii. Lakini kwa upeo wake mkubwa toka ameingia ameweza kujitahidi kuitatua kwa asilimia kubwa sana. Bado ipo migogoro ambayo sisi tunaweza tukaisemea ili tumsaidie aweze kuimaliza haraka, nayo ni hii migogoro ya viwanja. Nimekuwa nikimsumbua sana Mheshimiwa Waziri kumletea watu toka nimeingia hapa Bungeni, kwa sababu mimi ninapotokea, katika Wilaya ya Temeke, tumekuwa na matatizo mengi ya migogoro ya viwanja. Kwa hiyo, toka nimekuja Bungeni ninamletea Wananchi wangu ambao wana malalamiko ya viwanja ya muda mrefu na kwa kweli amejitahidi akaweza kuitatua kwa haraka. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili la Bajeti pia nimeshamletea Wananchi wangu kutoka Temeke ambao wana matatizo ya viwanja ya muda mrefu, inawezekana mimi nilikuwa shuleni. Mengine yalitokea mwaka 1978, ni muda mrefu sana. Kiwanja namba 144 Kitalu D kilichoko Temeke, kiwanja hiki kiko nyuma ya Ofisi ya Wilaya ya CCM, kina tatizo la muda mrefu sana kama nilivyosema, kuanzia miaka hiyo sisi tulikuwa bado tuko shuleni. Tatizo hilo limekuwa likiendelea kwa mawasiliano mbalimbali kabla madaraka hayajapelekwa kwenye Halmashauri zetu kushughulikia, Jiji lilikuwa likishughulikia. Kwa hiyo, limekuwa ni la muda mrefu sana na ndiyo maana nimesema kwamba, matatizo mengine ambayo yapo kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo, ni yale ambayo ameyakuta. Kwa hiyo, inakuwa ni tatizo kabisa kwa sababu unakuta wenzake walishaji-*commit* kuyatekeleza, lakini bila kuzingatia taratibu. *(Makofi)*

Kwa ruksa yako ninakuomba sana unisamehe, inawezekana nitakuwa ninakiuka kidogo, niwasimamishe ndugu ambao wamekuja ku...

**SPIKA:** Endelea tu na hotuba yako.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Ahsante. Lakini nia ya kuja ni kuja kumshukuru kwa sababu ameshafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, wanampongeza sana. Ninachotaka tu kusema ni kwamba, tunatunga mambo mazuri sana, lakini tatizo liko kwenye utekelezaji. Mheshimiwa Gideon Cheyo, anaweza akaelekeza kwamba nataka hili litekelezwe hivi, lakini wale wanaopewa dhamana ya kulitekeleza jambo inakuwa ni tatizo kubwa sana kulitekeleza kama alivyoagiza. Hili ndiyo tatizo ambalo linawakuta Waheshimiwa Mawaziri kwa maana ya Watendaji wanaoelekezwa, jamani nendeni mkalitatue kwa kufuata kanuni na taratibu. Wao wanakwenda kukiuka zile taratibu ambazo wameelekezwa. Kwa hiyo, mgogoro huu wa kiwanja hiki pamoja na Mheshimiwa Waziri kuonesha nia nzuri kabisa ya kuweza kulitatua suala hili kwa haraka, lakini bado Kamishna wa Ardhi anamwangusha kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwa kusema kwamba Kamishina wa Ardhi anamwangusha kutokana na barua ama na jinsi amekuwa akiwasiliana na kikundi hicho chini Mwenyekiti, wake ndugu yangu Simbila ambayo ni kamati imeundwa kutoka kwa walalamikaji hawa ambao ni waumini wa Kanisa la *Evangelist Assembles of God.* Hawa wamekuja kufuatilia suala hili, lakini wanapata matatizo na Kamishna wa Ardhi hataki kulitekeleza kwa haraka kwa kuzungusha mara nendeni kwenye Halmashauri, mara rudini huku. Sasa ule mzunguko umekuwa ni mrefu.

Kwa hiyo, mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na nia yake nzuri, ajaribu sana kuongea na Kamishna wa Ardhi, ili aweze kumwambia bwana nikikuagiza hiki basi fanya inavyotakiwa badala ya kuwasumbua wananchi. Taratibu zimekiukwa barua zote wanazo kuna faili kubwa sana hapa lina mawasiliano na Mheshimiwa Waziri kwa bahati mbaya walikuwa wanamficha hawamfikishii hili faili. Kwa hiyo, Ofisi ya Wizara ya Ardhi kulikuwa kuna mafaili zaidi ya nne suala moja. Kwani wanapohitaji kumwona Waziri, wanafika wanakuta kuna ukuta mkubwa sana wa kuwazuia kwenda kueleza matatizo yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kwa nia nzuri kabisa kaka yangu ninakuomba kabisa uone mapungufu haya katika Wizara yako, ili uweze kuyafanyia kazi na kwa kweli kama ulivyoona siku ile ya tarehe moja tulipokutana kantini na waumini hawa wako kwenye maombi ya kuiombea Serikali hii iendelee kufanya kazi zake vizuri pamoja na wewe. Ninakuomba utumie busara kwa kusukumwa na uwezo wa Mwenyezi Mungu uweze kulimaliza suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimelisema hili kwa kirefu, naomba sasa kama nilikueleza kuna nina mambo ya mawili. Naomba sasa kuongelea suala la pili, siku zote huwa nikisimama hapa nakuambia kabla sijaja Bungeni, nilikuwa ni mfanyakazi wa Shirika la Nyumba la Taifa.

Sasa ninataka nizungumzie suala hili kwanza niwapongeze sana kamati ambayo imechambua hotuba/bajeti hii ya Waziri wa Ardhi, wameligusia matatizo ya Shirika la Nyumba la Taifa na niwapongeze pia Kamati ya Upinzani na wao wamelizungumza kwa kirefu kwamba yako matatizo kwenye hili shirika.

Hili shirika tusipoangalia tunataka sasa *life* na tunampa ugumu sana Mkurugenzi wa Shirika la Nyumba la Taifa, kwa sababu wanapoleta mapendekezo yao kwa utaratibu kabisa ili waweze kupandisha kodi yao na waweze kujiendesha kibiashara lakini ipo sheria inayowabana na kuwaruhusu upande wa pili ili waweze kupinga. Kwa hiyo, wamekuwa na kesi za muda mrefu, sasa itafikia mahali watashindwa kujiendesha. Lakini naomba nichukulie tu kwa mfano kwa akili ya kawaida ukififikiria nyumba za Shirika la Nyumba bado bei yake iko chini kuliko nyumba za watu binafsi. Lakini bado watu hawaoni umuhimu wa kufikia kuzipandisha bei kwa sababu utapata matengenezo na kadhalika. Lakini pia unaishi kwa amani. *(Makofi)*

Sasa mimi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, kwa kweli pia nikupongeze kwamba umejitahidi kwa kiasi kikubwa kuweza kulisimamia shirika hili, ili liweze kufanikisha. Lakini bado uongeze jitihada zingine kuhakikisha wanapoomba kupandisha kodi zao basi waweze kukubalika. *(Makofi)*

Labda niseme njia nyingi ambayo wanaweza kuitumia ni njia ya ushirikishwaji basi, wasilale wakaamka tu wakafikiria kwamba sasa tunapandisha bila kuweza kuwashirika wapangaji. Jaribuni kukaa pamoja wakajadiliana. Kamati hii iliyochambua imesema kwamba wajaribu kufanya mikutano ama kutoa elimu kwa wapangaji. Kwa kweli na mimi hili nililikuwa naliona ni suala la msingi sana. Toeni elimu kwa wapangaji ili waone umuhimu wa kupokea yale ambayo mnayataka na kisha mtaweza kwenda pamoja badala ya kubaki tunavutana, sisi tunapandisha wengine wanagomea wanafungua kesi kwa hiyo, tunakuwa hatufanikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niliona nichangie haya na kwa kweli sikuwa na mengi ya zaidi, zaidi ni kuwapongeza sana kwamba Wizara hii inafanya kazi nzuri na nirudie kusema tu kwamba ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. RHODA L. KAHATANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi. Niruhusu nitoe pole kwa familia ya Comrade Kasapira ambayo imepotelewa na mpenzi wao. Mungu awape subira na ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba niunge mkono hoja. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Gideon Cheyo, Naibu Waziri *Al-Hajat* Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu, Ndugu Salome Sijaona na watendaji wote wa Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi yao nzuri ambayo tumeiona kwa kuiona kwa macho tunapokuwa huko katika shughuli zetu katika Wizara ile na jinsi tulivyoona mipangilio yao walivyochambua hotuba yao katika kitabu hiki cha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juhudi za Waziri na watumishi wenzake zimejionyesha hakika katika Wizara hii. Misululu tuliyokuwa tunaiona katika Wizara ya Ardhi imepungua, manung'uniko ya watu wanapokwenda pale Wizarani na walivyokuwa wanadharauliwa na hata vijana wadogo kabisa katika ile Wizara imepungua, jinsi wanavyoweka shughuli zao katika kompyuta inawarahisishia kupata kumbukumbu za viwanja vya watu na kwa kweli watu wengi wanasifu sasa hivi Wizara hii. Tunamshukuru Mungu, kwamba walau tunaweza kupata Wizara ambazo zitakuwa zinaonyesha utendaji wake mzuri, maana kitu kimoja kimoja ndicho kinaweka kikubwa na familia moja moja ndiyo inaunda taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nizungumzie katika viwanja ambavyo Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wamevipima, vimeonyesha mfano mzuri. Kule Dar es Salaam wamepima viwanja 20,000 na viwanja vile watu wake wamepata hati mara moja walio wengi ambao waliovinunua bila kuchelewa. Kazi ile ni nzuri lakini naomba Wizara kama inaweza iendeleze katika sehemu nyingine ya nchi kwa sababu makazi yanahitajika kwa wingi sana sehemu mbalimbali. Kama walisema wanapima viwanja hivyo kwa mfano kwa utaratibu wa kuangalia kama vitawezekana kuendelea. Sasa mimi namwomba Waziri na wenzake waweze kutafuta wapate fedha hawa wafadhili kama walivyopata katika viwanja hivi 20,000 ili waweze kwenda katika Mikoa mingine ambayo kuna shida nyingi za kuendeleza makazi katika Jiji la Mwanza na Miji mingine ambayo inakua kwa haraka haraka katika nchi yetu ili waweze kupima wananchi wawaze kupata viwanja hivyo na wajenge nyumba kama tunavyohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuzungumzia juu ya mashirika yanayojenga nyumba. Kuna mashirika mengi katika nchi yetu yamejitolea kujenga nyumba juhudi tunaiona kwa *NHC* wanajenga nyumba lakini mara nyingi wananchi hawapati fursa ya kununua nyumba zile kwa sababu zinajengwa chache na kwa sababu hawana fedha. Tumeona katika nchi nyingine wanavyofanya. Kwa mfano, mimi nilikwenda Botswana nilikwenda kutembelea Wizara ya Ardhi, nikawauliza wanafanya nini juu ya kujenga nyumba? Wakaniambia wao nyumba zinajengwa na mashirika mbalimbali na wana fedha za kuweza kuwakopesha watu. Kijana akitoka Chuo Kikuu, wanamwuliza unataka gari au unataka nyumba? Sasa pale ndipo anawekeana mkataba na kijana ambaye anakwenda kuanza kazi anayetaka gari watamkopesha gari, anayetaka nyumba wanamkopesha nyumba. Kwa hiyo, anakatwa mshahara kwa kadri alivyopewa.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nilipochangia katika Bunge hili nimeomba sana iwepo *financial institution* ambayo itakuwa inaweza kuwakopesha wananchi fedha za kuweza kununua nyumba. *(Makofi)*

Lakini inaonekana jambo hili linachukua muda mrefu sielewi ni kwa sababu gani. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, akae pamoja na wenzake Waziri wa Fedha, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa sababu ya utaratibu ule wa sheria Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais Utumishi na Mawaziri wengine watakaohusika na watu wenye mabenki wakae wazungumze kwa sababu jambo hili linatuchelewesha na pengine ndiyo linafanya hata vijana wetu wakaingia katika maofisi wakashawishika kupokea rushwa ili waweze kujenga nyumba wakae na wake zao na waume zao kwa

raha. Labda wakiwa na nyumba wakipata mara moja wanaweza kupunguza kupokea rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binadamu unajua ana mambo anayohitaji nyumba ni mojawapo ambayo hata katika imani yetu ya Tanzania, Watanzania tunasema nyumba ni muhimu na katika nchi zetu watu wanaona kwamba nyumba ni muhimu. Sasa hivi kijana anaanza kazi hana nyumba anamwona mtu kama Spika, anaingia pale anatafuta kiwanja kwa nini asimtoe upepo? Atamtoa upepo ili akajenge nyumba. Lakini kama amewekewa namna ya kupata nyumba yake kwa kukopeshwa sidhani kama atasumbua watu kuwatoa upepo kwa kuzungumza njoo kesho, njoo keshokutwa au unajua jua kali mambo kama hayo yatapungua. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ninaomba kwa dhati kabisa kwa uwezo alionao Waziri wetu wa Ardhi akae na wenzake na Waziri wa Fedha, naona yuko hapa wakae, yuko Waziri wa Utumishi, pale atapanga mipango ya kuwakata mishahara hawa wafanyakazi wake ili wapate nyumba zao wataridhika na nyumba zitakuwa na heshima kubwa kwa watu hao. Tunajua nyumba za Serikali sasa zimeuzwa hawa vijana wanaomaliza Vyuo vyetu Vikuu, hawa watu wanaokwenda mahali pengine watapanga wapi? Zikiwepo nyumba za watumishi huyu akienda Mwanza, huyu akija Dar es Salaam atapata nyumba ya mwingine aliyekuwepo pale. Huyu akienda Mtwara, mwingine Mbeya watakuwepo na nyumba za watu wengine waliokopa. Kwa hiyo, tutakuwa tunapunguza hasira za watu na tutapunguza joto katika mioyo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba jambo hili litiliwe mkazo sana. Ninapenda pia baada ya kuwepo chombo hicho cha kukopesha sasa vijana wetu na watu wengine wanaofanya kazi zao wenyewe wafanyabiashara kikiwepo hicho chombo kiratibu hizo benki sasa zinakopesha vipi kiangalie vile vile wasimpe mtu hela mkononi. Tunajua kwamba mtu akipata fedha mkononi wengine unajua tena wengine maadili ndiyo hivyo akipata hela zake mkononi ndiyo jioni baridi moja, moja moto na nyumba haijengwi. Kwa hiyo, zijengwe nyumba ndiyo watu wapewe, siyo wapewe hela mkononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wapangaji naomba Mheshimiwa Waziri, alete *bill* tuweze kuibadilisha hapa Bungeni kwa sababu sasa hivi hali inakuwa ngumu.

Mpangaji akitakiwa kuondoka katika nyumba hawezi kuondolewa mpaka kesi iende mahakamani, inakuwa kesi ya madai. Tunavyojua kesi za madai zinachukua miaka mingi. Kwa hiyo, hata kama tukiwa na mashirika yanayojenga nyumba yatakata tamaa kupangisha watu nyumba kwa sababu wataogopa kwamba kutakuwa na kesi ambazo zitasumbua badala ya kuendelea tutahangaika.

Kwa hiyo, ninaomba ile *bill* ya kubadilisha kesi za wapangaji ibadilishwe mwenye nyumba awe na uwezo wa kumwondoa mtu anayekaa kwenye nyumba. Sasa watu wengine nyumba zao hata watu binafsi anakuwa amejenga nyumba yake imkomboe labda atakapostaafu, amejinyima yeye na familia yake, sasa mtu akiingia ndani ya nyumba hatoki. Ukimtoa ni kesi. Sasa kukiwa na kesi za namna hiyo, mimi mali ni yangu

nimejenga nyumba ni yangu na huyu hajanitimizia malengo yangu, kwa nini nisimtoe? Kama mtu aliazima kanga yangu si nitaichukua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, ailete haraka sheria hii na ninaomba Waheshimiwa Wabunge, waibadilishe hiyo sheria, watu wanaopanga nyumba za watu wakishindwa kufuatana na utaratibu waliowekeana waondoke kwenye nyumba ndiyo maana shirika la nyumba linapata shida kwa sababu wapangaji wengi hawajalipa na hawawezi kuwaondoa mpaka kesi ziende mahakamani na mahakama tumesema hapa juzi tuna mahakimu wachache. Sasa kesi inaweza kukaa miaka mitatu, miaka minne hata miaka kumi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, jambo hili ulitilie maanani na tupate hiyo sheria tuweza kuipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho narudia kumshukuru Waziri lakini ninaomba uratibu ule walionao pale Wizarani, waupeleke mpaka Wilayani kwani Wilayani kule ambako kuna kasheshe. Watendaji wa Ardhi kule ni watu wa ajabu. Kuna Mheshimiwa Mbunge siku moja alisema juu ya watendaji wa kata kwamba ni kama miungu watu. Lakini watendaji wa ardhi kwenye Wilaya ni miungu watu wale. Tunaomba yale mema yaliyopo pale Wizarani yashuke mpaka kwenye Wilaya zetu. Hilo ni ombi maalum kwa Waziri ninaomba kabisa awaangalie watendaji wake katika Wilaya, ili nao wamuige baba na mama. Sasa mtoto unamzaa halafu anakuwa na hali tofauti jambo hili linatisha kabisa katika Wilaya zetu, kuanzia zile zilizopo Dar es Salaam, zipo jirani na yeye lakini apite pale azingalie hatujui watendaji wake wanafanya hivyo kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Waziri aangalie Wilaya zake na utendaji wake na kutumiza matakwa ya Wizara kwa Maendeleo ya Ardhi na Makazi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mchana huu. Naomba niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wana Jimbo wa Marehemu Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nina haki ya kuipongeza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa jitihada ambazo wameanza kuzionyesha na ambazo kwa kweli pengine zitatuondolea kero iliyokuwepo. Naelewa kwamba ardhi si tatizo kwa Watanzania. Ardhi kama ilivyo si tatizo, tatizo linaweza kutoka katika utaratibu na mipango yetu ya jinsi ya kuitumia. Halafu na jinsi tunavyochukua hatua kunapokuwa na matatizo. Lakini kama ni ardhi kwa ukubwa hiyo inatutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Wizara hii imekusanya shilingi bilioni 5.8 na inaomba matumizi ya shilingi bilioni 6.3. Kwa hiyo, kwa njia moja ama nyingine hii Wizara ni Wizara ambayo inaweza ikajiendesha kwa njia moja au nyingine. Basi kama ni hivyo tunaweza tukatumia ni kitu inachokitumia ili kukusanya

mapato yale kwa wingi ili sasa kipanuliwe na wakati huo huo tukiiongezea hela za matumizi ili sasa iweze kufanya kwa ufanisi zaidi kuliko inavyofanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la kwamba wamepima viwanja Dar es Salaam watapata hela. Sasa nilichotaka kushauri kwa leo, amezungumza Mheshimiwa Waziri, kwamba wana mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Taifa, mpango ule kwa kweli umechelewa sana. Pamoja na umaskini wa Watanzania na kwa msingi wa nadharia za Ki-*Max* ardhi ni mojawapo ya vitu ambavyo ni kama mtaji na kitu cha msingi sana. Sijui nikumbuke ni lini lakini nilisema hapa Bungeni, kwamba kitu ambacho Mwenyezi Mungu, ametusaidia na Baba wa Taifa, alitusaidia ni kuweka utaratibu ambao kila Mtanzania, anaweza akapata kipande cha ardhi ama aweze kujenga nyumba ama aweze kulima shamba kama akipenda. Sasa tungeiomba Wizara hii katika mpango huu iuharakishe ili iweze kutusaidia kwa sababu ardhi tunayo ya kutosha, lakini tunayo matatizo makubwa na ndiyo maana kwa sababu ardhi tunayo ya kutosha na hatujaitumia vizuri kila siku tuna migogoro kati ya wafugaji na wakulima. Sasa unatafuta wanachogombania ni nini na watu wanakufa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, huu mpango uharakishwe kwa sababu nimeona kuna mipango kama mitatu, huo wa taifa, uko wa vijijini, halafu uko na wa Wilaya. Kule kwetu wakati wa Waingereza, walikuwa wakigawa ardhi, kila viwanja tisa, kiwanja cha kumi wanaita *Mkama Land,* ardhi ya *Chief* wanagawa tisa cha kumi *Mkama Land* kwa maana ya kwamba watu watakaokuja kuishi pale pengine itakuwa shule ile ambayo wameita ya Mkama ile au pengine watajenga hospitali au pengine watajenge *cemetery.*

Lakini baada ya hapo kila mmoja akawa anajigawia walipowapa Serikali za vijiji bila utaratibu anakuja Mwenyekiti na karisiti kake anapiga hatua kumi anagawa ardhi zote. Wakazigawa ardhi zote hawana pa kujenga shule. Ukiwauliza ninyi kama kijiji tafuteni ardhi maeneo mengine ya kwetu kule hawana, tujenge shule ya sekondari hawana wanaanza kukimbizana na shamba la mtu wanamnyang'anya.

Wakati wa ukoloni kwenye maeneo ya mabonde kama kule kwetu walikuwa wakigawa pale kwenye chanzo cha maji, kama wamekugawia eka tano na wanataka kukupa eka kumi wanaruka maili fulani pale kwenye chanzo cha maji, pale bondeni halafu wanakupa sehemu nyingine kama ile ardhi haikutoshi. Lakini baada ya uhuru watu wakaponya unamkuta mtu amechukua chanzo cha maji anasema na hapa ni kwangu tena nyinyi msichote maji hapa anawafukuza watu. *(Kicheko)*

Sasa mambo kama haya ni kero na ndiyo maana tunaposisitiza hapa kutunza vyanzo vya maji, unakuwa ugomvi kwa sababu kuna mtu anaelewa kwamba ile ardhi ni haki yake ni ya kwake, ninyi hamuwezi kumwambia asilime pale kwenye chanzo cha maji. Kwa hiyo, tungeomba kwamba hili lishughulikiwe na wawaeleze kwamba wanapogawa ardhi na kuipangilia wawe wanapanga kwamba miaka 50, miaka 200 ijayo tutajenga wapi? Siyo mtu anataka pale, kijiji kinataka ardhi wameitana Halmashauri ninyi tutakaowagawia mtupe hela, wanataka hela tu bila ya kuangalia kwamba miaka 20, miaka 30, miaka 50 ijayo watajenga wapi kwa ajili ya upanuzi na kwa idadi ya watu inavyoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo, haitoshi kuna maeneo mengine kwa sababu ya rutuba na kwa sababu ya jiografia yake yanakua yana-*attract* watu wengi wanakwenda. Niliwahi kumwuliza Waziri wa Maliasili na Utalii, hapa kuna watu aliwafukuza huko kwangu walikuwa karibu na maeneo ya *game reserves,* iko ya Ibanda, iko na nyingine ya Rumanyika Rugundu. Sasa watu wamehama kutoka sehemu za Bukoba, kutoka Ngara, kutoka Bihalamulo na sehemu nyingine. Sasa wale waliokuwa wanaweka mpaka wa *game reserve* hata wao hawakuwa wanawauliza wenyeji mipaka ilikuwa wapi, kila mmoja alikuwa anafika anajiwekea tu anavyotaka.

Sasa unakuta kwamba watu wamekuwa wengi katika eneo lile na eneo halipo na nyingine imeshakuwa *game.* Sasa kinachoshangaza katika Wilaya hiyo hiyo ya Karagwe lipo pori linapakana na jimbo la Mheshimiwa Sebabili, Mbunge wa Ngara la Kimisi wamekwenda pale wameletewa madiwani kwamba Serikali inapendekeza sasa lile eneo litengwe liwe ni eneo la *game.* Madiwani wamekataa.

Lakini uongozi wa Mkoa umetumia nguvu na nadhani umekwisha kufikia kwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwamba eneo lile limetengwa rasmi. Kwa sababu tunapozungumza hapa mtu unatakiwa ulete ushahidi, Waziri wa TAMISEMI, Mkurugenzi aliyoko kule ni mtu wake na Serikali ikitaka iwaulize ni nini uamuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe. Maana ukichukua eneo lote walikuwa na *game reserve* ziko pale, iko Bungi, sijui iko wapi. Wakachukua na eneo la Kimisi bila ya kujua kwamba watu wanaongezeka wakapeleka Serikalini bila ya kufuata utaratibu wa kwamba ardhi ile ilikuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba Wizara hii inapotayarisha mipango hiyo na kwa sababu tumepitisha Sheria ya Ardhi ya Vijiji na marekebisho yake. Nadhani lengo kubwa ni kwamba ardhi ile itumike kuondoa umaskini si kwa kulima mle bali itumike kama kuweka dhamana katika mabenki. Sasa katika hili naomba kuishauri Wizara kwamba ishirikiane na Wizara ya Fedha kwa karibu na nikisema kwa karibu sasa kama wanakutupieni shilingi bilioni sita na nchi hii ilivyo kubwa na bado Waziri wa Fedha anasema sisi tunataka kuona watu wanakopa, tunataka kuona watu wamepima, wanapima utapima viwanja vingapi nchi nzima kwa shilingi bilioni sita (6) hizi? Kwanza hizi hela za maendeleo sijui ni bilioni ngapi.

Kwa hiyo, sisi tunachosema kwamba mshirikiane kwa karibu maana sisi tunaweza kukaa kama Wabunge tunamsulubu Waziri kwa nini hakutekeleza kazi zake lakini tunashindwa kujua kwamba hakuwa na vifaa vya kutendea kazi. Kwa hiyo, hilo kwanza tunashauri kwamba mshirikiane kwamba karibu na Wizara ya Fedha, kwa sababu Wizara ya Fedha, haiwezi kusema yenyewe inataka kusaidia kuunda vyombo watu wakope na kuyaambia mabenki wawakopeshe watu wakati watu hawa hawana hati za kumiliki ardhi hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, ni jukumu la Mheshimiwa Waziri mwenyewe, sijui hela utatumia hizi walizokupa sijui utaomba zingine mimi sielewi. Hiyo sheria tuliyoitunga, tumeiwekea mazingira gani iweze kutekelezeka vizuri? Maana kuna sera ndiyo

tumeitungia sasa sheria. Lakini nasema tuandae mazingira kwamba sheria hii unaitekeleza vipi kwa sababu si suala la kuwaamrisha watu kwamba ninyi watu wote mguu pande, mguu sawa au kila mmoja aje hapa amevaa suti *no,* ni suala la kwamba ungependa watu ardhi yao ipimwe, iwe *registered* isajiliwe, ramani ichorwe, atengenezewe hati na akabidhiwe ili anapoipeleka pale kwenye benki na wale wenye benki kwa mujibu wa sheria zinazoendesha vyombo vya vya fedha waweze kuikubali. *(Makofi)*

Sasa hatua hizo haziwezi kufanyika kama kuamrisha mvua inyeshe hasa tukilenga kwamba tunalenga nchi nzima kwa sababu ile huwezi kusema tutaanza Kinondoni lazima tuseme ni nchi nzima. Sasa mngekuwa mmetupigia zoezi hili linaweza kuhitaji gharama gani kwa nchi nzima, ama tutafika baada ya miaka mingapi, kwamba sheria tumeipitisha, kweli ni nzuri tumeshangilia, tunataka kuwaambia watu watumie ardhi waliyonayo ndiyo wawe na hati za kwenda kuomba mkopo katika benki. Sasa zoezi hili litachukua miaka mingapi na ni fedha kiasi gani ambacho kinahitajika katika kulikamilisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si kushirikiana tu na Wizara ya Fedha na Wizara nadhani ya Sayansi na Teknolojia, wao wameshamaliza bajeti yao. Lakini nadhani wangekuona mkashirikiana, maana tumepitisha hapa Bungeni kwamba kama ninyi tunakupa mkopo unaleta hati ya shamba ya baba yako, sasa wao wanataka hati hawataki kukusaidia? Maana mambo hayo sasa tunaona kwamba tunaingilia hata anayekwenda kusoma sasa ataguswa na baba yake kuwa na hati miliki, japo huku utaratibu wa kijiji mmeueleza hapa kwamba kijiji kutoa sijui hati miliki kwa ile ya kurithishana. Lakini hata hii haiwezi kuishia hapo watu wanahitaji kupewa semina. Mwenyekiti wa Kijiji haelewi anachopaswa kufanywa ni nini, siyo wanakaa kaa hapo kiurasimu. Kwa hiyo, utaona mambo haya yote yanahitaji mafunzo na yanahitaji kufikishwa kule na lazima tuyapangie ratiba ya utekelezaji. Ratiba ya utekelezaji na akina nani watatekeleza na miongozo na gharama za kuwafikisha kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hawawezi kukwepa hata watu wa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, lazima na wao washiriki katika zoezi hili. Pia huwezi kukwepa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, maana mambo yaliyotokea pale Dar es Salaam mlipokuwa mnabomoa nyumba za watu kujenga barabara inayokuja kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kikwete pale Chalinze. Mtu ramani imepimwa mwaka 1936, mwaka 1970 mkaanza kuwagawia tena anagawa pale mtu wa Wizara ya Ardhi na ramani na sheria ya ardhi, anakimbia pale inaandikwa anawakatia watu vipande anawapa wanajenga. Mwenye barabara anasema tunabomoa, wanapobomoa anasema tena bomoa, kama hutaki tunaleta tingatinga halafu unalilipa. Akianza kuhoji, wanamwambia shenzi tena unatuchelewesha. Hivi yeye anapata adhabu peke yake kwa sababu gani? Kwani aliyemgawia hapaswi kupata adhabu? Kwa sababu yule aliyemgawia na ana risiti alikusanya na kodi sijui na ramani na hela zote wakajilimbikizia kwa nini kwenye kumhamisha huyu mnafukuza yeye? Au Serikali waliochukua hizi hela walizochukua hizi hela wakaweka kwenye fungu na wakamgawia kwa nini wao wasiwajibike? Hatuwezi kuwapiga viboko, lakini kuwajibika kwamba angalau na wao walipe gharama si ndiyo walimgawia zingine walimgawia? Sasa mtu wa kawaida ametoka kijijini, hata kama ni mjini yeye hajui walipita hapa mwaka 1930 waligawa hiyo sheria haijui ramani

hana, huyu wa ardhi ana ramani na kila kitu anakijua na utaratibu anaujua anawagawa pale yeye mnampa adhabu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo haya yana maudhi kwa sababu sasa hivi mnachora alama za*'X'* kwenye nyumba za watu kwamba barabara tunataka inyooke, kwani lazima barabara inyooke kuelekea kwenye nyumba ya mtu? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1975 tulianzisha vijiji vya ujamaa na kwa lengo zuri Baba wa Taifa akasema watu waje kwenye vijiji, waje kwenye *center* tuweze kuwapa maji na waliokuwa wanakataa siku hizi ndiyo wanajileta kwenye *center,* kwenye miji midogo tuliyonayo. Lakini sasa wakati wa ugawaji kama kawaida wale waliokuwa wanagawa wanapiga hatua, hivi anakwenda anapiga hivi kwenye barabara anamgawia mtu, mtu anajenga nyumba. Hawakujua kama hiyo sheria ipo ya mwaka 1976 sijui imefanyiwa marekebisho sijui ya mwaka gani. Sasa leo hii mnamwambia hii mnamwambia uondoe nyumba yako, kwanza alikuwa amekaa na mababu zake kwenye bonde mlimtoa akapatekeleze na wengine wakapavamia, akaja hapa njiani na kuna *ruling* ya mahakama nadhani sijui ya rufaa kuhusu hayo mambo waliokuwa wanagombania ardhi waliopewa watu wakati wa vijiji vya ujamaa, sijui hiyo mnaionaje na kwamba amekaa pale zaidi ya miaka 12 katika masuala ya ardhi. Sasa leo hii mnamkuta pale mnamwambia tumekupa *warning* utoe nyumba yako, atoe nyumba yake si walimgawia? Tukisema *competition* mnakuwa wakali.

Mheshimiwa Spika, hayo ni mambo ndiyo tunayasema yanatakiwa yaangaliwe vizuri. Mimi nilikwenda wakati wanaweka alama za *'X'* kwenye nyumba za watu nikauliza sasa kuna utaratibu gani? Mimi Mbunge sijui, Mkuu wa Wilaya, aliyekuwepo pale kwangu akasema hata yeye hawakumwuliza. Sasa jamani hata kama tunataka kufanya ili watu wafurahi hata Mkuu wa Wilaya hamumwambii? Lengo ni zuri lakini nasema tushirikiane kuambizana. Kwa hiyo, ndicho ninachosema kwamba hii mipango mnayopanga, kila Wizara inajipangia mipango wake, halafu inapokuja Wizara nyingine nayo ina sheria ya kwake, anafanya madhara kwa watu kwa kweli huu siyo utaratibu mzuri wakati Serikali ni moja lazima muitane muambizane ili kufanikisha majukumu ya Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru mimi kwa nafasi uliyonipa na namshukuru Waziri.

**WABUNGE FULANI:** Unga mkono.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono siyo kwa kushinikizwa isipokuwa kwa kupenda naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kwa mujibu wa orodha ya waliomba kuchangia kwa mdomo kwenye hoja hii wamebaki wanne (4) na kipindi cha mchana kinawatosha wote 4 kwa hiyo wajiandae nao ni Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Profesa Mikidadi, Mheshimiwa Edward Ndeka na Mheshimiwa Edson Halinga. Hilo moja.

Asubuhi hapakuwa na nafasi ya kutoa matangazo lakini kulikuwa na tangazo moja la kikao cha Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Anne Makinda Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira wakutane leo saa saba mchana tukitoka hapa katika ukumbi Na. 231 ghorofa ya pili.

Taarifa kuhusu mabadiliko ya ratiba yetu kutokana na tukio la jana kwa hiyo, sasa tunahamishia mbele siku moja moja. Maswali ambayo yangejibiwa yatajibiwa Jumatatu na Wizara ambayo ingewasilisha hoja leo itawasilisha Jumatatu. Kwa hiyo, tunahama siku moja moja, hatimaye tutakapofika siku mbili za mwisho Ofisi ya Rais, Mipango ilipangiwa siku moja na Wizara ya Fedha, ilipangiwa siku moja. Sasa haitawezekana tena itabidi zote zitoa hoja zao kwa pamoja kama walivyofanya mwanzoni zijadiliwe kwa pamoja halafu ndiyo tukamilishe Bajeti za Wizara moja moja. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa Wabunge sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliahirishwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweli) Alikalia Kiti*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii leo hii na ninaunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia, kwa niaba yangu na kwa niaba wa Jimbo la Kitongoji, natoa mkono wa rambirambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kufuatia kifo cha Mheshimiwa Kasapira. Mungu amlaze mahali pema Peponi na awape subira ndugu wa Marehemu hapa duniani. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ambayo tunaizungumzia ni Wizara muhimu sana na ni tegemeo kwa umma wa Watanzania. Kwa hiyo, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majukumu makubwa ya Taifa hili ambayo ameyasimamia na anategemea kuendelea kuyasimamia. Namtakia mafanikio na kwa kweli tunamtegemea ili kuondoa matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kumpongeza tu Mheshimiwa Waziri kwa majukumu makubwa anayoyasimamia kwa Taifa hili na kwa kweli juhudi zake zimeonekana na kwa kweli Wizara yake naweza kusema ni Wizara muhimu kati ya Wizara muhimu za nchi hii, kwa sababu masuala ya ardhi yanamgusa karibu kila mtu katika nchi hii tukiwa idadi yetu tuko karibu watu milioni 34 wanategemea wapate maeneo ya kulima, maeneo ya kuweza kujenga nyumba za kuishi ambayo ni mambo ya msingi kwa mwanadamu yeyote yule anayeishi hapa duniani. Kwa hiyo nimesimama

hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri na kwa kweli majukumu yake hayo ayafanikishe ili aweze kuondoa matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niipongeze Wizara hii kwa mafanikio makubwa. Mwanzoni mwa mwaka huu tulifanya ziara ya Mkoa wa Kagera na tukatembelea mipaka yetu ya Tanzania na Uganda. Kwa kweli kazi kubwa iliyofanywa kuwekwa mipaka ile, nataka niipongeze Wizara hii ya Ardhi kwa sababu ninaamini kwamba ilishiriki kwa asilimia kubwa katika kufanikisha suala lile. Tukiangalia alama moja ya mpaka ilipita katika mlima mmoja mkubwa sana, kwa hiyo nampongeza Mheshimiwa Waziri na aendelee kufanya kazi hii kwa maeneo yote ya mipaka ya nchi yetu ili kuweka alama za Taifa hili ili kuondoa migogoro ya ardhi baina ya nchi na nchi ili tushughulikie matatizo yaliyoko ndani ya nchi tu. Zile *beacons* ambazo ziko kule mipakani, naomba ziwe za kudumu, isiwe yale mawe tu na udongo uliowekwa, zijengwe kwa saruji na ikiwezekana ziwekewe zege la uhakika ili kuondoa migogoro baina ya nchi na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitumie nafasi hii niiombe Serikali iipatie fedha za kutosha Wizara hii ili iweze kushughulikia mipaka ya nchi yetu na nchi ambazo tumepakana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 15 amesema kwamba katika mwaka 2004/2005, mwelekeo wa Wizara unatoa kipaumbele katika maeneo makuu matatu, naomba niyanukuu. Anasema, "Kwanza ni kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali; pili, ni kuwawezesha wananchi kutumia raslimali ya ardhi ili kuwaondolea wananchi umasikini; tatu, kuimarisha Utawala bora katika Sekta ya Ardhi ili kutoa uhakika wa miliki za ardhi sambamba na kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini." Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Hili ndilo tunataka katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kupata maendeleo ya nchi hii bila kuwa na umoja. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe binafsi, Naibu Waziri na Watendaji wake wote pamoja na zile Wizara ambazo zinashughulikia masuala ya watu ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kweli waweke nguvu ya pamoja kuweza kuliona suala hili. Maeneo haya matatu yamepelekea nisimame hapa nimuunge mkono.

Kwa kweli ndio msingi mkuu wa maendeleo wa Taifa letu hili, kwa sababu wananchi kama watakuwa na migogoro ya ardhi, kama watakuwa na migogoro katika maeneo yao ya kuishi, hatuwezi tukafikia yale malengo ambayo Serikali imekusudia. Kwa hiyo, namtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri na ninampongeza sana na tunamtegemea sana kwa hekima zake na utendaji wake mkubwa wa kazi ili aweze kufanikisha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa huo huo wa 15, Mheshimiwa Waziri amesema, Wizara imeweka lengo la kukusanya jumla ya Sh.5,896,650,000/=, kwa kweli

nampongeza sana. Lakini makusanyo haya yatakapokusanywa, ninaomba yatumike kama yalivyokusudiwa. Kwa kweli juhudi hizi ambazo wametupa mwanzo kabla hawajaianza hii kazi, makisio haya na malengo haya watakapofanikisha fedha hizi zitumike vizuri kama ambavyo zimekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo wa 15 Mheshimiwa Waziri ameelezea kuhusu huduma za maendeleo ya ardhi. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Nikimnukuu, amesema: “Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara iliendelea kutoa huduma za maendeleo ya ardhi zenye misingi ya lengo la kuimarisha utawala bora ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umasikini.” Hongera sana Mheshimiwa Waziri. Taifa linapigana na mkakati wa kuondoa umasikini na ardhi ndio msingi wa mwanzo ambao unaweza kuondoa wananchi wetu katika matatizo ya umasikini tukiamini kwamba asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo.

Kwa hiyo, yale matatizo ambayo yako katika ardhi katika Taifa letu na yale maeneo ya mashamba makubwa ambayo yanamilikiwa na matajiri, yamepakana na wananchi wetu wa kawaida ambao vilimo vyao ni vidogo vidogo, kuna vyanzo vya maji; ningeiomba kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, suala hili liangaliwe. Tunahitaji amani na utulivu kwa wananchi wetu na Taifa letu. Vile vile katika eneo hili hili, kwa yale ambayo mwaka 2003/2004 hayakufanikiwa, naomba Wizara hii iyasimamie na iweze kuyafanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kubwa, tumeona mgogoro wa ardhi ulivyotokea Zimbabwe, tumeona wenzetu Namibia wanavyofanya *operation* juu ya kuwashughulikia wananchi wao kupata ardhi. Kwa hiyo, Serikali ichukue hatua ya kuwapatia wananchi ardhi ili kuondokana na migogoro huko mbele ya safari. Kwa hiyo, namsisitizia Mheshimiwa Waziri kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wizara imekusudia mambo mengi sana na mimi nataka niipongeze sana. Kwa kweli kama watafanikisha haya ambayo wametueleza kwenye hotuba yao, kwa kweli tuna matumaini makubwa kwamba Taifa letu kwenye miaka ile ambayo imekusudiwa ya Dira ya Taifa mpaka 2025 tutafikia malengo hayo kwa mafanikio makubwa sana kwa sababu utulivu wa wananchi wetu ndio utakaoipa Serikali kuweza kutulia na kuweza kupanga mambo mengi na kufikia katika maendeleo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa sababu nimesimama hapa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, nina moja nataka nilizungumze kwa dhati kabisa.

Kwa muda mrefu Magazeti mbalimbali yalikuwa yanazungumza habari ambazo zilikuwa zinamgusa Mheshimiwa Waziri Mkuu na juzi ilipokuwa ikichangiwa hotuba ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilimgusa vile vile. Kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ustahimilivu wake mkubwa sana. Nimwombe kwamba asijaribu kujibu. Utendaji wake au usimamizi wake mkubwa wa Serikali ndio unaomsumbua. Mafanikio ya Serikali yetu kama ingelikuwa Waziri Mkuu ni mwepesi, tusingelifikia hapa kama tulipofikia. Kwa hiyo, aweze kuangalia wenzetu Wapinzani

hawa wana malengo gani? Wanachotafuta ni kumtoa katika *site* aliyopo wampeleke kwenye *site* ambayo nchi itaweza kuyumba. Kwa hiyo, hili alizungumza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Pia, nataka nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa yale majibu aliyoyatoa juzi. Lakini vile vile na mimi niiagize Wizara hii kwamba kama ni kweli shamba hili Mheshimiwa Waziri Mkuu analo au hanalo, naomba mara moja Wizara imtafutie shamba Waziri Mkuu. Sio kosa Waziri Mkuu kuwa na shamba! Hii ni nchi yake! Kama shamba hili halina kibali, naomba mara moja Wizara impe kibali rasmi alimiliki shamba hili. Waziri Mkuu ni yeye, familia yake haitaweza kufaidika na yale maposho au mambo mengine ambayo yatahusu kwa maisha yake ya baadaye. Huyu akimaliza Uwaziri Mkuu wake kuna mafao yatamgusa, lakini familia yake hayawezi kuwagusa.

Hakuna Waziri Mkuu yeyote duniani aliyekuwa maskini. Tunamwona Waziri Mkuu wa Italia pale tunasikia kwamba anataka kununua timu pale Uingereza. Wanawekeza katika Mataifa mbalimbali. Tunamwona Makamu wa Rais wa Marekani anamiliki Makampuni ya Mafuta. Haiwezekani! Kama jambo hili lilikuwa likifanywa kwa siri, mimi nazungumza kwa dhati kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu asibishane na hawa watu, tutakachomwomba aamue kujiuzulu ni sisi CCM, Serikali ya CCM na Wananchi wa Tanzania kwa ujumla, sio Viongozi wa Vyama vya Siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza kwa sababu nina ushahidi. Pamoja na shutuma zote ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amefikishiwa, lakini wananchi wa Tanzania kote alipokwenda amepata mapokezi makubwa ya kusikiliza Mikutano ya Wananchi na maelekezo aliyokuwa anatoa Wananchi waliyatekeleza. Kwa hiyo, nimesimama hili kuliunga mkono kwa dhati kabisa na ninalizungumza kwa uwazi kabisa. Kwa kulumbana hatuwezi tukafikia maendeleo ambayo tumeyakusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka nipeleke ombi maalum kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivi karibuni nimempokea mama yangu mmoja anaitwa Mariam Hamisi, anatokea sehemu za Tabora. Kwa kweli alikuja kuomba msaada kwa sababu nyumba yake imo katika mpango wa kubomolewa ili kujengwe barabara pale Tabora. Hakukataa kuvunjiwa ile nyumba yake, lakini anaomba kuna eneo ambalo tangu utoto wake walikuwa wanalima na mama yake, alikuwa anaomba tu lile eneo apewe ili aweze kujenga nyumba nyingine na tatizo lake kubwa ni kwamba eneo hili amepewa mtu anataka kujenga Kituo cha Mafuta. Ningeiomba Wizara hii iliangalie iweze kumpokea huyu mama tatizo lake na anakaa sehemu ya Chem Chem, *House Na.32.* Kama liko Wizarani naomba Wizara ilipokee kama halipo kwao naomba walitafute waweze kumsaidia.

Mama huyu anamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wake na Viongozi wengine mbalimbali aliokutana nao. Huyu mama ni Muasisi wa *TANU* na CCM kuna barua nyingi ambazo nimeziona zilizoandikwa na akina Paul Sozigwa, alipokutana na Mheshimiwa Spika huko Serikalini na mambo mengi sana. Kwa hiyo asaidiwe ili

kutimiza haya malengo ambayo amesema Mheshimiwa Waziri kwamba ardhi ndio msingi utakaoondoa umaskini. Suala la Makazi ni suala muhimu kwa mwanadamu yeyote, kwa sababu binadamu unaweza kuhangaika mchana kutwa lakini lazima upate eneo la kuweza kuishi na uweze kuendesha maisha yako kwa ajili ya familia yako. Idadi kubwa ya watu tuliopo Tanzania milioni 34, ninaamini kila mmoja anahangaikia apate eneo la kuishi ili aweze kuendesha maisha yake. Kazi anaweza kufanya eneo lolote lile, lakini makazi ni jambo la msingi kwa mwanadamu yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa dhati kabisa, nasema nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri, ninamtakia mafanikio makubwa, aangalie kwa haraka sana mipaka yetu baina ya nchi zile jirani hasa kule Uganda, Rwanda, Burundi na hata suala la Malawi limalizike kwa haraka sana ili tufikie muafaka wa kuweza kujua eneo letu na ikiwa inawezekana kama hakuna fedha tunaomba Serikali iipatie Wizara hii fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuunga mkono Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia na ninamtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDWARD N. NDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Kabla ya kufanya hivyo, naomba mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, nitoe salamu za rambirambi kwa msiba uliotupata hapa Bungeni wa ndugu yetu Kasapira, Mungu aiweke roho ya Marehemu huyu mahali pema Peponi na ndugu zake, Wapigakura wake awape subira katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya rambirambi hizo, naomba nimpongeze Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu wake na timu nzima ya Maafisa katika Wizara yake na zile Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hiyo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuandaa hotuba hii ambayo tunaijadili hapa Bungeni. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia hotuba hii, nimeona kipaumbele kimoja ambacho amekiainisha Waziri ambacho ni kupima maeneo ya Vijiji ili kuviwezesha Vijiji kupata hati za kumiliki ili kuimarisha amani na utulivu katika Vijiji hivyo pamoja na kuviwezesha kushiriki vyema katika masuala ya maendeleo. Kipaumbele hiki ni kizuri kwa sababu kinatoa fursa kwa maeneo ambayo yako chini ya Wizara yake katika suala la ardhi hasa Vijijini. Lakini kipaumbele hiki cha utekelezaji kwa ajili ya kupata malengo yaliyokusudiwa, nasikitika kusema kwamba hakikuonyeshwa na kipaumbele katika kuainisha maeneo ambayo yangepaswa yapewe katika kipaumbele katika kufikia malengo ya utekelezaji wa Wizara hii. Nitatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti ya Maafa ukurasa wa kwanza, Wakimbizi ni miongoni mwa majanga yaliyoainishwa ambayo yanapaswa yadhibitiwe. Kwa kuwa matatizo yanayoandamana na Wakimbizi ni miongoni mwa majanga ambayo yameainishwa kwamba ni majanga ya Kitaifa, inafuatia moja kwa moja kwamba mipango ya kuendeleza upimaji katika maeneo ya Vijiji

yangepaswa yaone hilo kama ni janga ambalo lazima lichukuliwe hatua katika kuwezesha kufikia malengo hayo ya kuleta amani ya kuwawezesha wakazi katika maeneo hayo kuimarisha shughuli zao za uzalishaji na kiuchumi. Mkoa wa Kigoma una Makambi ya Wakimbizi kumi. Mkoa jirani, Wilaya ya jirani yetu Ngara, kuna Makambi matatu. Mkoa wa Tabora eneo la Illalangulu kuna makazi ambayo zamani ilikuwa ni Kambi sasa hivi ni makazi ya Wakimbizi na katika Mkoa wa Rukwa, Wilaya ambayo ni jirani ya Mkoa wa Kigoma ya Mpanda ina makazi matatu. Kwa maana hiyo, ukanda huu kuanzia Mkoa wa Kagera, Kigoma yenyewe na Rukwa ni ukanda ambao kwa mujibu wa sera hii ni ukanda ambao uko katika maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ingetazamiwa kuwa mipango ya Wizara hii ya upimaji wa maeneo ili yaanishwe vizuri, Mkoa wa Kigoma na Ukanda wa Magharibi kwa ujumla ungekuwa katika kipaumbele katika utekelezaji wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Vijiji 232 vya Mkoa wa Kigoma, ambavyo vimepimwa ni Vijiji 34 tu. Hii ni sawasawa na asilimia 14. Kwa hiyo, ni matarajio yangu sasa kwamba kwa kutumia kigezo hiki, Wizara itaelekeza upimaji wa Vijiji hivi katika Mkoa huo uongezeke kwa kasi ya ku-*manage* janga hili la Wakimbizi. Kwa sababu kutofanya hivyo kunatoa nafasi ya walio katika Makambi haya wawe wanaingia katika maeneo ya Vijiji na Vijiji kwa sababu ya kutokuwa na mipaka ambayo imeainishwa haviwezi kusimamia kwa ukamilifu maeneo yao katika suala la maendeleo ya Vijiji vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo kingine ambacho Wizara inapaswa ikizingatie ili kufikia malengo hayo ukiacha hilo la janga lililoainishwa na sera hii ni kuwepo kwa eneo kubwa katika ukanda huo wa Magharibi, eneo la Ramsa. Hili ni eneo ambalo Tanzania iliridhia Mkataba wa kulitunza kama raslimali ya dunia. *Ramsa site* ambayo iko katika ukanda huu inagusa Mikoa minne; Mkoa wa Kigoma, Shinyanga kwa Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Tabora kwa Wilaya ya Urambo na Sikonge na Mkoa wa Rukwa kwa Wilaya ya Mpanda. Eneo hili linazungukwa na Vijiji. Ni eneo kubwa lenye hekta zipatazo milioni 3,250,000. Vijiji vinavyozunguka maeneo haya kama havijapimwa, usimamizi wa eneo hili ambalo Tanzania imelipokea na kulisimamia kwa niaba ya dunia hautaweza kufanikiwa bila hatua za kupima na kuanisha maeneo ya Vijiji vinavyozunguka katika eneo hili. Ni wito wangu sasa kwa sababu kutopimwa kwa Vijiji hivi kumeleta mgongano kutoka makundi mbalimbali na sera hii, mkakati aliouonyesha Waziri, shabaha mojawapo ya kutekeleza mkakati wa Wizara yake ni kuondoa migogoro ya ardhi kati ya makundi na makundi. Kutopima maeneo ya Vijiji kumesababisha mgongano kati ya wakazi wa Vijiji na Taasisi zilizoko katika maeneo hayo. Mfano dhahiri, kwa kuwa mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Kilimo na Ardhi, niliuzungumzia hata kwenye Kamati, ni mgogoro uliopo kati ya Taasisi ya Magereza na Kijiji cha Ilagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mvutano na Kijiji cha Ilagala na kwa mujibu wa taarifa ya Waziri, hakijapimwa. Mgongano mwingine umekuwepo kati ya Mbuga za Wanyama kwa mfano Mbuga ya Mahale na Vijiji vinavyozunguka mbuga ile hususan Kijiji cha Kalilani ambacho nacho kwa mujibu wa taarifa hii hakijapimwa. Kwa hiyo, wananchi katika eneo hilo la Kijiji cha Kalilani, wanapofanya shughuli zao Mbuga

ya Hifadhi ya Taifa ya Mahale inawaambia kwamba wanaingia katika eneo la mbuga ya wanyama. Ningeomba hilo liangaliwe kwamba upimaji wa Vijiji katika ukanda huo wa Magharibi na hususan Mkoa wa Kigoma ni mahitaji ambayo yanapaswa yapewe kipaumbele kwa ajili ya kufanikisha malengo ya maendeleo katika sehemu ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo kingine ambacho tungepaswa kukitumia ni mgogoro ambao upo kati ya Wawekezaji na Vijiji ambamo wanawekeza. Mfano hai ni Kiwanda cha Chumvi cha Uvinza na Kijiji cha Uvinza ambacho nacho kwa mandhari yake na ukubwa wake kingestahili kuwa Mji Mdogo, bado kwa mujibu wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri hakijapimwa. Huyu Mwekezaji anaelekea kuchukua maeneo mbalimbali katika Vijiji vinavyozunguka eneo la mgodi wake. Sasa kama hili halikuchukuliwa hatua, mgogoro na matumizi ya rasilimali zilizoko katika eneo hilo utaendelea. Kiwanda kile kinatumia kuni toka misitu ya asili inayozunguka eneo hilo. Kama hatua za upimaji vijiji za makusudi hazitafanyika, basi tutakuwa katika matatizo ya maendeleo katika ukanda ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa rai hizo na ambazo naamini Wizara ni makini kwa sababu nimekuwa nikifuatilia jinsi wanavyopanga mambo yao, ni matarajio yangu kwamba katika kuainisha vipaumbele, maeneo gani yapewe vipaumbele kwa shabaha hizo za maendeleo, lazima vigezo vinavyohalalisha vipaumbele vizingatiwe na kwa matumaini hayo, niseme hotuba ya Waziri na mipango aliyonayo, naiunga mkono asilimia mia. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache niliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Wizara hii miaka ya nyuma ilikuwa ni kati ya Wizara zilizokuwa zinatia mashaka, zilizojaa fikra ya rushwa, lakini leo hii ni Wizara ambayo kwa kweli ni ya kuitumaini sana. Mimi nataka nitoe pongezi kabisa kwa Waziri, Naibu wake na hasa Katibu wake Mkuu. Katibu wake Mkuu amefanya vitu vya ajabu na kushangaza wananchi wa Jimbo langu. Amekusanya viongozi wote na Makamishna wote wakaenda Vijijini kufanya Semina na kutoa hatimiliki za kimila na kupima mashamba kutambua mashamba 1,400 katika Jimbo langu Vijiji saba. Kazi hii wameifanya kuanzia asubuhi mpaka jioni kila siku. Sasa unaweza kuelewa kuwa kweli hawa ndugu zetu wameelewa maana hasa ya kumkomboa Mtanzania mwenye matatizo. Ningeziomba Wizara nyingine ziige mfano huu. Suala sio kukaa Ofisini, sio kukaa Dar es Salaam ukafikiri mambo yatakwenda. Hatuwezi kwenda hata kidogo! Kwa hiyo nazidi kuwapongeza sana na kwamba ninaunga mkono Bajeti ya Wizara hii asilimia mia. Ninaomba wote tuiunge mkono kama mfano wa kwanza wa kufanikisha shughuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vilivyopata hati walifanya kwa wazi na kwa hakika. Mimi kwa mara ya kwanza nilikuwa na wasiwasi, lakini mama mmoja mjane katika Kijiji cha Halungu amepata hatimiliki ya kwanza katika nchi hii ya Tanzania. Kwa kweli inaonyesha wazi kwamba kama utaratibu utafanyika, basi akinamama watakomboka katika masuala ya kunyanyaswa na ardhi na hii ndio itakuwa ukombozi

kwao maana hati zile watakwenda kukopa katika Mabenki na kuendeleza maisha yao na kujithamini wenyewe wasidhalilishwe na wanaume. Utaratibu huu wa hatimiliki za kimila hauna gharama, ni suala la watu kwenda kujuana mlivyokaa pale kwenye eneo lenu, mnakubaliana na mnawekeana sahihi Kijijini, mnapewa hati. Lakini hizi hati za kutaka kupima na kuwekewa beacons zina gharama na tusitegemee kuwa kuna watu wataweza. Sasa kwa njia hii ya hatimiliki za kimila, mimi nadhani ndio ukombozi wa kwanza kwa wananchi wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika nilikuwa naomba kwamba hivi vijiji vina tatizo moja havina uwezo wa kuwa na masjala ya kuweka vitabu na *documents* zinavyotakiwa kwenye kijiji.

Kunahitajika *safe,* jengo zuri, ma-*cabinet* na nilikuwa naomba Wizara kama ingelifikiria sana hapo ama ikatoa mkopo kwa vijiji vilivyo tayari kujenga watajenga wenyewe kwa vijiji vilivyo tayari wakakopeshwa vifaa hivyo vya kutunzia hizi *documents* nadhani ingetusaidia sana na ingefanya mambo haya yaende haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ningeomba kwamba Wizara itusaidie kuongeza watendaji. Kwa kweli hawatoshi maana kule kwangu kila kijiji kinataka kipate utaratibu huu wa kutoa hati za vijiji. Watendaji ni wachache mno, wako kama watano pale Wilayani.

Kwa kweli kitu hiki kitatuletea mifarakano maana watu wamefika mahali hawakubaliani na wanashinda Ofisini kuwataka wale watendaji waende wafanye shughuli hizo katika vijiji vyao. Ninaomba mkitufanyia hivyo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu tunawakopesha vijana mikopo, lakini nani anaweza kusema vijana ni mikopo gani wamechukua imeleta maendeleo. Hakuna. Unampaje kijana mkopo akautumie wapi.

Hana ardhi, lakini utaratibu huu kijana anaweza akamiliki eneo lake akiwa kwa mzazi wake na vijana wa namna hii kama wangepewa mikopo hii wakiwa na uhakika kuwa wana ardhi wanayomiliki wangezalisha na tungefanikiwa kuleta mabadiliko ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Lakini hii mikopo ya kuwapa wafanye biashara hawatakwenda mahali. Fanya biashara hata nyumba yenyewe ya kufanyia biashara hana atafanyia wapi?

Mimi nadhani hata mikopo hii ya vijana hata ya akina mama ingezingatia sana kuona kwamba wana ardhi wanayomiliki kwa hati hii miliki ya kimila ndipo waweze kufanyia kazi na kuzalisha kile wanachohitaji. Na vile vile tuna tabia hii ya kujenga majengo yetu, miji yetu ya kuweka tu mistari.

Sasa hii mistari hii haitatusaidia sana. Tunapanua sana maeneo, na tunazuia maeneo yote ya kulima. Nadhani tufike mahali tukubaliane kuanzisha utaratibu wa

kujenga hata ghorofa mbili, tatu mahali kijijini, kuacha maeneo ya kulima yawe yanatosheleza katika vijiji. *(Makofi)*

Lakini kwa tabia hii ya kila mtu eneo lake analolima ndiyo ajenge nyumba tutafika mwisho tutakwama. Maana sasa hatutakuwa na maendeleo na hawa wanaozaliwa sasa na kukua walioko shuleni watapata wapi maeneo ya kuzalisha. Nadhani tukae tuangalie na sera ijaribu kuliona hili suala litusaidie kuleta mabadiliko yanayoweza kusaidia.

Vile vile hata miji yetu hii, tunaipa miji midogo, lakini ukiona miji midogo majengo yaliyoko pale hayamo katika utaratibu. Hivi kwa nini tusiwe na utaratibu wa kusema miji yoyote inayopewa hadhi ya kuwa mji lazima iwe angalau ina ghorofa tatu, nne, tano kianzio ili kuonyesha kuwa kweli kuna watu. Hata ukienda nchi za wenzetu huko ng'ambo wao unafika mahali unapata kijiji tu pana ghorofa mbili tatu, ndiyo zinaonyesha kuwa hapa watu wanaishi. Lakini sasa sisi tunakwenda hata ukiangalia vijiji vyetu hivi unaweza usiamini kuwa hapa kweli watu wanaishi.

Umeme tunaoudai sana utaingia wapi? Lazima tuwe na utaratibu, maana maendeleo haya hata ungesema hali hii wananchi ndivyo walivyo. Lakini ndivyo walivyo mpaka lini? Lazima tuwe na taratibu za kwamba vijiji vina majengo yanayokubalika. Ndipo tunaweza tukapiga hatua ya mabadiliko ya hali ya usafi ya miji yetu na vile vile hali inavyoonekana katika Wilaya zetu. Na ndiyo maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mara nyingi nimekuwa nikipigiwa kengele, leo nadhani afadhali niwahi. Nashukuru sana kwa nafasi hii. Na nawapongeza sana Wizara hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na kuwaomba wasirudi nyuma. Isije ikawa tunamsifu mgema sasa tembo akalitia maji, hapana.

Tunaomba kwa kweli washike uzi na Makamishna ni watu wenye juhudi na moyo wa kazi hii. Wakazane ili kuliweka Taifa letu katika hali ya uwezo wa kuendeleza maendeleo yetu. Ahsante sana. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Waziri kwa hotuba nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, upimaji wa vijiji, kwa kuwa kuna vijiji vingi havijapimwa na kupewa hati ya kumiliki ardhi katika Wilaya ya Mpwapwa. Je ni lini Serikali itakamilisha zoezi

hilo na kuwapatia hati ambazo zitasaidia vijiji hivyo kupata mikopo ya kuendeleza vijiji hivyo.

Pili, Je ni lini Serikali itawapatia watendaji/wataalam katika Wizara hiyo vitendea kazi vya kisasa ili kutekeleza zoezi hilo.

Tatu, kwa kuwa miji mingi imejengwa bila kutumia *Master Plan* na kufanya nyumba kujengwa kiholela au bila mpango maalum. Je Serikali ina mpango gani wa kusaidia miji hiyo kupata *Master Plan?*

Nne, Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza wataalam wake waliopo Wilayani kwa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Tano, Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. FATIMA SAID ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchango; kwanza naipongeza Wizara kwa kukamilisha zoezi la utoaji wa ardhi na ubatilisho wa mmiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Mheshimiwa Waziri mbona mimi bado sijakabidhiwa hiyo *offer?* Ni zaidi ya miaka miwili (2) sasa nazungushwa na kiwanja changu cha Msasani - Butiama ambacho Maafisa Ardhi walikiri kukiuza na nikaahidiwa kulipwa kiwanja kingine Mikocheni A.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba msaada wako kwani Kamishna analifuatilia lakini limekuwa ni la muda mrefu. Wizara imeeleza (uk. 17) kwamba inaendelea kushughulikia maombi ya Viwanja Dar es Salaam. Maombi hayo ni kwa ajili ya maeneo ya uwekezaji na Balozi mbali mbali. Je, Viwanja kwa ajili ya Balozi si vilitolewa Dodoma, mji Mkuu wetu? Au Wizara imebadilisha maamuzi hayo? Balozi zetu zitajengwa Dar es Salaam badala ya Dodoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, naomba kupata maelekezo kuhusu ardhi na kuondoa umaskini kwa wanawake wa Tanzania.

**MHE. LEPHY GEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri wake na wataalam jinsi wanavyojitahidi kufanya kazi yao kwa makini na umahiri wa hali ya juu. Kwa sasa inaonekana kabisa kuwa kuna mabadiliko makubwa ya utendaji kazi katika ofisi ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu moja linahusu upimaji wa vijiji Tanzania Bara kimkoa, ni nini kilichoukabili mkoa wa Rukwa kuonekana kuwa hakuna vijiji mpaka sasa vilivyopimwa wala kutambuliwa. Kwanza katika Mkoa mzima, lakini vile vile katika mji wangu wa Mpanda kwa maana kwamba vijiji vilivyo katika jimbo langu la Mpanda kati havijapimwa wala kutambuliwa, lakini vipi na vinafanya kazi kwa hadhi hiyo kama vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maelezo kuhusu kijiji cha Ilembo, Nsemulwa, Kashaulili - Makanyagio, Shanwe, Kawajense - Kazima, Misunkumilo. Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Ardhi kama ifuatavyo: Awali nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri sana wanayofanya japo katika mazingira magumu sana. Matunda ya jitihada zao yameanza kuonekana. Sasa basi.

Kwanza, kwa vile, utaratibu wa kuanzisha mabaraza ya Ardhi katika vijiji vyote zaidi ya 10,000 utachukua muda na kwa kuwa mabaraza ya Ardhi ya sasa hayapokei tena kesi mpya, je Wizara kwa kushirikiana na Wizara zingine husika iko tayari kutoa mwongozo kamili wa namna ya kushughulikia kesi nyingi zilizokwama kutokana na hali hii ya kipindi cha mpito, hasa kwenye maeneo yenye mgogoro wa Ardhi kama ilivyo kwa maeneo mengi ya Mkoa wa Arusha na Manyara na hususan Wilaya ya Karatu.

Pili, Je, Wizara inaweza kutoa upendeleo maalum kwa kutoa fedha zaidi kwa Baraza la Rufaa la Ardhi ili kesi nyingi zilizoshindikana kushughulikiwa ziweze kumalizwa ili kuondoa kero nyingi kwa wananchi.

Tatu, naunga mkono kwa dhati kabisa, jitihada za Wizara kukarabati au kujenga upya jengo lenye mitambo ya kutengeneza Ramani. Kitengo hicho ndiyo uhai wa shughuli zote za ardhi, hivyo ninaomba mkakati maalum ufanyike kuwa na jengo, lakini pia kuimarisha mitambo, kitu ambacho kinategemewa na nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza maelezo yangu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara hii kwa jinsi walivyojitahidi kutekeleza majukumu yao vizuri kwa mwaka ulioishia Juni, 2004. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo ni kero kwa wananchi ambayo yangefaa Wizara ikayasimamia vizuri. Mfano:- uthamini wa ardhi na majengo kwa ajili ya kupata mikopo haukubaliki na Mabenki unapofanywa na wataalamu wa Wizara. Kwa nini wanapenda wathamini wao tu? Je hawana imani na watumishi wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mazao mbalimbali yanapofanywa bila kushirikisha wadau, mara nyingi huleta zigo. Kwa nini viwango hivyo visiwe

vinabadilishwa kila baada ya miaka miwili (2) au kila mara kutegemeana na hali ya uchumi na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, mfuko wa kupima viwanja bado haujatumika vizuri. Inaonekana unatumika kama mfuko usiotakiwa kurejesha fedha. Kwa nini fedha nyingi bado hazijarejeshwa Wizarani wakati watu wanapopimiwa, hulipa fedha taslimu? Ingefaa wahusika watoe taarifa za kuridhisha ni kwa nini hawajarejesha fedha hizo ambazo zinahitajika na miji mingi ikiwemo mji wa Sumbawanga.

Pia Mheshimiwa Spika, bado kasi ya kupima vijiji ni ndogo sana. Kwa nini katika hali hiyo tusianze na vijiji vinavyozunguka miji ya Wilaya ili kuvifanya vijiji hivyo visiwe chanzo cha *squatters.*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa kwa ujumla, ina sifa ya ujenzi wa nyumba nzuri za tofali za kuchoma. Kwa msingi huo, kwa nini Wizara isitumie nafasi hiyo ya kuwakopesha mabati peke yake ili Wizara ionyeshe mafanikio yake kwa Wilaya nzima kwa muda mfupi ili iwe kichocheo kwa Wilaya nyingine kujenga nyumba za tofali za kuchoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, hivi *master plan* ya Jiji la Dar es salaam hasa katika mabonde wa jangwani ambayo yalikuwa yawe ni *green belt* ya jiji kwa ajili ya uzalishaji wa mboga, kwa nini hilo limeshindikana? Nani alaumiwe kwa kushindwa utekelezaji wa maamuzi ya tangu zamani, Je ni kwa nini bado watu wanajenga karibu sana na ufuko wa bahari? Je ufuko wa bahari si mali ya wote?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ya *NHC* kujenga nyumba zaidi, bado ninashauri ujenzi wa nyumba uwe pia wa ghorofa za kupangisha kuliko kuendelea na ujenzi wa nyumba moja moja ambayo huhitaji eneo kubwa na hivyo kutumia ardhi kubwa kwa watu wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kuwapongeza kwa jinsi mnavyopambana na rushwa katika Wizara hii. Endeleeni kwa nguvu zote. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Gideon A. Cheyo kwa hotuba yake nzuri ambayo naiunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika kwa vile sasa Hazina imeiachia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ule mkopo wa T.Shs.1.8 bilioni kwa ajili ya viwanja vile 20,000 vya mkoa wa Dar es Salaam ili waendeleze maeneo mengine kuwapatia wananchi wa Dar es Salaam viwanja zaidi, je Wizara sasa iko tayari kupunguza bei ya viwanja hivyo kuliko bei ya sasa ambayo imeonyesha wananchi wengi hawana uwezo na gharama hiyo. Naomba Serikali ipunguze bei ya viwanja hivyo. Naomba pia Wizara ifanye hima kwa ushirikiano na *UN Habital* ili kuyafanyia kazi maeneo ya *squatter* ya Magomeni, *Kinondoni Quarters* ambazo hazifai kabisa kwa kuishi wananchi katika Tanzania ya leo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kufanikisha zoezi la upimaji wa vijiji katika Jimbo langu la Nanyumbu. Kulingana na orodha ilivyotolewa na Wizara karibu vijiji 50 vimepimwa hivyo kuonyesha kuwa vijiji vilivyobakia kuwa 20 tu. Naomba Serikali ikamilishe zoezi la upimaji wa vijiji vilivyobaki bila ya kuchelewa. Hali hiyo itapunguza katika kuleta migogoro ya Ardhi kati ya kijiji na kijiji na hata kati ya Wilaya na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na upimaji vijijini. Serikali itilie mkazo upimaji wa Miji midogo katika Jimbo la Nanyumbu. Vijiji vya Mangaka ambapo ni Makao Makuu ya Jimbo na Michiga ambavyo kila kimoja inakisiwa kuwa na wakazi zaidi ya 6000 hivi sasa ni bora vikapimwa kulingana na mahitaji ya miji midogo. Hii itapelekea kuwa na miji ya kisasa inayokua kulingana na mipango miji ya kisasa kinyume na huko nyuma ambapo miji iliachiwa kukua bila ya mipango yoyote hivyo kuwa na miji mibaya ambayo miundombinu yake isiyoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mangaka ni Makao Makuu ya Jimbo la Nanyumbu. Mji huo mdogo unakua kwa haraka sana. Hali ya ujenzi wa mji huo siyo nzuri kwa sababu hakuna mipango yoyote iliyoandaliwa hivyo mji hujengwa kiholela. Mji huo una Taasisi mbalimbali za Serikali na watu binafsi ambazo zinahitaji kupangwa vizuri. Hivyo ni muhimu Serikali ikahakikisha mpango ya kupima mji huo ikaharakishwa. Hali hiyo inahusu mji mdogo wa Michiga ambao nao una wakazi wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo inahitaji kupimwa ni eneo la Mtamba swala ambapo daraja la Umoja katika Mto Ruvuma limepangwa kujengwa. Kutokana na umuhimu wa eneo hilo kibiashara wananchi wengi wanajiandaa kwenda kujenga huko. Naomba Serikali ikaandae sehemu hiyo kabla ya uvamizi huo ili kuruhusu ujenzi wa Mji wa kisasa katika eneo la Mtamba swala.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuwasilisha mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Cheyo, Naibu wake Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu Ndugu Salome Sijaona, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara yao. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Kamati ya Bunge inayosimamia Wizara hii. Kwa hiyo naweza kujigamba kuwa naifahamu Wizara hii pamoja na viongozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya mfano wa kuigwa kwa sababu ya jinsi uongozi wake kuanzia ngazi ya Waziri hadi Mkurugenzi kuwa na mshikamano na umoja kama siafu katika kazi. Kwa sababu ya huu mshikamano wao wamefaulu maeneo mengi ya maendeleo katika Wizara yao kwa mfano kupiga vita rushwa, mpango endelevu na wa kisasa wa kusimamia ardhi na makazi, Mashirika yaliyo chini yake *NHC.* Kwa kweli mchango wangu wa kwanza ni kuwapongeza wote kwa uadilifu katika kazi na kuwaomba wadumishe sifa hii adimu!

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili unahusu upimaji wa mipaka ya vijiji, Kata na Wilaya uliofanyika katika Mikoa ya Manyara Arusha na Kilimanjaro. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uamuzi wake huu wa busara kwa mikoa iliyofanyiwa upimaji inaongoza kwa migogoro ya ardhi katika vijiji, Kata na Wilaya na baina ya makundi mbalimbali katika jamii ya wakulima wafugaji na wafanyabiashara. Kwa kweli kwa hatua hii sasa Wawakilishi wa wananchi tutatuliza vichwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa sasa ambalo litatukosesha utulivu kule katika Wilaya ya Same ni upimaji wa mji wa Same (mji wa Wilaya ya Same au Dar es Salaam ya watu wa Same) na mji mdogo wa Hedaru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya mwaka 2002 mji wa Same una wakazi wapatao 17000 na ule wa mji mdogo wa Hedaru watu 19500. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara kwa ujumla miji hii ifanyiwe upimaji katika muhula huu wa fedha 2004/2005, upimaji wa miji hii sio tu utaleta *impact* (msukumo mzuri) katika kazi ya upimaji wa mipaka uliofanyika bali pia utaijengea Wilaya ya Same mazingira mazuri ya kukua kiuchumi na Kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Same ni Wilaya Maskini sana katika mkoa wa Kilimajaro, hivyo haiwezi kuondokana na umaskini uliokuwepo sasa kama hatuipatii mazingira mazuri ya kuijengea mipango miji ambayo itakuwa chachu vitovu vya maendeleod ya Wilaya, miji yote miwili ya Same na Hedaru iko katika barabara kuu *(highway)* ya Dar es Salaam Arusha na inategemewa sana na Wilaya jirani ya Simanjiro umbali wa km 80 tu Wilaya ya Simanjiro inategemea miji hii kwa huduma za *bank,* usafiri, biashara masoko ya mifugo na mazao ya shambani. Naiomba Wizara ipime miji hii ili isikwame katika maendeleo ya Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu unahusu shamba la Katani lililoko Kijiji cha Makanya na linalomilikiwa na *Mohammed Enterprises (MOETL).* Kutokana na Sheria za ardhi shamba hilo linamilikiwa ardhi ya pande zote mbili mahali barabara kuu ya Dar es Salaam - Arusha inapopita hapo Makanya, Wananchi wamewekwa pembeni na mbali kabisa na barabara kuu ya Dar es Salaam - Arusha. Hali hii inawakwamisha katika maendeleo yao ya uchumi na Kijamii. Wananchi wako tayari kumwongezea au watoe fidia eneo lingine kuwa shamba la *MOETL* ili mmiliki huyu aachie eneo linalozunguka barabara kuu pale Makanya kwa makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Wizara iangalie ni vipi au kwa taratibu gani jambo hili linawezekana kisheria au kwa maelewamo wananchi wapate eneo hilo linalozunguka barabara kuu kwa makazi yao. Mheshimiwa Waziri hali ya wananchi kukosa eneo hili kwa makazi yao limewakwamisha sana wananchi wa Makanya katika maendeleo yao ya uchumi, sasa tunaomba kupatiwa uwezekano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa nne unahusu utaratibu endelevu wa mipaka ya vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa. Je Wizara ina mpango gani wa kubuni mipaka *(imaginary boundaries)* itakayotokana na kukua kwa vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa badala ya utaratibu wa hivi sasa wa kugawanyagawanya vijiji, Kata Wilaya na

mikoa kila mara haja inapotokea kutokana na kukua kwake? Je hali hii si inaiongezea Serikali gharama za kupima kila mara hali hii ya mabadiliko ya Kijamii, kiuchumi na kisasa yanapotokea. Utaratibu endelevu ni upi na ambao ungeweza kuiondolea Serikali yetu mzigo unaotokana na wananchi katika vijiji, Kata, Wilaya na Mikoa kutaka kugawanywagawanywa? Sheria ya ardhi inalionaje hili na wapi itatufikisha na hasara gani au matumizi gani Taifa inapata kutokana na hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine uhahusu upimaji wa hati mmiliki Wilayani. Katika Wilaya yangu ya Same gharama ziko juu mno kiasi kwamba wananchi hawana uwezo kuzilipa. Zinafikia kiwango cha 2.0 milioni mpaka 3.0 wakati anayepimiwa ardhi ni shamba lake au kiwanja cha kukimiliki kimila. Hata Bwana Ardhi akipokea malipo kutoka kwa wananchi anapokea malipo hayo siyo kwa stakabadhi za Serikali bali kwa uthibitisho wa maandishi yamkono.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ninao uthibitisho huo ambao wananchi wanaolalamika wameniletea katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 17 aya ya mwisho Wizara imeagiza Halmashauri ziajiri Maafisa Ardhi wenye sifa zinazostahili. Nina wasiwasi juu ya uwezo wa sifa wa Bwana Ardhi wa Wilaya ya Same. Nashauri iweze kusimamia kuwa taratibu na utaalamu wa mambo ya ardhi unazingatiwa na kila Halmashauri na Maafisa Ardhi wake.

Pia Wizara iweke viwango vya wananchi kulipia upimaji wa hati mmiliki za viwanja na mashamba zinazopimwa na wataalamu wa ardhi Wilayani. Hii ni kwa sababu maafisa hao huwachaji wananchi gharama za juu mno za kazi ya upimaji. Kiwanja kimoja kule katika Wilaya ya Same nimesema wamelipisha 2.5 milioni.

Je, wananchi wangapi wataweza kulipa malipo hayo ili kupata hati mmiliki? Nimesema ninao ushahidi ambao unathibitisha kuwa kuna mazingira ya rushwa na ulaghai katika zoezi zima la kupima ardhi. Kisingizio cha Afisa Ardhi huyu ni gharama za kazi hiyo, malipo ya utaalamu katika Ofisi yake Wilayani na Wizarani ninaomba kufahamu malipo hayo na viwango vyake na ni kwa nini wananchi walipie gharama za wataalamu walioajiriwa na kulipwa kwa kodi zao.

Naamini Wizara italiangalia hili na kuona ni vipi na kwa utaratibu upi wa taratibu na huduma za ardhi katika Halmashauri zote na Maafisa Ardhi wote nchini unakuwa wazi. Naamini nitapata majibu ambayo yatakidhi kero niliyoitaja hapa na hivyo kupata jibu la kumpatia mwananchi wangu aliyeniletea malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Ndugu yangu Cheyo, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na mshikamano wa kuongoza Wizara yao na kutumikia wananchi wetu. Namalizia kwa kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. PROF. P. P. MBAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Aidha naomba Waziri wa Ardhi na Makazi aidhinishe viwanja vyote

vilivyopimwa kwenye *site* ya Namtumbo. Hii itaongeza kasi ya wanaotaka kujenga kiangazi hiki cha Julai hadi Oktoba 2004.

Mhehimiwa Naibu Spika, vile vile tunaomba viwanja vyote vya kupimwa kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka zinazohusika kuanza kuweka majina kwenye *streets* husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuidhinisha ramani za majenzi kutapunguza kasi ya *slums* kuanza kujengwa. Kadhalika ni rahisi kutenga maeneo mapema ya kujenga Magereza, Polisi *(OCD)* Hospitali ya Wilaya, Mahakama ya Wilaya, Sekondari ya Serikali, Shule zaidi za Msingi, Soko la Wilaya, Ofisi ya CCM Wilaya, Posta, Simu ushirika, viwanda, Hoteli za Kitalii *(Selous Conservation Programme* ni jirani) mabanki ya maji, *TANESCO* na kadha wa kadha. Bustani za Burdani *recreation parks.*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naandika kuunga mkono hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kusisitiza juu ya tatizo la ujenzi holela katika miji hasa nyumba za gorofa zinazoleta sura mbaya katika jiji la Dar es Salaam maeneo ya Kariakoo. Vile vile ujenzi usio na mpangilio katika vijiji vinavyokuwa haraka katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Pili nawapongeza Wizara kutoa mchanganuo wa vijiui vilivyopimwa na ambavyo bado kupimwa katika nchi. Juhudi za kupima vijiji vilivyobaki ziendelee ili wananchi wajue mipaka halali ya vijiji vyao na kuondoa migogoro ya Ardhi inayoweza kutokea kwa kadri idadi ya watu inavyoongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo naomba nifanye masahihisho ya mpangilio wa vijiji katika jimbo langu la Korogwe Magharibi. *Column* ya Tarafa isomeke Kata.

**Kata ya:**

1. Bungu - Vijiji viko sawa.

2. Chekelei - Futa Kijiji cha mwisho yaani Mudumu;
   - Vilivyobaki viko sawa.

3. Dindira - Kijiji Msasa hakijapimwa;
   - Kijiji cha Mpaka kisomeke Mpake;
   - Vijiji vilivyobaki viko sawa.

4. Lutindi - Rekebisha vijiji vyake visomeke ifuatavyo
   - Lewa
   - Lutindi
   - Weki

- Masange
- Tanota
- Mashindei

5. Makuyuni - Masahihisho yafuatayo yafanywe:-
- Kijiji cha Mgombe kisomeke Mgobe
- Futa Kijiji cha Magila Mkumbate
- Vijiji vilivyobaki viko sawa.

6. Mazinde - Vijiji viko sawa.

7. Mkalamo: - Rekebisha vijiji vyake visomeke ifuatavyo:
Mkalamo, Magamba/Kaoshichonge, Makayo,
Changalikwa, Makole, Toronto, Mbugani,
Kweibewa, Pasilasi.

8. Mkomazi - Fanya masahihisho yafuatayo:-
- Futa Kijiji cha Makayo
- Nanyonge kisomeke Nanyogie

9. Mombo - Rekebisha vijiji vyake viwe vifuatavyo:-
- Mlembule, Jitengeni, Mambo mjini, Mwisho wa shamba.

10. Vugiri - Futa Kijiji cha Mgobe, vilivyobaki viko sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE: ABDULKARIM E. SHAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongezea na kutoa shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Gideon Cheyo, Naibu Waziri Mheshimiwa Hajjat Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kuandaa hotuba nzuri yenye muelekeo wa maendeleo ya wananchi wetu hasa kwa mpango huu wa upimaji viwanja na kuipa thamani ardhi yetu. Huu ni ukombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ziara yake aliyoifanya katika Wilaya ya Mafia kwa kuja kutuelekeza nini tufanye ili tufanikishe kupata ardhi iliyokuwa ni shamba la Mzungu ambalo tunategemea kuongeza kkupanua mji wetu mdogo wa Kilindoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa kuandika barua toka ofisini kwake na kwenda kwa Mkurugenzi amuhimize ili utaratibu wa kulipata sehemu ya shamba hilo ili tutoe nafasi kwa wananchi watakaohamishwa kutoka Bondeni kilindoni kwa ajili ya kutoa nafasi ya ujenzi wa bandari.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana sana Wilaya ya Mafia tupatiwe Afisa Ardhi Wilaya tena hilo ni muhimu sana. Hivi sasa hatuna.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba niseme naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Mungu awabariki wote.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Pili naelekeza mchango kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata/Nyumba: Naona lipo tatizo linalohitaji ufafanuzi kwani Mahakama hazipokei kesi zinazohusu ardhi na nyumba na wakati huo huo mabaraza usuluhishi wa Ardhi hayapokei au kufungua mashauri mapya tangu *October 2003* na hii imewafanya wananchi kutangatanga, tatizo hili nimeelezwa na Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Babati hivyo naomba ufafanuzi kama ndivyo ilivyo kwa sasa.

Pili, bado haijulikani ni nani atalipa posho za Wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya vijiji na Kata. Na kama ni Halmashauri ya Wilaya ni muhimu kujiuliza kuwa sasa Halmashauri ya Wilaya zinapata wapi fedha baada ya vyanzo vingi kufutwa?

Tatu, lipo tatizo la usafiri kwa Baraza la Ardhi na nyumba la Wilaya ya Babati. Pia hawana ofisi za uhakika kwa shughuli za Baraza na utaratibu wa posho zao unahitaji uangaliwe vizuri kwani wanafanya kazi ya kutoa haki kwa mashauri yanayohusu maisha na rasilimali za wananchi hivyo usitizamie kuwa mtu mwenye njaa atoe haki sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata maelezo ya kina kuhusu Kamati za kugawa ardhi Wilayani kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa nini utaratibu wa zamani umeondolewa wa Mkuu wa Wilaya kuwa Mwenyekiti.

Pili, ni vigezo gani sasa vimetumika kuamua kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya awe ndiye Mwenyekiti wa Kamati akiwa na Wajumbe ambao ni Wataalam tu.

Tatu, ni vema tukajua ni kwa nini Waheshimiwa Madiwani sasa hawapo kwenye Kamati hizo. Hii ni kasoro kubwa katika ugawaji wa ardhi na sasa hata haijachukua muda tumeona mianya mingi ya ukiukaji wa taratibu za kugawa ardhi hasa viwanja kwa kutokuhusisha wadau au wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba ni muhimu kabisa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya awe ndiye Mwenyekiti wa ugawaji wa ardhi na ni lazima kuwepo kwa Waheshimiwa Madiwani na baadhi ya Wakuu wa Idara ndipo unaweza kupata UWAZI NA haki wakati wa zoezi la ugawaji. Vinginevyo kutakuwa na migogoro mingi kati ya Mkurugenzi na Waheshimiwa Madiwani.

Nne, ugawaji wa viwanja ni muhimu uende sambasamba na ulipaji wa fidia. Hili ndilo tatizo kubwa kwa sababu Kamati za ugawaji zimekuwa zikitwaa ardhi kabla hata ya

kuwasiliana na wahusika. Ni muhimu kabisa kuwe na Kanuni zinazoeleweka kwa watu wote kuwa maeneo yao yatachukuliwa tu baada ya fidia kulipwa. Kwa sasa kinachofanyika Wilayani ni vurugu tupu na Serikali bado hauonyeshi kuona kama hiyo ndiyo kero ya kwanza kwa wananchi. Ni vizuri Wizara itoe maelezo ya kina ikiwa ni pamoja na adhabu kwa watendaji wanaokiuka maelekezo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pia Naibu Waziri na watendaji wote wa Waizara hii kwa mageuzi makubwa waliyoifanya kwa muda mfupi hasa 2002/2004 na kuijengea heshima Wizara hii iliyokuwa imejaa rushwa na utendaji wa ubabaishaji wa njoo kesho, njoo ksho.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za upimaji na utoaji hati hasa Makao Makuu ya Wizara unakwenda vizuri na kwa wakati. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri lazima afanye jitihada kuona kwamba Ofisi ;za Ardhi ndani ya Halmashari zinafanya kazi kwa msingi na nidhamu ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi nyingi za Ardhi ndani ya Halmashauri bado zimejaa wazembe, wababaishaji na bila shaka wala rushwa wa siri. Viwanja kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza vinatoalea kwa watu zaidi ya mmoja kwa kiwanja kimoja na kuzua migogoro na migongano kila siku. Migogoro ya viwanja Muheza imefikia hata bila kujali kuwagonganisha viongozi wa juu wa Serikali hadi ngazi ya Majaji.

Upimaji na ugawaji wa mashamba hasa eneo la Mlingano ni kero tupu hakuna usimamizi bora na kila mara eneo moja linatolewa kwa zaidi ya mtu mmoja, au kunyang'anywa eneo kila baada ya miezi mitatu. Hali kama hii inaharibu sifa za Wizara ya ardhi hasa yanapofumbiwa macho na Halmashauri yenyewe na hata Ofisi ya Mkuu wa Wilaya malalamiko yanapotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Wizara ya Ardhi itatekeleza wajibu wake kama ilivyoeleza katika sehemu (9)(x) Kuimarisha Ofisi za Sekta ya Ardhi katika Halmashauri? Hasa sasa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningeomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ifafanue juu ya utaratibu wa Halmashauri kupata fedha kutoka katika Mfuko wa *Plot Development Revolving Fund, (PDRF).* Inawezekana Halmashauri/Manispaa nyingine hazijui kuwepo kwa mfuko huo. Katika Jedwali 13 inaonyesha kwamba ni Halmashauri mbili za Ileje na Nkasi, na Manispaa ya Mbeya tu ndiyo zimerejesha sehemu ya mikopo ya fedha hizo? Je kuna ukiukwaji wa taratibu za marejesho au muda wa wakopaji wengine wa marejesho ulikuwa haujafika. Nia ni kuona mfuko huu unaendeshwa vizuri badala ya baadhi ya Halmashauri kuhodhi fedha za mfuko na kuzifumia kinyume na utaratibu.

Mwisho naomba Wizara ya Ardhi na Mandeleo ya Makazi iongeze jitihada kuifanya Serikali ikubali na hatimaye kupitisha utaratibu wa Kisheria utakaohusu

utekelezaji wa mazingira mazuri yatakayo mwezesha mwananchi mfanyabiashara na mfanyakazi kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba ili kuboresha makazi ya wananchi wa Tanzania ambao wanakabiliwa na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya viwanja vinavyopimwa maeneo ya Boko na sehemu nyingine Dar es Salaam na muda wanaopewa viwanja kutakiwa kulipia ni kikwazo kwa wananchi wenye uwezo mdogo na hasa kwa wale ambao walikutwa wakiishi katika maeneo yaliyopimwa. Tunaomba Mheshimiwa Spika gharama hizi ziangaliwe, vinginevyo viwanja vitabaki mikononi kwa wachache wenye uwezo ambao huvinunua kutoka kwa wale waliyopewa wasio na uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa ardhi na Maendeleo ya Makazi 2004/2005.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Cheyo Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Hajat Tatu Ntimizi, Katibu mkuu Ndugu Sijaona na kikosi chote cha watendaji kwenye Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanyika hapo Wizarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongea wote hawa kwenye maeneo yafuatayo:-

Kwanza binafsi mimefarijika sana kuona jinsi mradi wa upimaji viwanja 20000 jijini Dar es Salaam ulivyo kuanza kusimamiwa na kutekelezwa na Wizara hii. Inatia moyo kufahamu kwamba kinyume kabisa na imani ya wengi mradi huu ulibuniwa na wataalamu Wazalendo, ukatengenezewa *programme* ya *computer* na wataalam wetu na utekelezaji wake umesimamiwa kwa ufanisi ulizoaa mafanikio makubwa yanayostahili kupigiwa mfano katika utendajdi wa Serikali hii katika idara zake nyingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana Kamati yetu ilipotembelea mradi huu kwa hakika tulivutiwa sana na ujasiriamali uliodhihirishwa na Wizara hii katika zoezi hili, nashauri kama tulivyokwishasema huko nyuma, kwamba mwingine yenye matatizo ya dhahiri yanayofanana na yale ya Dar es Salaam. Ila kwa kuwa fedha zilizotumika kwenye zoezi hizi zilitolewa kama mkopo toka Hazina likubaliwe wazo la kufuta mkopo huu ili fedha zitumike kama *Revolving fund* kwa ajili ya shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile Wizara hii imekuwa ikishutumiwa kwa miaka juu ya tatizo la rushwa, utekelezaji wa mradi huu umekuwa kielelezo chema cha dhamira ya Uongozi wa Wizara kuepukana na kupambana kwa vitendo na tatizo sugu la rushwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wake unazingatia haki kwa walengwa na kuhuisha taratibu za utendaji katika uendeshaji wa shughuli. Watu wote wanaopata nafasi ya kupata maelezo na kushuhudia mambo yalivyoendeshwa kote Mbweni, Bunju, Kijichi na kadhalika, wanakubaliana na ukweli huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na kuwatakia kila la kheri wadumishe mwelekeo huu mwema.

**MHE. MOSSY S. MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu, kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Wizara hii kwa mashirikiano yao ya pamoja baina ya Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wao wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze mchango wangu katika Wizara hii kama inavyojieleza Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Wananchi walio wengi wa kipato cha chini wamepangisha katika nyumba zilizojengwa baada ya kupata uhuru hivyo uchache wa makazi hivi sasa unajionyesha baada ya ongezeko la watu wa ujenzi finyu unaoendelezwa, hivyo nashauri Wizara hii ishirikiane na Taasisi mbali mbali za ndani na nje katika ujenzi wa Majumba ya kisasa yenye kupunguza gharama za matumizi ya ardhi yaani yenye ghorofa ndefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha tulipata tetesi kuwapo kwa taasisi moja kutaka kujenga nyumba nyingi kwa mpango huu sijui Wizara imetoa changamoto gani kwa hilo, na kama kweli Taasisi hiyo ipo tayari kujenga nyumba hizo tunaomba urasimu usiwepo ili wananchi wa nchi yetu wanufaike na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue fursa hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo/Chakula ili waweze kubuni mpango maalum wa kupima maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya kilimo hii itasaidia sana kuhamasisha wananchi mbali mbali kuendeleza kilimo kwenye mashamba ya kati na makubwa na yenye hati zilizotayarishwa kwa ajili ya kupata mikopo kwa ajili ya uendelezaji wa mashamba hayo, hii itasaidia sana wasomi mbali mbali kuingia katika ajira binafsi hivyo Serikali itafaidika kwa upande wa kutoa ajira na pia kupatikana chakula cha uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina utamaduni wa watu wetu kutokuelewa kwa kina kuhusu upimaji wa maeneo yao na kupata hati miliki, hivyo naiomba Wizara hii itumie kitengo chake hiki kukitangaza kwa faida ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kidogo nitoe mchango wangu katika zoezi la ukataji na ugawaji viwanja katika sehemu mbali mbali.

Ardhi katika nchi yetu tunayo ya kutosha mimi binafsi siridhishwi na ufinyu wa mkato wa viwanja hasa vile vya bei ya kati, tuangalie mfano wao nyumba zinavyopendekeza kule Masaki hii inatokana na kutokufanya ubahili katika zoezi zima la mwaka (47) hivi iweje miaka hii ya kisayansi kubanana na wakati tunayo ardhi ya kutosha tunapaswa tujenge na baadaye tujitegemee ndani ya makazi yetu ya kumiliki vi-*project* vidogo vidogo hasa kwa kina mama na watoto wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara hii iwatumie vizuri wataalam wake na wanavyo vya ardhi kwa kuwapa muda kubuni miundo mbinu katika kupanga namna ya kuitumia ardhi tuliyowayo pamoja na makazi ya watu. Ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. STEPHEN MASABA KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa maandishi. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Theodos Kasapira, Kepteni mstaafu, wananchi wa Mkoa wa Morogoro kwa jumla lakini hasa hasa wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, kwa kifo cha Mbunge wao Marehemu Theodos Kasapira. Mungu aiweke roho ya Marehemu pema peponi amina.

Namshukuru sana Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Gideon Cheyo kwa hotuba yake ya Bajeti 2004/2005 ni nzuri na ya kimageuzi. Pia nimshukuru sana na kumshukuru Naibu ?Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Hajat Tatu Ntimizi kwa mshiriki wake kwenye maandalizi ya hotuba hii nzuri. Shukrani nyingi pia kwa Katibu Mkuu Salome Sijaona pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye hotuba hii ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu utaratibu wa kujenga nyumba za makazi wananchi wa Tanzania. Jukumu la utaratibu huu ni la Wizara ya Ardhi kwa namna kwamba wananchi sasa waachane na ujenzi wa nyumba kwa pesa taslimu. Uwepo mpango wa Mkopo kwa wananchi waweze kukopeshwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi. Kumbukumbu ya utaratibu huu inaendana na Benki ya Nyumba Tanzania. Kwa hiyo Shirika la Nyumba la Taifa liwe kiini cha mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naiomba Wizara kupitia kwako ziiombe Serikali iwe na kuendeleza mambo mazuri kwa faida ya wananchi wote. Mpango wa kupima viwanja hivyo matumizi mbali mbali ki-mipango miji kama ilivyofanyika kwa Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo pesa kiasi cha Shilingi 8.9 bilioni ambacho kilipewa/kukopeshwa kwa ajili ya kutekeleza mpango huu basi zisirudishwe Hazina bali zibaki Wizara ya Ardhi. Pesa hizi zitasaidia sana kuendeleza makazi kwenye miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo imani kwamba Waziri wa ardhi atakubaliana nami kwamba zinalo jukumu loa wazi kupima viwanja kwenye Jiji la Mwanza kama alivyofanya Dar es Salaam. Kwa hiyo, nasisitiza kwamba pesa hizo shilingi 8.9 bilioni zisirudishwe tena Hazina bali zibaki na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili iweze kutoa hii huduma kwenye miji yetu na kwa hali hiyo, Jiji la Mwanza sasa lipewe nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali yenye uzito huo huo, ni vizuri Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ikasimamia kwa karibu utendaji kazi kwenye

Halmashauri zetu za Wilaya. Pamoja na wito alioutoa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwenye hotuba yake kwamba ni vizuri Halmashauri za Wilaya ziweze sasa kutatua tatizo la wafanyakazi wasio na uwezo au kuhakikisha kwamba zinfapata watumishi wenye uwezo ili wajaze nafasi zote muhimu kwenye idara hii ili kuboresha utendaji lakini mimi naona kwamba Wizara isibaki nyuma kwenye ubora wa kazi hizo kwa kuzisimamia kwa karibu Halmashauri za Wilaya zote. Jambo hili ni la muhimu sana. Kuna malalamiko mengi ya wananchi kwenye Halmashauri zetu hizi. Malalamiko hayo hasa hasa kwa sehemu kubwa yanatokana na uwezo mdogo wa watumishi wa Ardhi na Upimaji kwenye Halmashauri nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili niwe wazi zaidi hili ndilo eneo ambako hisia za rushwa na pia ushawishi mkubwa wa kutoa rushwa unafanyika. Wakazi wa Jiji la Mwanza wanailalamikia Halmashauri ya Jiji sana kwamba watu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji ndiyo hasa walio na tabia ya kupenda rushwa sana. Kwa hiyo, usimamizi hapa utasaidia sana kupunguza au kutatua hili tatizo la rushwa kwa wananchi hawa. Baada ya kusema haya, ninayo imani kwamba Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi atanipa majibu kwenye hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikitishwa sana kuona kwamba katika hotuba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, hakuzungumzia mpango wa Serikali kusimamia uanzishwaji wa Mikopo ya Nyumba *(Housing Mortgage Scheme)* ili Watanzania walio wengi waweze kukopa na kujenga nyumba za makazi.

Katika hotuba ya mwaka 2003/2004, Waziri aligusia mpango uliokuwa unakamilishwa na Serikali wa Mikopo ya Nyumba *(National Housing Finance Programme)*. Inashangaza kwamba katika hotuba ya mwaka 2004/2005, Waziri hakugusia kabisa mpango huo umefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyombo vya fedha kutoa mikopo ya nyumba ni muhimu sana kuwezesha wananchi walio wengi na wasiokuwa na uwezo wa kuwekeza fedha za pato lao la kawaida kuweza kujenga nyumba, waweze kupata na kumiliki nyumba. Tanzania ni kati ya nchi chache sana (kama siyo nchi pekee) ambapo wananchi wake wanajenga nyumba kwa fedha zao tu bila mikopo ya aina hii, ukiacha watumishi wachache wa Serikali wanaopata mikopo chini ya mpango wa Mikopo ya Nyuma Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mabenki na vyombo vingine vya fedha, wanashindwa kuanzisha mikopo hii kutokana na Serikali kutoweka mazingira, utaratibu na *regulatory framework* kuwahamasisha wawekezaji na mabenki katika kuanzisha mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kwamba kutogusiwa suala hili katika Bajeti, haina maana Serikali imetupilia mbali mpango huu. Naomba sana Wizara iendelee kukamilisha *National Housing Finance Programme.*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kamati ya Ugawaji wa Ardhi. Kamati hii haifahamiki kwa wengi inavyoundwa na inavyofanya kazi. Kidogo linalofahamika ni kwamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Ugawaji Ardhi Wilayani, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli *DED* ndiye Mwenyekiti, mimi nashauri *DED* asiwe Mwenyekiti kwa sababu zifuatazo:-

(i) *DED* ni mtumishi ambaye anaweza kuhamishwa siku yoyote na anaweza kuvuruga ugawaji wa ardhi, kwani anajua wananchi hawatafanya lolote.

(ii) *DED* anaweza kujigawia ardhi na kujihalalishia kwa njia haramu. Mfano, *DED* wa Simanjiro, *Mrs.* L. Ngiloriti, amejimegea ardhi yeye mwenyewe na baadhi ya rafiki zake na amemtishia Afisa Mtendaji wa Kijiji aitishe kikao na Serikali ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji iwapitishie mashamba hayo. Vinginevyo huyo Afisa Mtendaji wa Kijiji atafukuzwa kazi. Serikali ya Kijiji imekataa kuidhinisha mashamba hayo na sasa *DED* anataka kitongoji hicho kiwe kijiji ili ahalalishiwe mashamba. Haya ni matumizi mabaya ya madaraka.

(iii) Siyo itifaki sahihi *DED* kuwa Mwenyekiti wa kikao chochote ambacho Madiwani ni Wajumbe.

(iv) *DED* atapendekeza majina ya watu ambao anajua atawaburuza.

(v) Kamati ya Ugawaji wa Ardhi iwe na wachaguliwa zaidi, kwani ndiyo wanaowajibika zaidi moja kwa moja kwa wapiga kura wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya awe Mwenyekiti wa Kamati ya Ugawaji wa Ardhi ya Wilaya. Wajumbe wa Kamati ya Ugawaji wa Ardhi, wateuliwe na Baraza la Madiwani na kuthibitishwa na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ianzishe haraka Mahakama ya ardhi ngazi ya Kata na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa siyo la Mijini peke yake ila na hata Makao Makuu ya Wilaya ya Vijiji. Najua Shirika hili halina uwezo wa kujenga nyumba kila kijiji, lakini naamini linaweza kujenga nyumba Makao Makuu ya Wilaya hasa Wilaya mpya, hususan Wilaya ya Simanjiro. Nyumba za Shirika zikijengwa Wilaya

ya Simanjiro, zitawasaidia sana watumishi wanaohamishiwa huko na Serikali. Kwa hiyo, nijulishwe mpango wa Shirika la Nyumba la Taifa kujenga nyumba Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro, Orkesumet.

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri ya Bajeti ya Wizara. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu mwaka 2000, kwenye Mkutano wa Kampeni *Usa River,* Mheshimiwa Rais alitoa dira *(vision)* yake ya kuwa na mazingira ya kumwezesha kila Mtanzania kuwa na nyumba bora. Juhudi za Wizara kutekeleza dira hii imeelezwa kidogo ukurasa wa 42 hadi 43 wa hotuba. Lakini jitihada hizi zimeishia na uandalizi wa sera ya maendeleo ya makazi ambayo inasimamia uendelezaji wa makazi nchini. Hatua ya kuwa na sera ni muhimu na inafaa kupongezwa. Lakini naomba nikiri sijaiona hiyo sera na huenda kuna wengine kama mimi hawajaiona hiyo sera. Je, hiyo sera inatekelezwaje na hasa kwenye maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *mortgage finance* lilishia wapi baada ya Benki ya Nyumba *(THB)* kufa? Bila *long term property investment finance infrastructure* kwa mfano, *Housing Development Bank,* maendeleo ya makazi nchini yataishia kwenye makabrasha ya sera tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu nianze kuchangia Wizara hii mwaka 2001, nimekuwa nikiomba Mheshimiwa Waziri atutembelee akaone matatizo ya mpaka kwenye Tarafa ya King'ori na hasa vijiji vya mpakani kati ya Arumeru Mashariki na Hai. Wakati fulani Waziri aliahidi (kufuatia swali Bungeni) kwamba angetuma wataalam wake kufanya *survey.* Mpaka leo hakuna Ofisa wa Wizara aliyetumwa. Matatizo na kero zimezidi kushamiri pamoja na jitihada za viongozi wa Wilaya na Mkoa husika. Je, wakati huu Waziri atatoa kauli gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga miono hoja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kuleta mafanikio makubwa sana kwenye nyanja ya ardhi hasa katika mwaka 2003/2004. Aidha, napenda kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, ningeomba yafuatayo yaangaliwe. Maeneo ya makazi vijijini, yapimwe haraka. Ningeomba zoezi la kupima maeneo ya makazi vijijini, lianze haraka iwezekanavyo na hatimiliki zitolewe kwa wanavijiji ili nao waweze kunufaika kwa kujipatia mikopo baada ya kuweka ardhi rehani kwa vyombo vya fedha. Aidha, isisitizwe kwamba zoezi hili lifanyike bila rushwa na urasimu, ambavyo vilikuwa vimeigubika Wizara hii siku za nyuma. Pia kusambaza elimu kuhusu vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi na hasa wale wa vijijini, wanastahili kupewa elimu kuhusu matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu vifaa vya ujenzi vyenye gharama nafuu ili waweze kuboresha makazi yao. Aidha, Serikali iondoe kodi zote kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi wengi waweze kujijengea makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Usajili ziwe Makao Makuu ya kila Mkoa. Hivi sasa ziko ofisi chache sana nchini za usajili wa ardhi kiasi kwamba inawagharimu wananchi kiasi kikubwa cha fedha. Kwa mfano, mtu wa Kasulu anatakiwa aende Mwanza kushughulikia usajili. Ningeshauri uangaliwe uwezekano wa kufungua Ofisi za Usajili kila Makao Makuu ya Mkoa, badala ya kuwa na Ofisi za Kanda *(Zone)* kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka za Ardhi ziwe kwa lugha ya Kiswahili. Nashauri nyaraka nyingi za ardhi, kwa mfano hatimiliki na *offer,* ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kahama na mimi mwenyewe, natoa rambirambi kwa familia ya Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Kepteni Theodos James Kasapira, ambaye ametuacha na kutangulia mbele ya haki, tarehe 21 Julai, 2004. Wakati huu wa majonzi mazito, nawapa pole familia ya Marehemu na wananchi wote wa Jimbo la Ulanga Mashariki kwa msiba huu mkubwa. Tumwombe Mwenyezi Mungu, aliye asili ya mema yote, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Naibu wake, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu, Mama Salome Sijaona, viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya. Hotuba ya Waziri ni ya matumaini makubwa katika kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta hii ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kuja na mkakati wa kugeuza ardhi kutoa mtaji mfu na kuwa mtaji hai. Kwa Wilaya kama ya Kahama ambayo ina ardhi nzuri, lakini ni Wilaya yenye wakazi wengi na kasi kubwa sana ya ongezeko la idadi ya watu. Mkakati huu utawawezesha wananchi kuwa na raslimali ambayo itawasaidia katika harakati za kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la ongezeko kubwa la watu mijini, ni matumaini yangu kwamba mikakati iliyoandaliwa na Wizara itawawezesha kufanikisha upatikanaji wa viwanja kwa wakati na kukidhi mahitaji ya waombaji mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ombi rasmi kwa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mji wa Kahama ni mmoja ya miji 7 hadi 8 ambayo imeainishwa na TAMISEMI kuwa Miji Midogo *(Townships).* Mji wa Kahama upo mbioni kukamilisha azma ya kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo mwaka huu. Namwomba Mheshimiwa Gideon

Cheyo, awezeshe uhakiki wa mipaka ya Mji na mpango wa maendeleo ya Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kahama unakabiliwa na tatizo la ongezeko kubwa la watu na kasi ya ongezeko hilo inazidi uwezo wa wataalam waliopo kupima viwanja vya makazi. Vile vile Mji wa Kahama, pengine kutokana na msongamano wa watu mjini, umekosa fursa za kuandaa Mpangomji yakinifu. Kwa hiyo, kama kweli mji huu utakuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, ni dhahiri kabisa kwamba sambamba na kuhakiki mipaka ya mji, utahitaji kuwa na Mpango Mji mahsusi wenye matumizi ya ardhi bayana na wenye mwelekeo wa Mji wa Kahama kuwa Halmashauri ya Mji katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa 2004/2005.

**MHE. PHILIP A. MAGANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyingine tena, kumpongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na wasaidizi wake wote, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii katika kuondoa kero za wananchi, zitokanazo na maswali ya ardhi na katika kuboresha makazi hususan mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafanya kazi nzuri katika upimaji wa viwanja mijini, pamoja na kusanifu mipango miji ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na miji ya kisasa inayokidhi mahitaji ya kisasa ya sayansi na teknolojia. Hapa kuna kero ambazo zinatokana na wafanyakazi wachache ambao katika utekelezaji wa mipango miji, hawawi makini na mara nyingi kufanya mabadiliko bila kupata kibali cha Wizara. Hili linatokana au kwa uzembe au kiburi tu cha watendaji wa Halmashauri za Miji, pengine kwa kushirikiana na baadhi ya Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano ni mingi ya jinsi gani mipango miji mizuri ilivyoigharimu Serikali fedha nyingi, imeharibiwa na kuyafanya makazi mapya, hayo yachukue sura ya ujenzi holela yaani *slums.* Mfano mzuri ni *Mbezi Beach.* Natoa rai kuwa utenganishaji wa maana ya makazi na maeneo ya biashara, yazingatiwe ili kuepuka kero na athari zinazotokana na mchanganyiko wa makazi na viwanda. Wanaohusika na ukiukwaji wa mipango hiyo, wachukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya makazi hususan katika Jiji la Dar es Salaam, hayana miundombinu ya kuondoa maji machafu pale ambapo baadhi ya wenye majumba humwaga au hupeleka maji barabarani na kwenye nyumba za jirani. Huu ni uvunjaji wa kanuni za afya ambazo zina umuhimu wa pekee katika miji wanakoishi watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuwa matatizo yote haya yanatokana pengine kwa utengano wa majukumu baina ya Wizara za Serikali na Taasisi mbalimbali. Mfano, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Ili kuboresha kazi za

maendeleo ya makazi na matumizi bora ya ardhi, nashauri mahusiano na madaraka ya Taasisi na Wizara za Serikali, yafanyiwe mapitio ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujengaji wa *condominiums* au maghorofa katika *prime areas* kama unaendelea katika maeneo ya *Oysterbay* na Masaki, yasitishwe mara moja. Pamoja na kuharibu mandhari ya maeneo hayo ambayo yalikuwa sehemu za kujivunia, inasababisha matatizo makubwa katika utumiaji wa miundombinu kwa mfano, umeme, maji na kadhalika.

Miundombinu hiyo ilijengwa kukidhi mahitaji ya watu wachache *(lowdensity)* na siyo msongamano unaotokana na kubadilisha maeneo yawe makazi ya *high density.* Napendekeza jambo hili lishughulikiwe mara moja ili tusiendelee kuharibu miji yetu ambayo ilisanifiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii ili niweze kuwapongeza Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri wanayoifanya. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hotuba hii. Baada ya kuunga mkono hoja, sasa ninayo machache ya kusema.

Mhershimiwa Naibu Spika, miaka michache iliyopita Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ilikuwa inalaumiwa sana kuwa imejaa rushwa, lakini sasa hali ya Wizara hii imebadilika kabisa. Wizara hii ni moja ya Wizara chache sana hapa nchini ambayo imepiga vita rushwa kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kupiga vita rushwa hadi kuitokomeza kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atupatie Mtaalam wa Ardhi katika Wilaya ya Serengeti. Kwa miaka mingi, Wilaya yetu ya Serengeti imekaa bila Mtaalam wa Ardhi na hii imesababisha viwanja visipimwe na hivyo kuleta kero sana kwa watu wanaotaka kujenga.

Tunamwomba Waziri aiombe *NHC* kujenga nyumba za bei nafuu Mjini Mugumu, Wilayani Serengeti, ili kuwaondolea kero ya ukosefu wa nyumba kwa wananchi wanaoishi Mji wa Mugumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kusema tena kuwa naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kutoa pole kwako, Bunge, wapiga kura wa Ulanga Mashariki na familia ya Marehemu, kwa kifo cha ghafla cha Marehemu Mheshimiwa Kepteni Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ningependa kutoa rai zifuatazo juu hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa viwanja 20,000 katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara imefanya kazi nzuri sana katika kupima viwanja hivyo, lakini yako matatizo yaliyojitokeza. Bado miundombinu haijakamilika hasa barabara na maji. Pale ambapo barabara zimechongwa, imekuwa shida kufikisha vifaa vya ujenzi viwanjani kwa kuwa wakandarasi wamechimba mifereji mikubwa sana ya maji ya mvua katika njia nzima, bila kuweka makalvati ya kuvukia. Ni wazi shida hizi za miundombinu zitasababisha kushindwa kwa wamiliki wa viwanja hivyo kumaliza ujenzi katika muda uliopangwa. Naomba tatizo hili liangaliwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia nzuri ya kuwa na viwanda hivyo, upanuzi wa Jiji umekwenda kwa kasi kubwa mno. *Horizonal expansion* imesababisha ujenzi wa kilometa nyingi za barabara, mabomba ya maji safi na maji taka na usambazaji wa umeme. Pia sehemu za huduma za jamii zinasambazwa eneo kubwa mno. Wakati umefika sasa tufikirie kupanua Jiji kwenda juu *(vertical expansion),* ili kupunguza gharama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji wa vijiji. Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri iliyofanyika na naitakia heri katika kuendeleza kazi hii. Katika kiambatisho "G" cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa kwanza, imeonyeshwa wazi kuwa katika Jiji la Dar es Salaam, hata hivyo, kuna makundi ya watu wanaojiita Serikali ya Kijiji hasa maeneo ya Kibamba, wanaochukua ardhi ya watu na kuiuza kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko rasmi juu ya uhalali wa vitendo hivi ambavyo vinahatarisha amani. Tamko lake litasaidia kuwaelimisha wakazi wa Dar es Salaam juu ya nani mwenye madaraka ya kutwaa ardhi Jijini Dar es Salaam, haki ya yule anayeuziwa ardhi na wanaojiita Serikali za Vijiji Jijini Dar es Salaam. Nina imani kuwa hili liko katika uwezo wa Mheshimiwa Waziri, hasa ikizingatiwa uadilifu wake na ari yake ya kutatua migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno hayo machache, naomba kutamka kuwa naiunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana viongozi wote wa Wizara hii na naunga mkono hoja ya Wizara kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri ufuatao kwamba pamoja na kuipongeza sana Wizara kwa jitihada za kupambana na *squatters* katika miji yetu mikubwa kwa kupima mapema maeneo yanayozunguka miji mikubwa, nawapongeza sana. Naomba Wizara itafute njia ya kuondoa *squatters* za Manzese na maeneo mengi ya Dar es Salaam na Mji wa Mwanza, kwa kukopa fedha *UNDP* au *HABITAT,* ili kurekebisha kasoro hizi kwa usalama, maana hivi sasa ukitokea moto, maeneo ya *squatters* yatakuwa hakuna namna ya kuuzima moto huo. Naomba Wizara ieleze namna gani inajitahidi kuondoa *squatters* katika Mji wa Mwanza na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kushauri kuwa nyumba zinazojengwa mijini kwa hivi sasa hazifuati sheria. Maana wanaotengeneza na kuuza matofali hawayafyatui vilivyo na kupunguza *size* ya matofali. *Standard size* ni *6"x9"x18"* kwa kuta za nje. Sasa hivi nyumba nyingi mijini zinajengwa kwa matofali hata ya *4"x5"x18",* ama hata ndogo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Engineers* wa miji, naona nyumba nyingi hawazikagui vilivyo. *Engineers* wengi hawana *inspection hammers* za ku-*test* ubora wa matofali. Katika miji mikubwa, *Engineers* ni wachache na hawatoshi. Kama kwa bahati mbaya linatokea tetemeko, nyumba hizi za ubora hafifu zinaweza kuwa kama mabomu kwa kuangamiza wakazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maghorofa yanayojengwa katika Jiji la Dar es Salaam, usimamizi ni hafifu hasa eneo la Kariakoo. Unaweza kukuta nyumba ya ghorofa 10, lakini haina ghorofa inayoenda chini ili kuzuia kuanguka kama kuna tetemeko. Ni vyema Wizara ikaweka *limit* ya ghorofa kwenda juu kwa maeneo ya miji mingi. Naomba *Engineers* kama wa Jiji la Dar es Salaam na miji inayojengeka sana, kuwa wa kutosha. Sehemu nyingi unaweza kuwaona *Engineers* wachache na uwezo wa usimamizi na upungufu wa vitendea kazi kwa watu hawa pamoja na kuboresha mapato yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia Wizara hii utekelezaji wa malengo mema mliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2004/2004.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Naibu Waziri wake, watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kusimamia majukumu yao vizuri ndani ya Wizara hii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu kwa baadhi ya maeneo yaliyomo katika hotuba hii, nachukua fursa hii kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki, ambaye amefariki akiwa hapa Bungeni, Dodoma akihudhuria

Kikao cha Bunge la Bajeti la mwaka 2004/2005. Pia natoa rambirambi kwa wapiga kura wa Jimbo la Ulanga Mashariki pamoja na wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kutoa mchango wangu, napenda kukiri kuwa Wizara hii ni moja ya Wizara muhimu sana katika maendeleo ya wananchi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyoelewa kuwa binadamu pamoja na shughuli zake mbalimbali za kila siku, analazimika kupata makazi ambayo yatamwezesha kuishi na kupanga mambo yake ya kila siku ya kimaisha na kimaendeleo yake binafsi na Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, ni imani yangu kuwa Wizara na Serikali kwa ujumla italiona hili na kulisaidia hasa kwa upande wa wananchi wetu ambao ni maskini kwa kipato, ili na wao waweze kumiliki ardhi na maeneo ya makazi yao na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 15, tunaelezwa kuwa mwelekeo wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, unatoa kipaumbele kwa maeneo makuu matatu ambayo yanaweza kuwa kichocheo kikuu cha kuwaletea Watanzania maendeleo. Maeneo hayo matatu ni:-

(i) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

(ii) Kuwawezesha wananchi kutumia raslimali ya ardhi ili kuwaondolea wananchi umaskini.

(iii) Kuimarisha utawala bora katika Sekta ya Ardhi, sambamba na kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi sana kwa Wizara hii kwa kuyaona na kuyatamka maeneo haya matatu ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla, kuweza kufanikiwa yale ambayo yatachochea maendeleo makubwa ya wananchi hapa nchini. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kulisimamia vizuri eneo hili ambalo kwa kweli tunaweza kufanikisha lengo letu la kuipeleka nchi yetu katika maendeleo ya kweli

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la migogoro ya ardhi na ugawaji wa ardhi kwa Watanzania, liwe ni *agenda* ya kwanza kabisa ili kuwapatia uwezo wananchi wa nchi hii. Tuwe waangalifu sana katika ugawaji wa ardhi yetu kwa wageni kutoka nje. Pia suala la wageni kumiliki maeneo ya mashamba makubwa ambayo yanawaathiri wananchi, kutumia vyanzo vya maji vilivyopo pamona na mashamba hayo ya wageni au wakulima wakubwa na wanaotoka nje ya nchi yetu yaangaliwe sana na baadaye yashughulikiwe vizuri ili wananchi waweze kutumia vyanzo hivyo kwa faida na maendeleo yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa huo huo wa 15, tunaelezwa kuwa Wizara imejiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi 5,896,650,000/=. Naipongeza

sana Wizara kwa kujiwekea malengo hayo, lakini pia nichukue fursa hii kuiomba Wizara hii kwamba makusanyo haya yakusanywe na yatumike vizuri.

Mheshimiwa Spika, ukurasa huo huo wa 15, unaelezea juu ya Huduma za Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea kutoa huduma za Maendeleo ya Ardhi zenye misingi na lengo la kuimarisha utawala bora ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kazi hii ya Wizara iliyoifanya ya kutoa huduma za Maendeleo ya Ardhi zenye msingi na lengo la kuimarisha utawala bora kwa mwaka 2003/2004 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini, kwa kweli naipongeza sana Wizara kwa kutoa huduma hiyo na pia niiombe kuangalia kasoro zilizojitokeza ili katika mwaka huu wa 2004/2005, Wizara ifanye vizuri zaidi kuwapatia wananchi maendeleo mazuri na ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa salaam za rambirambi kwako wewe binafsi na kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Kepteni Theodos Kasapira. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kumpongeza Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri hasa ya upimaji wa viwanja pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atueleze ni lini mikoa ambayo vijiji vyake havijapimwa kama vile Rukwa, Kigoma na kadhalika, vitapimwa ili wananchi wa vijiji hivyo waweze kujipatia hati zitakazowawezesha kupata mikopo na hivyo kuondokana na umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuelezwa iwapo Halmashauri za Mkoa wa Kigoma zilikwishapewa mikopo kutoka mfuko maalum wa kupima viwanja. Hii itatusaidia kufuatilia na kujua ni kwa nini vijiji vingi havijapimwa. Kama Halmashauri zetu hazijapewa mikopo, tunaomba zifikiriwe, ikitiliwa maanani kwamba ardhi yetu inavamiwa na wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kwa hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa kina ambayo ameitoa asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika,kipekee naipongeza Wizara hii kwa programu yake ya kupima viwanja katika Jiji la Dar es Salaam na baadaye kwa miji mikubwa kama ya

Mwanza na Arusha, jambo ambalo limewawezesha wananchi wengi kumiliki ardhi na hivyo kuwa na makazi ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naiomba Serikali, hususan Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, ihakikishe kuwa katika kumilikisha ardhi, wananchi wenye kipato kidogo wanapewa kipaumbele. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, nafanya hivyo hasa kwa sababu nimeridhishwa na hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na Serikali katika kutatua matatizo yanayotokana na umilikaji wa ardhi usio wa haki na usawa. Kushirikisha wananchi katika mazungumzo yahusuyo ugawaji wa ardhi hasa kuptia viongozi wao, kumesaidia sana katika kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunasubiri kwa hamu sana suala la ubinafsishaji wa mashamba ya umma ya *West Kilimanjaro,* kwa mfano *NAFCO* na *NARCO,* ili watu wetu nao waweze kupata makazi ya kudumu. Natambua kuwa suala hili linahusu Wizara nyingi na vyombo mbalimbali kama *PSRC,* lakini tunaamini Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, itasaidia kuweka fikra sahihi ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena narudia kuunga mkono hoja hii.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya, ikiwa ni pamoja na hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukosekana kwa ramani ya nchi nzima ya matumizi ya ardhi, ardhi nzuri kwa kilimo inatumiwa vibaya kwa kujaza majengo ndani ya mabonde na mbuga nzuri. Vipi kusiwepo mwongozo wa kuelekeza kuwa majengo yajengwe katika maeneo yenye ardhi mbaya na milimani (yenye mawe, mchanga, kokoto na kadhalika). Madhara haya yanaongeza umaskini katika nchi, kwa vile ardhi nzuri kwa kilimo inamezwa na majengo (makazi), huenda wakati umefika wa Wizara kuunda Kamati ya kukagua matumizi kila mwaka. Suala hili ni muhimu kwa hali na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kuzingatia ni aina ya majengo yanayojengwa katika miji yetu. Kwa sababu ya umaskini, wakazi wengi wa mijini wanapendelea kujenga nyumba fupi *(bungalow)* na hivyo kusababisha miji yetu kupanuka kupata kiasi na kumeza ardhi ya kilimo. Mfano mzuri katika suala hili, ni ujenzi wa nyumba za Serikali Mbweni, Bunju *(NHC),* Kisasa hapa Dodoma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujenge maghorofa chini ya *NHC.* Kwa nini tunajenga *barracks* katika karne hii? Kwa nini tusiwe na miji katika nchi hii? Vipi tusijenge nyumba zenye bustani na kufanya miji yetu kuwa *architectural gardens* na kuzuia mji wetu kuwa *concrete (jungle) towns?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Gideon Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi, wataalam mbalimbali na taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pongezi hizi ni za dhati kabisa, nikiwa miongoni mwa wanakamati wa Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa michango yangu na ushauri wangu mwingi nilitoa wakati wa Kamati, nimepata majibu na ahadi mbalimbali. Nimeonelea sina sababu ya kurudia kuyachangia tena, ila naomba kusisitiza majibu niliyopata, naomba sana yatekelezwe kwa vitendo badala ya kuwa kwenye makaratasi tu bila kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo amabyo ni kero na sugu kwenye Jimbo langu la Korogwe Mashariki Wilaya ya Korogwe na Mkoani Tanga kwa ujumla ni mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa hasa ya *Katani Ltd.* kugawiwa wananchi ambao wana shida kubwa sana ya ardhi ya kilimo na makazi. Naomba sana kero sugu ya Kata ya Kwagunda katika Vijiji vya Mngaza, Mkokola, Maguna Cheke, Kwagunda, *Gereza East,* Mkwakwani, Kwemzindawa na Mnyuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa wanashida kubwa sana ya ardhi, kero yao ni ya muda mrefu sana. Ardhi imekuwepo toka *PSRC* kwa muda mrefu lakini hadi leo ni kero hiyo haijaisha. Bila ardhi hakuna maendeleo yoyote na hii inamaanisha maeneo hayo yataendelea kuwa na umaskini wa kutupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero hii ni ya muda mrefu, naomba Wizara isaidie kulikamilisha hasa kwa kuzingatia tamko la Mheshimiwa Rais kwamba mashamba makubwa yaliyokodishwa na hayaendelezwi wakabidhiwe wananchi. Sasa kwa nini swala hili lifanikiwe Mkoani Arusha na lisifanikiwe Mkoani Tanga? Naomba jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shamba la Chavda la Hale Mwakinyumbi, Korogwe. Naipongeza sana Serikali kwa kuwapatia wananchi wa Hale shamba la Chavda la Hale Mwakinyumbi. Aidha, tunampongeza Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, kwa kukabidhi shamba hilo rasmi kwa Serikali ya Mkoa wa Tanga kwa maana Halmashauri ya Korogwe kukabidhiwa shamba hilo na kulipangia utaratibu wa matumizi kwa kuzingatia maombi ya muda mrefu ya Mji wa Hale ambao unakua kwa kasi na hauna eneo la makazi na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka tupatiwe shamba hilo na Waziri wa Kilimo na Chakula, Halmashauri imeshindwa (hasa Idara ya Ardhi), kwa kisingizio kwamba hawawezi kufanya hivyo kwa sababu hawajapata kibali toka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi tu toka Serikalini. Hata hivyo, imeleta manung'uniko mengi

miongoni mwa wananchi wa Hale kucheleweshewa ujenzi wa makazi na kilimo, hasa wakijua kwamba Mheshimiwa Waziri Keenja tayari ametoa kibali cha ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilijitahidi sana kumwomba Waziri Mheshimiwa Charles Keenja, atupatie kibali cha Serikali. Mheshimiwa Charles Keenja alifanya hivyo. *CRDB* ambao ndio wamiliki wa shamba hilo la Chavda, walikubali kutoa shamba hilo. Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja ndipo alipomjulisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga kulitumia shamba hilo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili sasa kazi hiyo ifanyike ya kuwagawia wananchi wa Hale, naomba Wizara itoe maelekezo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe (Ardhi) wapime ardhi hiyo ili wananchi wapatiwe kwa utaratibu ambao utaondoa kero hiyo kubwa ya Hale. Mheshimiwa Waziri, shamba la Chavda Hale Mwakinyumbi ni pori tupu, hamna kabisa Mkonge. Nimeliomba shamba hili zaidi ya miaka tisa sasa, ndiyo juzi tu tumelipata. Naomba kauli yako kwa suala hili nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanja cha Mtaa wa Majengo - Korogwe Mjini, kilichopangwa kujenga *Nursery School* na badala yake kupewa mtu binafsi na kujenga nyumba ya kuishi. Lipo tatizo la ajabu ambalo limefanywa na Watendaji wa Idara yako ya Ardhi Korogwe, kwa kumpatia mtu binafsi eneo lililotengwa kwa Shule ya Awali na mtu huyo kujenga nyumba yake. Suala hili ni baya sana, limeleteleza akinamama wa eneo la Majengo Korogwe kufanya maandamano kwenda kwa Mkuu wa Wilaya. Katika suala hili, ipo dhana iliyojengeka kwa wananchi kwamba labda kuna tatizo la rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara watusaidie kuhakikisha matumizi ya awali ya ujenzi wa Shule ya Awali, yaendelee. Inavyoelekea uongozi wa Wilaya umeshindwa kutatua mgogoro huu. Nasikitika kueleza kwamba kwa hali ilivyo sasa, mgogoro huo kwa eneo la Majengo Mjini Korogwe, umekuwa wa kisiasa.

Kuhusu ununuzi wa nyumba za *NHC* Dodoma, yupo Ndugu Samwel J. Kapande wa Nyumba Na. 137 1A BK 16 amenunua nyumba hiyo. Amelipa sehemu ya malipo ya shilingi 1,688,000/=. Ameomba aongezewe muda hadi mwaka 2005 ili aweze kumaliza deni lake. Lakini jibu alilojibiwa ni kupewa *notice* ya kuondoka kwenye nyumba hiyo. Nashauri kwamba kwa kuzingatia umaskini wa mtu huyo na juhudi alizofanya za kupunguza deni hilo, aidha, juhudi kubwa za kikao chako na wadau hawa kwamba waeleze matatizo yao binafsi. Mtu huyu, maombi yake yafikiriwe. Naomba majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hotuba hii muhimu kwa asilimia mia moja.

**MHE. DR. IBRAHIM S. R. MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na kumpongeza yeye mwenyewe, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake na watumishi wa Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni mwa mwaka huu, Mheshimiwa Waziri alinipa msaada wa Maafisa wake wa Ardhi, Makao Makuu kwenda nao Kibaha kushughulikia tatizo la Ardhi Kibaha. Maeneo husika yalikuwa Mwanalugali na Sofu, Kata ya Tumbi. Maeneo hayo yamegubikwa na mgogoro wa Ardhi kati ya wakazi na Halmashauri ya Wilaya bya Kibaha. Mgogoro unahusu fidia, upimwaji na ugawaji wa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Afisa Ardhi, Naibu Mkurugenzi, nilikwisha kwenda naye kwenye maeneo husika, nitashukuru sana kama Wizara sasa itatoa mapendekezo yake au uamuzi wake wa jinsi ya kumaliza kadhia hiyo. Wananchi wa Mwanalugali na Sofu, Wilayani Kibaha, wanakuwa wakingojea kwa hamu ufumbuzi wa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukrani zangu kwa ushirikiano wa Mheshimiwa Waziri. Natamka tena kuwa naunga mkono hoja ya Waziri. Nawatakia kazi njema.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ningeomba kutoa rambirambi kwa ndugu zetu wapendwa Waheshimiwa Wabunge wawili waliotutoka wakati tukiwa hapa Ndugu yetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini na leo Ndugu yetu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira. Kwa niaba ya wapigakura wangu wa Jimbo la Igalula, naomba kutoa pole na rambirambi kwa wote waliopatwa na msiba huu kuanzia sisi mpaka jamii yote ya Marehemu. Mungu aweke roho zao mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuwashukuru wote waliotushukuru Waziri na mimi na watendaji wote kwa kuona kazi ambayo tunaifanya katika kipindi cha mwaka huu mzima, tuliyoyafanya mazuri wametushukuru na mengine ambayo yalikuwa yana utata wametushauri, tunawashukuru sana kwa kuwa karibu na sisi katika utendaji wetu wa kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na mimi ningependa pia nichangie hoja kadhaa ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa kwa kujaribu kutoa majibu mbalimbali na pia kuchangia kama mchangiaji katika hoja hii ambayo naiunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamechangia kuanzia kwenye bajeti ya Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na pia kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula na kwenye hoja ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wote Waheshimiwa Wabunge wamechangia mengi kuhusiana na Wizara yetu. Lakini na sisi tumekuwa makini tumetoa majibu haraka haraka na Waheshimiwa Wabunge wote wanayo. Kwa hiyo, leo tunarudia au kukumbusha tu yale majibu ambayo tulishatoa. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, nyaraka ambazo tumezigawa naomba mzisome kwa makini, mje na majibu ambayo mmeyazungumza, mmetushauri kuhusu sera tumeeleza,

mmetushauri kuhusu utendaji wa kazi, tumeeleza mgawanyo ulivyo wa Wizara, Halmashauri mpaka Serikali nyingine kuu ambazo ziko Mikoani na Wilayani.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, hizi nyaraka naomba sana mtaielewa vizuri Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na kuiongoza tena kutusaidia, mkisoma nyaraka hizi itawasaidia sana hasa huko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza wakati labda nianze na hoja hii ya ndugu yangu, njia moja, Ndugu Edward Ndeka, Mbunge wa Kigoma Kusini. Bahati nzuri alichangia katika Kamati na majibu tumempa. Lakini leo amerudia pia kutukumbusha yale aliyochangia, lakini atazame katika kitabu kile majibu ya ufasaha kabisa tumempa na bado tutakuwa na yeye katika kumsaidia. Lakini kwa taarifa tu kwamba katika kupima vijiji kutokana na yale aliyozungumza kwamba ni Mkoa wa mpakani matatizo ya wakimbizi. Lakini kwa taarifa yako Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wa Mkoa wa Kigoma mmo katika orodha ya mikakati ya kupima vijiji katika kipindi cha mwaka huu wa bajeti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika nchi nzima tunatarajia kupima vijiji kama 750 lakini kipaumbele tutakipa Mkoa wa Kigoma kutokana na hayo ambayo umeyazungumza. Lakini nakuomba na naomba Waheshimiwa Wabunge wa Kigoma zishaurini Halmashauri zenu kwa sababu hatuwezi kupima bure, kuna gharama kubwa ambazo ni muhimu kuchangia. Kwa hiyo, Halmashauri na ninyi mkajiandae, mkirudi majimboni kwenu mkawaambie waanze kuweka akiba kidogo kidogo ili wataalam kutoka Wizarani watakachokuwa nacho kitasaidia kupima vijiji ambavyo havijapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, amezungumza kuhusu mama wa Tabora. Namshukuru kutoka Pemba mpaka Tabora kwenda kujua tatizo la huyu mama wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi mimi naona tuwasiliane, kama kweli aliyoyazungumza huyu mama, Kada wa CCM, kanyang’anywa kiwanja chake, halafu wanajenga kituo cha mafuta. Lakini nafikiri tatizo siyo la Wizara, bila shaka ni kule kule Mipangomiji na Maafisa Ardhi kuweza kunyang’anya kiwanja hiki kujenga hicho kituo. Lakini kama matatizo haya yapo naomba Mheshimiwa Mbunge wa Tabora Mjini na ndugu yangu mtoa hoja basi tuwasiliane ili tutatue tatizo hili ili huyu mama asinyanyasike kama ulivyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirejee kwa wale ambao wamezungumza na wengine kwa njia ya maandishi na kwa mdomo. Ndugu yangu Mheshimiwa Frank Mussati, Mbunge wa Kasulu Mashariki, ameshauri kuhusu elimu, ni muhimu kusambazwa, kuhusiana na vifaa vya ujenzi wa gharama nafuu. Ni kweli Wizara yangu kupitia wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba bora na vifaa vya ujenzi inafanya utafiti wa vifaa vya ujenzi vinavyopatikana hapa nchini na kutokana na utafiti huo vitasambazwa kwa vyama vya ushirika vya ujenzi, mashirika mbali mbali, watu binafsi na Serikali kwa ujumla. Kwa njia ya semina, warsha, mafunzo ya nadharia na vitendo, pia na maonyesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongeza uzalishaji, bei za vifaa vya ujenzi vitashuka na hivyo kuwezesha wananchi wengi kujijengea makazi bora bila kuingiliwa na kodi ya vifaa vinavyoagizwa nje.

Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, amechangia kwa maandishi kwamba maeneo yawekezwe kwa ajili ya ujenzi wa maeneo mbalimbali katika Mji wa Namtumbo na kweli Wizara itazingatia uidhinishaji wa mipango hii ili iweze kutekelezwa kama ilivyokubalika. Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, usiwe na wasiwasi Wizara itakuwa karibu na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba pia kuzungumza machache aliyotueleza Mheshimiwa Paul Kimiti, kwamba Wilaya ya Sumbawanga na Mkoa kwa ujumla una sifa ya ujenzi wa nyumba bora, *master plan* hawana. Mimi nafikiri hili jambo ni la kuzungumza na Halmashauri yake, waone kama je, ni muhimu kuweka *master plan* hivi sasa. Basi wakitayarisha na sisi Wizara tutawasaidia, asiwe na wasiwasi, lakini mambo yaanzie kwao, kwa sababu wao ndio wenye matatizo ya Mji na watajua namna ya kututafuta ili tuweze kushirikiana kutanzua tatizo hilo.

Mheshimiwa Jackson Makwetta, amesema kwamba kwa sababu ya umaskini wakazi wengi wa mji wanapenda kujenga nyumba *full bungalow* na hivyo kusababisha miji yetu kupanuka kupita kiasi na kumaliza ardhi ya kilimo.

Ningependa kumwambia Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwamba Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 inasisitiza umuhimu wa kujenga kwa kuelekea juu badala ya ujenzi wa kusambaa hali ambayo itatumia ardhi ndogo na hivyo kuacha maeneo mengi kwa ajili ya matumizi mengine kama ya kilimo na kadhalika. Kila Halmashauri ya Mji na Wilaya ina mamlaka ya kuandaa sheria ndogo ndogo ya ujenzi ambao utasaidia kuboresha sura ya Miji yake. Lakini bado kama atahitaji msaada wa Wizara, tuko tayari kusaidiana, mradi tu watendaji wake wa Halmashauri waweze kufanya mawasiliano na Wizara kuwapatia watendaji.

Mheshimiwa Raphael Mlolwa, ameshauri kwamba Mji wa Kahama umeainishwa na TAMISEMI kuwa Mji Mdogo. Kuna umuhimu wa Mji huu kuwa na mpango wa kuuendeleza na kweli Miji Midogo iliyotangazwa ina umuhimu wa kuandaliwa mipango ya kuiendeleza. Ni jukumu la Halmashauri ya Miji hiyo kuiandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuongeza ukuaji wake. Wizara yangu itasaidia katika kutoa ushauri wa kitaalam pale itaomba kufanya hivyo na pia niliwahi kutembelea Wilaya ya Kahama na haya yalijitokeza na nilimshauri vile vile. Lakini nashangaa kwamba bado hawajaanza na Mheshimiwa Mbunge namshukuru kwa kukumbusha tena. Lakini hili jambo liko katika mikono ya Halmashauri na nilipotembelea hapo nilieleza hayo hayo na waanze mara moja kufanya matayarisho ya huu mji ili tuupange vizuri Mji wa Kahama.

Mheshimiwa Phillip Magani, amezungumza kwamba baadhi ya Maofisa wa Mipango Miji hawatekelezi taaluma zao kuhusu mabadiliko ya matumizi ya ardhi. Maeneo ya viwanda yatenganishwe na maeneo ya makazi, maeneo ya makazi yawekewe

miundombinu, maeneo ya *Oysterbay* na Masaki yanavamiwa na ujenzi unaoharibu sura ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2004/2005 Serikali imeandaa sheria itakayosimamia taaluma ya mipango miji ambayo itawadhibiti maofisa ambao watafanyakazi bila kuzingatia maadili ya kazi. Wakati wa kupanga maeneo kwa matumizi mbalimbali ya ardhi mara nyingi maeneo ya viwanda, hasa viwanda ambavyo vinaanza kuleta madhara kwa wananchi, huwa yanatazamwa. Sera ya Maendeleo ya Makazi inasisitiza umuhimu wa kuweka huduma ya makazi kabla ya viwanja kutolewa. Ujenzi kwa mtu anayeendelea kufanyia katika maeneo ya *Oysterbay* na Masaki unafanywa kutokana na utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Makazi ambao unazingatia utumiaji mkamilifu wa miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, usimamizi wa karibu unafanyika ili kuona kuwa ujenzi huo unaendelea na taratibu za ujenzi unavyoruhusu. Kwa hiyo, Halmashauri bado ni eneo muhimu waweze kutazama miji yao inapangwa namna gani siyo miji ya nje ya Dar es Salaam. Hata Dar es Salaam pia imo katika mlolongo huo kwamba wao wadhibiti maeneo katika ujenzi.

Mheshimiwa Leonard Derefa, amesema udhibiti wa ujenzi holela katika Mji wa Mwanza na Dar es Salaam iwekewe udhibiti, usimamizi na ukaguzi. Ningeshauri kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Dar es Salaam na ile ya Jiji la Mwanza kama nilivyosema hapo awali katika jibu la ndugu yangu Mheshimiwa Pillip Magani kwamba na jibu la lile Jiji la Mwanza liongezewe uwezo wa wataalam na fedha kwa ajili ya kupanga, kupima, kulipa fidia maeneo ya makazi na pia kuongeza viongozi vya udhibiti wa ujenzi mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho siyo kubomoa, bali ukarabati na kujenga miundombinu. Kanuni mpya za ujenzi mijini zitatangazwa hivi karibuni ambazo zinaelekeza uzingatiaji wa udhibiti wa ujenzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira ya wahandisi na wakaguzi wa majengo ziongezwe kwenye Halmashauri na waajiriwa hao wapewe usafiri wa kutosha kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti, pia ameshauri Shirika la Nyumba la Taifa lijenge nyumba za ghorofa za kupangisha kuliko kuendelea na ujenzi wa nyumba moja moja kama ambazo hazihitaji eneo kubwa na hivyo kutumia ardhi kubwa kwa watu wachache. Shirika la Nyumba la Taifa linajenga nyumba za aina zote. Hata ukifika Dar es Salaam utaziona yaani nyumba moja, moja, kuzingatia matakwa ya soko kwa vile ni za kuuza. Aidha, zinajengwa nyumba za maghorofa katikati ya mji hapa jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupangisha.

Pia Mheshimiwa Joel Bendera, ameomba mnunuzi wa nyumba Na. 137 Dodoma aongezewe muda wa kukamilisha malipo haya. Si huyo tu, wengi wameomba kuongezewa. Lakini kila mara wakileta barua kwa Waziri au kwangu, tunawashauri

kwamba wawasiliane na Tawi. Lakini Serikali inahimiza kwamba ifikapo mwezi wa Agosti, 2004 wawe wamekamilisha malipo kwa sababu tangazo hili limetokea muda mrefu karibuni miaka tisa kwamba nunueni nyumba. Lakini watu wameweka kwamba bado, labda kesho, labda kesho, kesho yake ndiyo matokeo hayo sasa muda umekwisha.

Kwa hiyo, ombi lake huyu binafsi naomba aendelee kushirikiana na Tawi halafu baadaye Makao Makuu, Wizara tutaliona kama lina umuhimu wake lakini wajitahidi mwezi wa Agosti, 2004 ni mwisho kulipa. Lakini kila mmoja alete ushauri wake au maombi yake binafsi. Sio kwenye kampuni au siyo kwenye *group* la wapangaji. Kila mwenye shida alete shida yake binafsi, itatazamwa lakini bado Serikali iko pale pale kwamba tunaomba mwezi Agosti, 2004 mmalize la sivyo ukishindwa basi mwachie mwingine mwenye nguvu anunue.

Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, kazungumzia Shirika la Nyumba na Taifa lielekeze kujenga nyumba za gharama nafuu katika Mji wa Mugumu, Serengeti ili kuondoa kero ya ukosefu wa nyumba kwa wananchi mjini. Kwa mujibu wa Sera ya Uchumi linalofuatwa sasa Shirika la Nyumba la Taifa ni chombo kinachofanya shughuli zake kibiashara. Kwa hali hiyo, inatoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za kuuza. Lengo ni kuzungusha mtaji mdogo uliopo kwa kasi zaidi na hivyo kuliwezesha kujenga nyumba nyingi na kuwahudumia wananchi wengi zaidi. Shirika la Nyumba la Taifa litakuwa tayari kujenga nyumba za makazi katika mji wa Mugumu ikiwa wanunuzi wa uhakika wa nyumba hizo watapatikana.

Naomba Mheshimiwa Mbunge, uwasiliane na uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa katika utekelezaji wa jambo hili. Lakini kuweko kweli na wateja, la sivyo tusiweke pesa ambazo hazizalishi na hili Shirika linajitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ali Said Salim, amesema migogoro baina ya wakulima na wafugaji vijijini. Nakiri kuwa baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Shinyanga pekee hawajapata vitabu hivi kwa sababu vilikwisha.

Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2004 Mkoa huo utapata vitabu vyote baada ya kuvichapisha kiasi cha kutosha. Kwa hiyo, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Kagera, Kigoma, Rukwa na Lindi kuwaagiza Ma-*RAS* na Wakurugenzi Watendaji wapeleke vitabu hivyo, Pwani tumekwishavipeleka. Ni kwa mikoa hiyo tu ambayo hatujapeleka, lakini vingi ya vitabu vimepelekwa, sasa badala ya *RAS* kusambaza au kuwapelekea Halmashauri au Halmashauri kupeleka Vijijini au kwenye Tarafa, hapeleki vinakaa kwenye *Museum,* naomba kuwahimiza Wabunge kwa sababu sisi ndio wakereketwa, wapigiwa kura, twende katika Ofisi hizi ili tukaone vitabu vipo, ili tuchukue jukumu katika ziara zetu tuwasambazie.

Narudia kuhusu migogoro ya ardhi na wafugaji inayosababisha kuhama hama. Ndugu zangu Wasukuma, nafikiri ndiyo wanalengwa hapa. Waheshimiwa Wabunge napenda kurejea Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 2000 kuwa kila raia wa Tanzania ana haki ya kwenda kuishi mahali popote ili mradi havunji Sheria ya nchi. Ndiyo maana hata Wapemba wengi

wapo Tabora. Nasisitiza kuwa tangu tarehe 1 Mei, 2001 Sheria ya Ardhi ilipoanza kutumika kwa ardhi ya Kijiji inasimamiwa na Halmashauri ya Kijiji. Waheshimiwa Wabunge naomba muendelee kuwahimiza Maofisa wa Halmashauri ya Wilaya kuwaelimisha Halmashauri za Vijiji ziweze kusimamia ardhi ya vijiji iliyoandikisha wahamiaji halafu vijiji wanafuata mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niendelee na Mheshimiwa Ali Said Salim, alisema kwamba kiwango cha shilingi 500,000/= ni kikubwa sana katika kununua Kiwanja Dar es Salaam ukilinganisha na wananchi wengi na vipatao vyao hata shilingi milioni moja haifiki. Kutokana na tuhuma nyingi zilizokuwepo katika upatikanaji wa viwanja vya Dar es Salam, Serikali ilichukua mkopo wa shilingi bilioni 8.9 ili kuwapatia wananchi wa Dar es Salaam viwanja 20,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji ya mradi huo imegawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Naomba msome ili muwaeleze wananchi wenu kwamba kama kuna ulanguzi, sidhani, lakini kazi imefanyika. Katika upatikanaji wa viwanja hivi, ilibidi ardhi ichukuliwe chini ya Sheria Na. 4 ya mwaka 1969 kwa kulipa fidia, kupanga, kupima, kugawa viwanja hivyo kwa wananchi waombaji kwa Kamati za Manispaa.

Aidha, wananchi wote waliokuwa na ardhi katika maeneo ya mradi walilipwa fidia kwa wakati na wenye nyumba walipewa viwanja kwa gharama ya upamaji isiyozidi laki moja na hawakulipiwa gharama za miundombinu, gharama za viwanja hivi imefikia shilingi 500,000/= na hawakulipia gharama za miundombinu, vile vile ni nia ya Serikali kurejesha mkopo unaotajwa bila kumvalisha mwananchi asiyehitaji kiwanja gharama hii kupitia kwenye kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa gharama hii ya shilingi 500,000/= bado ni asilimia 80 tu ya gharama zote kwa vile mishahara haikujumuishwa katika utekelezaji, kwa sasa hakuna hakuna upungufu wa viwanja katika Jiji la Dar es Salaam, labda wale ambao wamehodhi hawataki kuvilipia wala kuvirudisha ili wenzao wenye mahitaji waweze kupata. Pia ameendelea kusisitiza kwamba Shirika la Nyumba la Taifa kutakuwa na Mahakama ya kumlipa mpangaji wa jengo la Hoteli ya *Etiens* lililopo Upanga Dar es Salaam shilingi milioni 600 katika kesi ya madai ya kutolipwa kodi ya pango iliyofunguliwa Shirika lenyewe.

Ni kweli mpangaji wa *Etiens Hotel* anadaiwa malimbikizo ya kodi ya shilingi 205,114,920/=. Kutokana na hali hiyo Shirika limempeleka Mahakamani. Kabla ya kesi kuamuliwa Jaji alitoa amri ya Shirika kumlipa mpangaji milioni 600 ikawa ajabu, Shirika limepinga amri hiyo kwa vile siyo haki, kwa vile suala hili liko Mahakamani, siyo vizuri kulizungumzia kwa undani. Hivyo nashauri tusubiri Mahakama itoe uamuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, amesema amekabidhiwa barua ya kiwanja mbadala Mikocheni “A” baada ya kiwanja cha Msasani kupewa mwombaji mwingine. Utaratibu wa kupatikana viwanja kwenye maeneo yaliyokwishagawiwa hupitia hatua nyingi. Hata hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Kamishna wa Ardhi kama siyo Dar es Salaam hata leo yuko hapa afanye

muda muafaka akamwone amwelezee ili suala lake liweze kupatiwa ufumbuzi. Ameeleza pia umilikaji wa ardhi wa *TIC* na Balozi mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu haina mamlaka ya kuziamulia Balozi au Taasisi nyingine nchini mahali pa kuomba viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Wizara yangu ni kushughulikia maombi kama yalivyowasilishwa kwa taratibu na sheria zilizopo. Hivyo Baraza likiomba viwanja Dodoma vitatolewa. Uamuzi wa Balozi zijengwe wapi siyo suala la Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Kwaangw', ameuliza kwa nini Mkuu Wilaya siyo Mwenyekiti wa Kamati ya kugawa ardhi? Ni vigezo gani vimetumika? Utaratibu wa zamani wa Mkuu wa Wilaya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kugawa Ardhi uliondolewa na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 chini ya kifungu cha 12. Kwa hiyo, nakuomba na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge tuliwagawia Hati hizi zote ambazo nafikiri baada ya Sheria kupita hii ya mwaka 1999 mlipata Sheria ya 69 Na. 4 na Na. 5. Kwa hiyo, nina hakika Mheshimiwa Mbunge ukiisoma hii ataona jinsi gani huyu Mwenyekiti ameondolewa. Sheria hiyo inatekeleza na Kanuni za Kamati ya Kugawa Ardhi zinazopaswa kuundwa kwenye Mamlaka ya Wilaya kwa sababu hiyo, Mkuu wa Wilaya ambaye si sehemu ya Halmashauri, kisheria hawezi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolewa kwa ardhi pasipo kulipwa fidia. Mheshimiwa Omar Kwaangw', ameendelea kulizungumzia hilo kwamba, Sheria na Kanuni za Ardhi zimeelekeza fidia kulipwa wakati ardhi ya mtu inapotwaliwa. Aidha, iwapo ardhi husika inagawiwa kwa mtu au Taasisi inabidi, fidia hiyo irejeshwe kutokana na malipo yanayofanywa kwa kupewa ardhi hiyo. Kufanya kinyume na utaratibu huo ni ukiukaji wa Sheria. Hivyo Kamati ya Kugawa Ardhi inashauriwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ardhi wakati wa kutoa na kugawa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Frank Mussati, alisema nyaraka za ardhi ziwe katika lugha ya Kiswahili. Wizara imekwishaanza kutafsiri Sheria na nyaraka za ardhi ziwe katika Kiswahili. Hadi hivi sasa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 69, Kanuni za Ardhi ya Vijiji ya mwaka 2001 nikijumlisha nyaraka zinazotumika kwenye ardhi ya vijiji ni pamoja na hati za kumiliki na barua ya toleo *(Offer)* tayari imekwishaanza kutafsiriwa katika lugha ya Kiswahaili kwa manufaa ya watu wengi zaidi na wananchi hasa vijijini. Hatua inayoendelea hivi sasa kufanya tafsiri ya aina hiyo hiyo kwa Sheria ya Ardhi Na. 5. Lakini mkumbuke kwamba Waheshimiwa Wabunge, Sheria nyingi bado zinatungwa kwa Kiingereza. Kwa hiyo, Kiswahili kwa kweli Wizara imejitahidi sana, kwa hiyo, tunastahili pongezi kwa kutafsiri sheria hizi ambazo tumewapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Herbert Mntangi, amesema kwamba ugawaji wa ardhi usiozingatia taratibu. Mamlaka ya kugawa ardhi imewekwa chini ya Halmashauri kupitia Kamati za Kugawa Ardhi zilizoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999.

Aidha mamlaka na nidhamu ya watumishi kwa sekta ya ardhi ndani ya Halmashauri, ni jukumu la Halmashauri zenyewe. Ingawa hapa nimekuwa napata maswali kila siku kwamba watumishi wa Halmashauri wana matatizo, rushwa, wanyanyasaji, lakini kwa kweli mdhibiti wa nidhamu ni Halmashauri. Sisi tunatafuta wataalam, tunawapa Utumishi, Utumishi wanawapa Halmashauri kutokana na ajira wanazozihitaji. Kwa hiyo, iwapo mtumishi wa sekta ya ardhi ni mzembe, mbabaishaji, mla rushwa na hivyo kugawa ardhi nje ya utaratibu uliowekwa na sheria, ni wajibu wa Halmashauri kumwajibisha vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia pia suala la kuimarisha Ofisi za Sekta ya Ardhi katika Halmashauri. Kwa kuwa kuimarisha Ofisi za Sekta ya Ardhi katika Halmashauri ilikuwa ni moja ya malengo ya Wizara kwa mwaka 2003/2004, Wizara imekwishachukua hatua za awali kwa kutembelea Ofisi za Sekta za Ardhi katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na Muheza. Baada ya kuona hali halisi ya Ofisi hizo, Wizara inaandaa mkakati wa kuimarisha Ofisi hizo kwa kushirikiana na TAMISEMI. Lakini pia natoa wito kwamba huwa tunarejesha hela za kodi ya ardhi. Halmashauri wakikusanya wanaleta Wizarani lakini 20% inarudishwa kwao. Halmashauri nyingine wamekuwa wanazichukua wanaziingiza katika bajeti zao lakini hizi moja kwa moja zinakwenda katika Ofisi za Ardhi ili kuimarisha ofisi zao, kununua dhana ndogo ndogo na mahitaji madogo madogo.

Kwa hiyo, natoa wito tena Halmashauri na Wakurugenzi hizi fedha tunazozirudisha kutoka Ardhi, naomba zibakie katika Ofisi ya Ardhi lakini bado Halmashauri ina wajibu wa kuimarisha Ofisi hizi za Ardhi katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Paul Kimiti, ameendelea kusema kwamba uthamini wa ardhi na majengo kwa ajili ya kupata mikopo unaofanywa na wathimini wa Serikali haukubaliki na Mabenki. Wizara yangu haijapata taarifa rasmi kutoka kwenye Mabenki kuhusu kutokubali uthamini unaofanywa na wataalam wa Wizara. Hata hivyo, uthamini ambao haugusi maslahi ya Serikali unaweza kufanywa na kampuni binafsi ya uthamini ambayo imeandikishwa na kupewa leseni ya kufanya kazi za uthamini nchini. Lakini pindi ambapo kuna wathamini ambao wanakuja katika maeneo yenu, hawana leseni, hawana ujuzi, hawana utaratibu wowote ule ni wajibu wenu kuripoti katika Halmashauri zile wakachukuliwe hatua kama ikizidi basi Wizara tuko tayari kupokea malalamiko hayo na kuyafanyia kazi lakini kuna wapimaji, wathamini wa Wizara, Serikali na binafsi na wenye kutambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi pia ameeleza kwamba Ofisi nyingi za Ardhi ndani ya Halmashauri bado zimejaa uzembe, ubabaishaji na labda wala rushwa. Hivyo utendaji kazi kwa misingi na nidhamu kama Wizara ni muhimu sana. Ni kweli. Utaalam tunatoa sisi lakini udhibiti wa nidhamu ni pale anapofanyia kazi Afisa huyo. Bado naendelea kuomba tena kama nilivyosema hapo awali kwamba mfanyakazi yeyote yule siyo Wizara ya Ardhi tu, Kitengo chochote kile kama hana nidhamu, mla rushwa na mna ushahidi kwa nini asichukuliwe hatua? Pamoja na kutueleza hapa leo katika Bajeti ni sahihi, lakini bado naona kwamba kazi inarudi kule kule kwenu mkiwa

ninyi Madiwani, mnaenda katika vikao, ni mahali muafaka pa kuwazungumzia halafu zikachukuliwa hatua za nidhamu mara moja wakaondolewa.

Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, aliuliza kwa nini Wizara mbalimbali za Serikali hazishirikiani katika utekelezaji wa mipango mbalimbali na hivyo kuwasababishia wananchi hasara? Ni kweli kuwa kila Wizara inafanya kazi zake kwa kuzingatia sheria zilizotungwa kwa shughuli hizo na mara nyingine kumekuwa na mgongano wa sheria hizo na hivyo kusababisha hasara kwa wananchi. Nachukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kutoka Kambi ya Upinzani inayosema kwamba urasimu wa kutoa viwanja unachangia watu kujenga mabondeni. Kujenga mabondeni hakusababishwi na urasimu wa kutoa viwanja ndugu zangu, husababishwa na uhaba wa viwanja pamoja na ukaribu wa sehemu hizo na mjini na pia sehemu za kazi. Mfano hai ni ule wakati wa mafuriko ambapo watu wa mabondeni walipimiwa viwanja maeneo ya Wazo, lakini wengi wao waliviuza na kuendelea kubaki mabondeni. Ili kuondoa uhaba wa viwanja, Wizara yangu ilibuni mradi wa viwanja 20,000 ambavyo vinaendelea kuuzwa na vingine vinasubiriwa. Lakini kuna wengine wamechukua viwanja mpaka leo bado hawajaviendeleza na sheria inasema kama huendelezi kiwanja baada ya miaka mitatu basi mpishe mwenye nguvu ajenge badala ya kuacha pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuongea hayo machache, najua wengi ambao mmechangia mtapata majibu kwa maandishi. Kwa hiyo, ninachoomba tu ndugu zangu muunge hoja hii mkono leo tupate hizo fedha kidogo tulizoziomba ili tukaendeleza, pale ambapo mmetusifia tumefanya kazi kwa sababu msipotupa ile sifa itakuwa imeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Awali ya yote, napenda kuwashukuru na kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu. Waliochangia kwa kuzungumza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Salama Khamis Islam, kwa niaba ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Rhoda Kahatano, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Hadija Kusaga, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Edson Halinga na Mheshimiwa *Hajjat* Tatu Ntimizi. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Abdulkarim

Shah, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Hebert Mntangi, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Mheshimiwa ambaye sikumtaja mnaweza kunifahamisha ili niweze kumtambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Waheshimiwa Wabunge 42 ambao walichangia sekta ya Ardhi na Makazi katika mijadala yote iliyopita katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bajeti tangu hotuba ya Waziri wa Fedha, Mipango na Ubinafsishaji, Waziri Mkuu, TAMISEMI na kadhalika. Tumejitahidi kuzijibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na tumeziwasilisha kwao kwa maandishi. Nawashukuru sana wote kwa michango yao mizuri na tuko tayari kuendelea kuwasiliana endapo ufafanuzi zaidi utahitajika au kama upo ushauri mpya.

Aidha tumejitahidi kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wakati wa kuchambua na kupitisha Makadirio ya Wizara yangu na tumekwishawasilisha majibu kwa maandishi. Nao pia nawaomba kama kuna mahali bado kunahitaji ufafanuzi, tuko tayari kuendelea kufafanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa *Hajjat* Tatu Ntimizi, Naibu Waziri kwa kuunga mkono hoja yangu na kwa kunisaidia kwa kiasi kikubwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mimi nitajielekeza katika maeneo machache ambayo nadhani pengine yanahitaji maelezo au ufafanuzi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Salama Khamis Islam, kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati kwa ufasaha. Naishukuru Kamati kwa taarifa yake nzuri na mapendekezo mazuri ambayo wameyatoa na yote tunayaafiki kwa asilimia mia moja kwa hiyo hakuna sababu ya kujibu hoja moja moja. Hoja zote kuanzia 4.1 mpaka 4.11 zote tumezipokea na nyingine tumeanza kuzifanyia kazi na tutaendelea kuzishughulikia. Hii inadhihirisha jinsi Kamati ilivyo karibu na Wizara yangu, jinsi tunavyoshirikiana, wanaelewa nini kinafanyika, wanatushauri, tunayapokea, tunaendelea na utekelezaji, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo mchango wa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Kwanza, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Ali Said Salim, Msemaji Mkuu wa Upinzani kwa Wizara hii kwa mchango wake mzuri. Aidha, namshukuru kwa ushirikiano wake, hatujawa na purukushani zozote, tunashauriana, tunawasiliana bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maoni na mapendekezo ya Mheshimiwa Ali Said Salim, ambayo ni mengi kuanzia Aya 2.1 hadi 2.18 pamoja na nyongeza ambayo ameiwasilisha leo asubuhi. Mapendekezo ni mengi hatuwezi kuyajibu yote lakini napenda niahidi kwamba kama alivyofanya ameyaandika na sisi yote tutayajibu kwa maandishi ili na yeye awe na kumbukumbu ya hoja zote ambazo amezitoa na kama bado kutakuwa na maeneo yana utata basi tuko tayari kuendelea kuwasiliana ili kuweka mambo sawa kwa yale ambayo aliyazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda niseme kwa jumla tu kwa Mheshimiwa Ali Said Salim na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba tumejitahidi kutoa nyaraka mbalimbali za sera, sheria na majibu mbalimbali ambayo tumekuwa tukiyatoa kwa maandishi. Rai yangu ni kwamba naomba tujitahidi kuzisoma, masuala mengi ambayo yanajitokeza, yanajirudiarudia kwa yale ambayo tayari ama tumekwishayajibu au yako kwenye sera zetu. Kwa hiyo, naomba tujipe muda kurudia ili kwa kweli yaweze kutusaidia katika shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, basi labda kwa ufupi tu nigusie machache ya Mheshimiwa Ali Said Salim, ili angalau tutoke na kitu pamoja na kusubiri hayo ambayo tutapewa kwa maandishi.

Mheshimiwa Stephen Kazi na wewe umechangia kwa maandishi. Tunakushukuru sana lakini kama hatutajibu hoja zako pengine ni muda wa kuwasilisha lakini tutazijibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitaje mambo machache ambayo pia yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Suala la bajeti, tumekiri kwamba bajeti yetu bado ni ndogo, finyu, kazi ziko nyingi kwa hiyo, hatuwezi kutekeleza mahitaji yote. Sisi wenyewe tutaendelea kutafuta mbinu mbalimbali za kujiongezea uwezo kifedha ili tuweze kutekeleza mengi yale ambayo tunahitaji kuyatekeleza kwa ngazi ya Taifa lakini kwa ngazi ya Halmashauri na TAMISEMI tunaendelea kuombana kwamba katika bajeti zetu za kila mwaka tuhakikishe kwamba masuala yanayohusu sekta ya ardhi tusisahau kuyapangia fedha katika maeneo yetu. Kwa hiyo, tukishirikiana kwa pamoja pengine tunaweza kupiga hatua kubwa zaidi katika kutekeleza majukumu ambayo yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango, kila mwaka tuna mpango wa kazi na hata hivi sasa Katibu Mkuu na timu yake wapo hapa tukimaliza tu bajeti hii wanakaa wanapanga utekelezaji wa yale tuliyoyapitisha hapa. Kwa hiyo, kila mwaka tunapanga na tunasimamia matumizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ali Said Salim, nikuondoe hofu kwamba mambo yetu yanakwenda kisayansi, tunajitahidi kuyapanga, kuyasimamia na kuyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niligusie ni mradi wa upimaji wa viwanja 20,000 Jijini Dar es Salaam. Kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamepita huko wametupongeza na kwa kweli ningeomba Waheshimiwa Wabunge wote mkipata nafasi mpite katika maeneo hayo muone kazi inayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam lilikuwa limejaa katikati, sasa hapa nitajibu na hoja ya Mheshimiwa Jackson Makwetta, Sera ya Makazi ipo, wataalam katika miji yetu yote wanayo, wanahitaji kusimamia ujenzi na uendelezaji wa miji yetu. Humu ni ruksa kujenga ghorofa moja, ghorofa 20 sera inatoa uwezo na mipango ya kila mji lakini katika Jiji la Dar es Salaam lilikuwa na msongamano katikati hata tukisema tuanze kujenga maghorofa hayatoshi ni lazima tuipanue na huko tulikopanua maeneo 11 hayo yakijengwa na baadaye tukajenga maghorofa sasa mji utakuwa umepanuka na kuweza kubeba watu wengi zaidi kuliko ilivyo sasa. Kwa hiyo, mradi huu ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kujibu kwa hoja ambazo zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, mradi huu hauondoi kazi ya kawaida ya Manispaa za Dar es Salaam kuendelea kubuni na kupima viwanja kwa ajili ya wananchi katika hali ya kawaida. Huu ni mradi maalum, haujasimamisha shughuli nyingine za Manispaa, waendelee kuainisha maeneo na kupima na kuwagawia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mradi maalum ambao Wizara tuliona tuingilie kati tusaidie tatizo ambalo lilikuwepo.

Kwa hiyo, mradi huu usiwe tena ni nongwa kwamba sasa unazuia wananchi kupata viwanja kwa bei nafuu, hapana Manispaa endeleeni kubuni na kugawa viwanja kwa bei nafuu kama mnaweza, lakini huu ni mradi maalum wa kujaribu kutatua tatizo maalum na ni gharama na tunalifanya kwa mkopo ambao lazima urudi na miondombinu yote tunaishughulikia wenyewe. Barabara sio Wizara ya Ujenzi wanaojenga ni ndani ya mradi ndio maana kidogo gharama zimekuwa kubwa. Lakini tumejifunza kwamba pengine tutakapoendelea, tunawezesha kuhusisha sekta nyingine ili kupunguza gharama. Wanaohusika na barabara wajenge barabara, wa umeme walete umeme, wa maji walete maji ili gharama za viwanja ziweze kuwa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shamba la Bagamoyo. Mheshimiwa Ali Said Salim, taarifa umetupa leo asubuhi, tutaendelea kulichambua tufanye uchunguzi, tukikamilisha tutakupa majibu kamili, nadhani utaridhika na majibu haya.

Jambo lingine ambalo nataka niligusie kwa ufupi ni suala la utendaji, limezungumziwa sana. Tunashukuru tumepongezwa tunajitahidi katika utendaji katika ngazi ya Wizara, lakini mmezungumzia katika ngazi ya Halmashauri zenu. Naendelea kutoa wito, usimamizi uko huko huko kwenu, nawaomba sana. TAMISEMI naomba tusaidiane ili hali nzuri inayoonekana katika ngazi ya Taifa basi iendelee mpaka huko chini na tuendelee kusimamia kwa karibu, bila kuogopana lakini kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niligusie kwa kifupi, tunajitahidi kupiga vita rushwa za aina zote, vita bado ipo na ni ya kuendelea. Suala la rushwa linaonekana ni nyeti, gumu na ambalo halina ufumbuzi. Nadhani Watanzania

tuamue kwamba suala la rushwa sio gumu, sio nyeti na linaweza kutatuliwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naungana na Mwandishi wa Kitabu cha Methali, anayesema anamwomba Mungu anasema naomba usinipe umaskini wala utajiri lakini unipe chakula cha kunitosha kwa kadri yangu. Si-*quote* moja kwa moja, lakini naeleza yaliyomo humo, usiombe upewe umaskini wala utajiri, lakini omba upewe chakula cha kukutosheleza kadri ya hali yako. *(Makofi)*

Mwisho napenda kutoa shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, kwa jinsi wanavyotusaidia kutuelekeza kusimamia masuala ya sekta ya ardhi na makazi katika Taifa letu. Tumejitahidi kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 kwa zaidi ya 90%, naomba tuendelee kushirikiana kutekeleza sehemu iliyobaki. *(Makofi)*

Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wenu mwenu, kwa imani mliyonayo kwetu na sisi tunarejesha imani hiyo kwenu kwamba tutaendelea kutenda lile ambalo linatupasa kutenda kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

Nawashukuru Watanzania wote kwa jinsi walivyoanza kutambua umuhimu wa raslimali ardhi kwa maendeleo yao. Nawaomba waendelee kuitumia kwa ajili ya maendeleo yao bila migororo, bila kugombana, sheria na taratibu zipo tutumie raslimali yetu kwa kutuendeleza na kutuondolea umaskini hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Nawashukuru wananchi wa Ileje kwa uvumilivu wao, kwa ushirikiano wao, naomba tuendelee kushirikiana mpaka mwisho wa safari yetu na mwisho napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa uongozi wenu katika shughuli zetu za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na kama kawaida yetu, tunaahidi hoja zote za kuzungumza na za maandishi tutazijibu kwa maandishi kwa wote wanaohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

### Matumizi ya Kawaida

### Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... ...1,496,195,100/=

**MWENYEKITI:** Nawaona Waheshimiwa Wabunge watatu, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Omar Kwaangw' na Mheshimiwa Parseko Kone.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu hicho 1001, wakati nachangia niliuliza kwamba mradi wa kupima viwanja kwa mujibu wa sheria ambayo tumeipitisha hapa Bungeni ili waweze kuwasaidia wananchi nia ni kutumia ardhi na mashamba waliyonayo kwa ajili ya kupata mikopo katika vyombo vya fedha.

Sasa sikupata majibu kwa sababu ninavyoelewa kuna wanaopima ardhi mjini kwa sababu ya kuwapa watu viwanja vya kukaa na kujenga mahoteli, lakini *concern* yangu ilikuwa ni kwamba kwenye mashamba ya kawaida tunakwendaje kupima na kuna maelekezo gani wale wataalam wa ardhi walioko pale Wilayani waende kupima ili watu wale waweze kupata hati na utaratibu upi wa kuwarahisishia kwamba Serikali iwaelimishe na iwahalalisishie ili waweze kupima mashamba yao ya migomba, kahawa na nini ili waweze kupata mikopo? Nilikuwa nimeuliza hilo na kwa ajili ya kuwapa hati miliki ni utaratibu gani unatumika? Sikupata majibu.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kwanza ningemshauri tu haya masuala yote wataalam wako kwenye Halmashauri yako wanaelewa utaratibu wote. Tumechukua *initiative* kama Wizara kwamba ni muhimu tukatambua mipaka ya vijiji vyote nchi nzima lakini tunafanya hivyo kwa kushirikiana na Halmashauri husika hatuendi tu tukavamia mahali, tunawasiliana, tunakubaliana ndio tunakwenda kupima.

Sasa baada ya kutambua mipaka ya vijiji, hatua inayofuata ni kupima maeneo ndani ya kijiji nayo pia sio ya kulazimisha, wenyewe watake na wanavijiji katika maeneo yao ndio wanaosimamia. Kwa hiyo, sio suala la kulazimisha na kuingia tu kwenye eneo la mtu na kuanza kupima. Ni lazima mwenyewe atake, akubali na viongozi wa mahali pale ndio wanaosimamia kazi hiyo sisi tunapeleka utaalam tu wa kusaidia ili kazi iweze kwenda haraka.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la mipaka ya vijijini sikulilalamikia kwa sababu naelewa tangu zamani Serikali imekuwa ikipima mipaka ya vijiji na watu wana hati wale ambao hawajapima ni wale wanaobishania, vijiji vipya au kitu kingine. Mimi sisemi kwamba ni suala la kulazimisha, nimemwambia Waziri kwamba tunapoweka kanuni, sera, sheria lazima tuziwekee utaratibu wa ku-*facilitate* kwa njia ya elimu au njia nyingine. Kwa hiyo, nilichouliza sio wananchi walazimishwe ni kwamba sheria na kanuni hizi hawazifahamu. Wale walioko Wilayani wanaweza kuweka urasimu kwamba sisi hatuna hela ya kwenda kupima, wakawa wamekaa ofisini kama ambavyo wanakaa nadhani kila Mbunge anajua kwamba wanakaa pale. Hicho ndicho nilichotaka msukumo kwa njia ya ushauri, kuelimisha na kuwaelekeza ili waweze kupima na zoezi lile liweze kwenda kwa haraka sana tujue kwamba ni kipindi gani ambacho tunaweza kukamilisha zoezi hilo na iweze kupimika kwamba ni maeneo mangapi yamepimwa *qualitatively* na *quantitatively.*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani yote anayosema ndio tunavyofanya na wataalam wote wana taarifa hizi na miongozo na jinsi ya kufanya shughuli hizi na Waheshimiwa Wabunge karibu kila mwaka tumekuwa tukiyasema haya kwamba mtusaidie kufuatilia na kusimamia katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, akirudi kwenye Halmashauri yake awabane watalaam wa sekta ya ardhi, wasimamie kazi hii na kuwaelimisha wananchi na miongozi ipo.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu kitabu hiki ambacho kina idadi ya Vijiji vilivyopimwa, kimekosewa kosewa katika maeneo fulani fulani, kinahitaji kwa kweli kurekebishwa. Katika ukurasa wa 62, kwanza, sehemu iliyoandikwa Wilaya ni sawa, lakini *column* inayofuata badala ya kuandikwa Kijiji imeandikwa Tarafa. Halafu vile vile sehemu ile ya Tarafa inapaswa kuwa Kata. Lakini vile vile katika sehemu zingine za Kata, nazo Vijiji vyake vimekosewa. Kwa mfano, ukurasa wa 62, pale Manyara, Na. 76, 77 na 78, Kata ya Singe hakuna Kijiji cha Dyedabung wala Kijiji cha Endakiso. Inayofuata tena imeandikwa Kata ya Singe imeandikwa tena Kijiji cha Mutuka, siyo sahihi. Nadhani kwamba kitabu hiki kinahitaji kurekebishwa, tunaomba wakiweke vizuri na pengine kwa namna rahisi zaidi. Kwa hiyo, la kwanza lilikuwa hili kwamba kwa sababu hii imeonyesha kwamba inafuatana na hotuba ya Waziri, tunaomba marekebisho hayo yafanyike ili ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye ukurasa wa 27, Mheshimiwa Waziri amezungumza suala la Sheria ya Mahakama ya Ardhi na amekiri mwenyewe kwamba ile Sheria ya *Land Disputes Court Act, 2002* ilianza tangu tarehe mosi. Amesema hata hivyo Mabaraza ya Ardhi na Nyumba hayakuweza kuundwa kutokana na matatizo ya kiutendaji na sheria.

Sasa hapa kuna tatizo la msingi ambalo linahitaji kufanywa haraka na Serikali. Pale chini ameandika namna ya kutatua kufuatana na ufumbuzi wa matatizo haya, Wizara inalenga kuunda jumla ya Mabaraza 23 katika kila Mkoa, lakini hali iliyoko sasa hivi ni kwamba kuna baadhi ya Vijiji vina Mabaraza ya Ardhi. Hata watu wakipeleka kule hizo kesi zao hazina maana kwa rufaa. Mabaraza ya Kata hayajaundwa, hili la Wilaya halifanyi kazi, Mahakamani hawapokei hizo kesi, sasa tunafanya nini?

Kwa hiyo, watu wanapigwa danadana katika maeneo haya. Serikali lazima ituambie kitu katika hili ili wananchi wasiendelee kubabaika kwenda Mahakamani, wanawaambia nendeni kwenye Baraza, Mabaraza nayo mmeyasitisha kwa sababu ya matatizo yanayoonekana hapa ya kiutendaji na kisheria. Sasa tunataka kusikia kauli ya Serikali kuhusu utatuzi wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo yana matatizo makubwa sana ya ardhi. Kama sisi wengine migogoro ya ardhi ni jambo la kawaida na linafahamika. Tungependa hili kwa kweli liweze kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo kwa kweli nilikuwa nimeomba ni kuhusu Kamati ya Ugawaji wa Ardhi, sehemu yake kweli Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu, lakini sehemu nyingine hakujibu. Nimeuliza pale, sasa baada ya Halmashauri kuwa ndio inahusika na ugawaji wa ardhi kwa nini Mkurugenzi ndiye anakuwa Mwenyekiti wa Ardhi na Madiwani hawapo. Nilitoa ushauri kwamba na Mheshimiwa Waziri amesema tunataka ushauri mpya, ushauri mpya ni kwamba Mwenyekiti wa Halmashauri ndiye anayefaa kuwa Mwenyekiti wa Ugawaji. Sasa watendaji wenyewe ndio wanagawa viwanja, inakuwaje na migogoro ni mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Omar Kwaangw', kama ifuatavyo:-

Kwanza nikiri kwamba kile kitabu cha orodha ya Vijiji vilivyopimwa kina makosa katika maeneo kadhaa. Kwa hilo tunakiri, tumeona itabidi masahihisho yafanyike na tutaomba Waheshimiwa Wabunge kama mna marekebisho yoyote mnaweza kutusaidia kutupa ili tuendelee kukisahihisha na kukirebisha ili kiweze kuwa katika hali nzuri. Hilo tumeliona na tunakiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi ya Kata yamekuwepo kwa muda mrefu, pengine tatizo ni kule kufanya kazi, mengine yalikuwa yamefifia, sasa itabidi yafufuliwe ili yaweze kutimiza wajibu wake. Kwa hiyo, Mabaraza ya Kata yapo hayaanzishwi upya. Mabaraza yanayoanzishwa upya ni yale ya Vijiji ambayo nayo ndiyo zoezi limekwishaanza katika ngazi ya Vijiji.

Kwa hiyo, Wizara yangu na TAMISEMI, tutashirikiana na kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba mwaka huu lazima tufanye kazi ya ziada kuhakikisha kwamba Mabaraza haya ya Vijiji na ya Kata yanatekeleza wajibu wao ili sheria hii iweze kutekelezwa kuanzia ngazi ya chini kwenda juu. Kwa hiyo, hili tutaendelea kujitahidi na kwa kuwa matatizo yaliyokuwepo tumekwishayaondoa, nadhani mwaka huu wa fedha tutajitahidi kwenda kwa kasi zaidi kuimarisha na kuboresha Mabaraza katika ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kamati za Kugawa Ardhi katika Halmashauri zetu, hili tumejaribu kulieleza na tangu mwanzo tulilieleza tulipokuwa tunapitisha sheria hizi na kuanza mfumo huu mpya kwa mujibu wa sheria mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Kamati ni ya utendaji si ya kisera, ndio maana tuliona tuwaachie watendaji wenyewe wafanye hiyo kazi kukiwa na matatizo wanakwenda kwenye *Council* ambako ndiko Madiwani wapo wenye sera na hii Kamati itakuwa inatekeleza maamuzi ya kisera katika Halmashauri hiyo, hawawezi wakagawa maeneo bila kuzingatia maamuzi ya Halmashauri yao. Wakikosea, ndio wanarudi kwenye vikao na wanakalishwa chini kuweza kujieleza kwa nini hawakuzingatia maelekezo ya Madiwani.

Pamoja na hayo kuna Waheshimiwa Madiwani wawili, mmoja mwanaume na mwingine mwanamke kwenye hiyo Kamati. Ni ile kwamba tu sasa wenye *policy* waangalie Kamati inafanya kazi vipi. Kwa hiyo, tulidhani pengine muundo huo ndio utatusaidia zaidi kuliko tena kurudi kule nyuma kuingiza watu wengine. Kwa hiyo, mabadiliko yamekuja kwa maana hiyo na kwa mujibu wa sera na sheria mpya ambazo tunazitumia hivi sasa.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi zaidi ni hilo la mwisho alilouliza Mheshimiwa Omar Kwaangw', hili la Kamati ya Ugawaji wa Ardhi.

Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba hii ni Kamati ya utendaji sio ya sera, lakini katika utekelezaji siyo sahihi na sheria inavyosema. Mkurugenzi Mtendaji ndio Mwenyekiti, wapo kweli hawa Madiwani wawili na kwanza pale itifaki imekosewa, kwa sababu sio itifaki sahihi Mkurugenzi Mtendaji kuwa Mwenyekiti kwenye Kamati ambayo Diwani yupo. Hapo kwanza itifaki tumeshakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sasa hivi hiyo Kamati ndio inagawa ardhi na ndio ya mwisho, wala hawaleti taarifa kwenye Halmashauri. Kama ninyi Waheshimiwa Mawaziri mnaletewa kwenye Majimbo yenu, kwenye Majimbo yetu haileti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingine hawa wametumia nafasi hii kujigawia ardhi bila kupitia utaratibu. Tunajua ukitaka ardhi, unaomba kwanza kwenye Serikali ya Kijiji. Kuna kiwango cha ardhi ambayo hupewa na Mkutano Mkuu wa Kijiji, lakini hao hawafuati hivyo, kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi anajimegea tu. Kwa mfano, Mkurugenzi wangu amejikatia ekari mia tatu, tena kwa kuwanyang'anya wakulima wadogo wadogo kwa kutumia nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuwapa hawa watendaji kuwa wao ndio wanashikilia ardhi, hata likitokea lolote anajua kwamba atahamishwa, lakini Mwenyekiti wa Halmashauri angekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ugawaji wa Ardhi na wakawepo Madiwani, hawa wataogopa kumega ardhi wanavyotaka kwa sababu wanajua wanawajibika kwa wananchi moja kwa moja. Lakini huyu mtaalam anajua kesho ataondoka.

Kwa hiyo, napenda kupata maelezo kwa nini tusibadilishe Mwenyekiti wa Halmashauri awe Mwenyekiti wa Kamati ya Ugawaji Ardhi na wawepo Madiwani wasiopungua wanne? Kama atakuwepo Mkurugenzi awe kama mtaalam, kwa sababu limetokea hilo na mifano haipo na hilo limeshafikishwa kwenye ofisi ya *PCB* mtu kuwanyang'anya kwa kutumia madaraka yake ya Uenyekiti...

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Parseko Kone, imeeleweka.

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Kuwanyang'anya watu mashamba yao na kujilimbikizia yeye.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Parseko Kone, imeeleweka kwa sababu na Mheshimiwa Omar Kwaangw', alisema hivyo hivyo. Kwa hiyo, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maelezo yangu yatakuwa ni yale yale. Lakini ninachoomba na nasema siku zote matatizo ya watu binafsi yasiingilie kwenye mfumo wa uongozi na utendaji, maana yakiingia huko kwa kweli tutakuwa tunapata tatizo kila wakati. Hata ungebadilisha mfumo wa sasa kama ni matatizo binafsi bado yangekuwepo.

Kama Mkurugenzi Mtendaji ana tatizo kwa nini asishughulikiwe na Madiwani wana uwezo. Huyu ni mtumishi wao kwa hiyo, wana uwezo. Mimi nitashangaa kweli yaani Mkurugenzi Mtendaji anajifanyia mambo tu na Waheshimiwa Madiwani wapo, Mheshimiwa Mbunge upo, wananchi wanalalamika anakwenda tu! Haiwezekani. Hapo lazima kuna tatizo, sio tatizo la mfumo ni tatizo la watu. Basi tuwashughulikie watu katika matatizo yao, lakini mimi nadhani mfumo kwa kweli ni mzuri tu. Tukirudi kule nyuma, maana tumetoka huko na matatizo tuliyaona yalikuwa mengi tu. Sasa tunataka Madiwani wasimamie kweli sera zao na wadhibiti, wasijiingize tena kwenye matatizo ya kwamba wao wanajigawia viwanja. Tumeyaona hayo jamani, tumetoka huko na sasa tunataka kwenda mbele. *(Makofi)*

**MHE. PARSEKO V. KONE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hatugombani na hapa namsahihisha Waziri kwamba sio matatizo ya binafsi. Mheshimiwa Omar Kwaangw', ameeleza matatizo hayo hayo katika Jimbo lake, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanapiga makofi ni kwamba yapo hayo kwenye Majimbo yao. Kwa hiyo, hili sio suala la binafsi. Tuseme tu na Serikali pia iache kejeli ya kutukejeli Madiwani na Wabunge kwamba chukueni hatua hapo hapo kwa sababu mara nyingi tunaleta hata na ushahidi lakini inachukua miaka minne, mitano, ama kutofanyiwa kazi kabisa. Kwa hiyo, tuelezane kwamba huu ndio mfumo tulio nao sasa, lakini tuache kejeli ya kusema Madiwani na Wabunge mnaweza kuchukua hatua, mara ngapi tumeleta ushahidi na hatua hazikuchukuliwi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, huo ni ushauri wako na *statements* ambazo ume-*conclude.* Nadhani Waziri hana la kusema kwa hilo.

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... 604,590,200/=
Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 169,260,500/=
Kifungu 1004 - *Management Information System* ... ... ... ... ... 98,872,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Land Development* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 48,939,100/=

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Waziri kwa majibu ya hoja mbalimbali ambazo nilizitoa. Ila katika programu ya ishirini, *Land Development Services, Subvote 2001* kwenye *Land Development,* nilizungumza katika hotuba yangu asubuhi kitu kimoja ambacho ni *very specific* au lilikuwa ni tatizo la mgogoro wa ardhi kwenye sakata la shamba Na. 39 katika Kijiji cha Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo.

Hapa sijapata maelezo yoyote kuhusu suala hili juu ya hawa wanakijiji ambao kwanza waligawiwa hili shamba na baadaye Serikali ikamnyang'anya mmiliki huyu baada ya kushindwa kutekeleza maagizo ya sheria ya ardhi wakapewa na Kijiji kwa amri ya Mheshimiwa Rais na Waziri mwenyewe, lakini ni hivi juzi tu kama nilivyoeleza kwamba Afisa Ardhi wa Wilaya ya Bagamoyo katoa ushauri mpya kwamba shamba lile lote lirejeshwe kwa mmiliki wa awali wakati watu walipewa tokea mwaka 1997, wameshajenga nyumba, wana mashamba, kumejengwa Makanisa, kuna shule, lakini leo Afisa Ardhi huyu anataka shamba hili lirejeshwe kwa mmiliki wa awali na kwamba wananchi hawa wote ambao wanafikia mia moja wahamishwe. Hili bado sijapata maelezo.

**MWENYEKITI:** Mimi nilifikiri wakati anajibu ulikuwepo, amesema nimelipokea na nitalifanyia kazi. Lakini kwa sababu mwenyewe yupo acha nimpe nafasi.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nakushukuru kwa kunisaidia kujibu. Nilisema hivyo, Mheshimiwa Ali Said Salim, jana aligawa hotuba yake kama Msemaji Mkuu wa Upinzani, katika hotuba yake ya jana hilo alilolisema halikuwemo, lakini asubuhi hii amenieleza analolizungumza na mimi nimejibu kwamba kwa kuwa tumepata leo, basi tupe muda tulifanyie kazi, tukimaliza tutakujibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Survey and Mapping* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 863,030,800/=

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimetoa ombi kwa Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi juu ya Vijiji hususan kuhusu Vijiji ndani ya Jiji la Dar es Salaam na hii ni kwa sababu katika kiambatisho "G" cha hotuba yake inaonekana kwamba hakuna Vijiji ndani ya mipaka ya Jiji la Dar es Salaam na mimi kwa mujibu wa kazi ninayofanya najua kuna *Government Notice* ambayo inasema hivyo.

Lakini katika Jiji la Dar es Salaam hususan Wilaya ya Kinondoni na hasa Jimbo la Ubungo na Jimbo la Kawe na maeneo ya Kata ya Kunduchi na Kata ya Kibamba kuna watu wanaojiita Halmashauri za Vijiji na wamejichukulia madaraka ya kutwaa maeneo ya ardhi zinazomilikiwa na watu na kuzigawa au kuziuza kwa watu wengine.

Hii imetokea Kibamba, Jimbo la Ubungo na imetokea Madale Jimbo la Kawe, sasa ninavyojua mimi kisheria hakuna Vijiji kwenye maeneo haya. Hawa watu wamediriki hata kutoa karatasi ambazo wanaziita ni hati za kumiliki ardhi za Vijiji. Sasa nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko juu ya hii tabia ya watu kutwaa maeneo ya watu na kuyagawa kwa watu wengine na msimamo wa Wizara kuhusiana na jambo hilo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijibu la jumla tu kwamba mwelekeo ni kwamba katika Miji yetu hatutakuwa na Vijiji. Kwa hiyo, TAMISEMI wanaendelea kufuta Vijiji vyetu ambavyo vilikuwa ndani ya Miji na kwa Dar es Salaam hivyo hivyo. Kwa hiyo, tutashirikiana na TAMISEMI kufuatilia hili ambalo amelisema ili tuweze kulidhibiti kwa mujibu wa sheria.

**MHE. DR. MASUMBUKO R.M. LAMWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu zuri la ujumla, nini msimamo wa Wizara juu ya hali ya namna hiyo kwamba watu wanatwaa ardhi na wanatoa hati za kumiliki ardhi za Vijiji ndani ya Jiji la Dar es Salaam na *status* ya huo mgao ambao umeshatolewa, wale wanaogawiwa na wale wanaonyang'anywa haki zao, nini msimamo wa Wizara?

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, anafahamu jibu kwamba, sheria na taratibu zipo, kama hazifuatwi ni kosa au kama hawafuati sheria na taratibu zilizopo ni kosa, hawana mamlaka ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyombo vyenye mamlaka chini ya sheria zilizopo. Sasa kama watu wanajichukulia madaraka ambayo sio yao, ni makosa, hawapaswi kufanya hivyo na ndio maana nikasema tutafuatilia. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2003 - *Customary Land Tribunal* ... ... ... ... ... ... ... 224,104,000/=
Kifungu 3001 - *Human Settlements Development* ... ... ... ... 867,688,500/=
Kifungu 3003 - *Building Research Unit* ... ... ... ... ... ... ... 617,992,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... ... ... 73,000,000/=
Kifungu 1004 - *Management Information System* ... ... ... ... 210,000,000/=
Kifungu 2001 - *Land Development* ... ... ... ... ... ... ... ... ... 160,000,000/=
Kifungu 2002 - *Survey and Mapping* ... ... ... ... ... ... ... ... 230,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2004/005, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge, ningependa tu kuwataarifu kwamba, kutokana na msiba mkubwa ambao umetupata, nadhani kwa hivi sasa mnafahamu, zile shughuli ambazo zilipangwa kwa *weekend* hii zote zimefutwa na zimepangiwa wiki ijayo. Hii ni pamoja na Usiku wa Mwanamke wa Kitanzania na zile mbio ambazo zilipangwa kwa kesho za *VIP Race,* kwa hiyo, havitakuwepo kwa *weekend* hii kutokana na msiba huo.

Baada ya taarifa hiyo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.55 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 26 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*